

## **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 1 Julai, 2009**

*(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua*

**TAARIFA YA SPIKA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hapa Mezani kwangu nina taarifa mbili za Spika. Kwa mujibu wa Kanuni Na. 33 (1) ya Kanuni za Kudumu za BUnge, toleo la Mwaka 2007, ninaomba niwape taarifa zifuatazo:-

Waheshimiwa Wabunge, taarifa ya kwanza katika Mkutano wa 16 wa Bunge unaoendelea, Bunge lilipitisha Miswada miwili ya Sheria ya Serikali iitwayo, “*The Executive Agencies Amendments Bill, 2009*” na “*The Finace Bill, 2009*”. Waheshimiwa Wabunge, mara baada ya kupitishwa Sheria hizo na Bunge na baadaye kupitia katika hatua zake zote za uchapishaji, Miswada hiyo ilipelekwa kwa Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili ipate kibali chake rasmi na iweze kutumika.

Kwa Taarifa hii Waheshimiwa Wabunge, napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba tayari Mheshimiwa Rais, ameshatoa kibali chake na sasa Miswada hiyo ni sheria za nchi na zinaitwa, “*The Executive Agencies Amendment Act No. 13, 2009*.” Na “*The Finance Act, No. 14, 2009*.”

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo hiyo kwa taarifa ni kwamba Sheria hizi sasa zitaanza kutumika kama Sheria kamili katika nchi yetu. Naomba niwashukuruni wote kwa kufanikisha hilo na tunamshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kumaliza kazi yake.

Waheshimiwa Wabunge, taarifa ya pili ni Hati za Kuwasilishwa Mezani na Wizara ya Miundombinu. Waheshimiwa Wabunge, taarifa zifuatazo hazikuweza kuwasilishwa Mezani leo asubuhi, kwa sababu utayarishwaji wake bado haujakamilishwa. Kwa sababu hiyo ninaomba na ninapenda kuwaarifu kwamba taarifa hizo zitawasilishwa Mezani kesho Alhamisi, Tarehe 2 Julai, 2009 asubuhi, hapa ndani ya Ukumbi wa Bunge. Na taarifa hizo ama hati hizo ni za utekelezaji juu ya masuala yafuatayo:-

1. Uendeshaji usioridhisha wa Shirika la Reli Tanzania, unaofanywa na Kampuni ya *RITES* ya India.
2. Utendaji wa Kazi usioridhisha wa Kampuni ya *Tanzania International Container Terminal Services, TICTS*.
3. Taarifa ya uuzwaji wa nyumba za Serikali.

Kwa hiyo, ninaomba niwape taarifa kwamba Hati hizo za utekelezaji zitawasilishwa kesho tarehe 2 Julai, 2009 ndani ya Ukumbi wa Bunge.

Katibu tuendelee na *Order Paper*.

### **HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge baada ya kupokea taarifa za Spika, sasa tutaendelea na Hati za Kuwasilishwa Mezani. Hati ya ya kwanza ni ya Waziri wa Miundombinu. Mheshimiwa Naibu Waziri.

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

#### **NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010. Naomba kuwasilisha.

#### **MHE. MOHAMED H. MISANGA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/2009 pamoja na maoni ya kamati kuhusu Makadirio na Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

#### **MHE. JUMA SAID OMAR K.n.y. MHE. KABWE Z. ZITTO – MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Msemadi Mkuu wa Kambi ya Upinzani Mpango na Makadirio ya Wizara ya Matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

#### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA:**

Taarifa ya Hali ya Mazingira Nchini kwa Mwaka 2008 [*State of Environment Report, for the year 2008*].

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 139

### Uwakilishi Sawa wa Wanawake na Wanaume Bungeni

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Ilani ya Uchaguzi ya CCM inasema wazi kuwa, ifikapo mwaka 2010 kutakuwa na uwakilishi wa asilimia 50/50 kati ya Wanaume na Wanawake Bungeni; na kwa kuwa, suala hili limebadilishwa na kuwa asilimia 50/50 kwa Majimbo yaliyopo 232 ambapo nusu yake ni 116 na kama wanawake watashindwa katika Majimbo yote ina maana wanawake watakuwa ni 30.2%.

Je, kwa utaratibu huu Serikali ya Chama cha Mapinduzi haioni kuwa imeshindwa kutekeleza ahadi yake hiyo:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kumjibu Mheshimiwa Susan Lyimo, swali lake kama kama ifuatavyo:-

Lakini kabla sijajibu swali hilo, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Susan Lyimo pamoja na wenzake wa upande huu kwa kusoma kwa umakini na kuelewa vizuri ilani ya Chama Tawala. Kama ulivyosema badiliko alilofanya halileti tofauti yoyote. (*Makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba kwa mujibu wa Ibara ya 120 (a) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005, Chama Cha Mapinduzi kiliahidi ifuatavyo, na ninanukuu:-

*“CCM itazielekeza Serikali kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali za uongozi wa kisiasa, kiutendaji na nafasi za maamuzi kwa lengo la kufikia asilimia 50 ifikapo mwaka 2010 kama ilivyokwisha azimiwa na Umoja wa Afrika.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia ahadi hii ya Chama cha Mapinduzi siyo kweli kwamba Serikali ya CCM imebadilisha muelekeo wake au haitekelezi ahadi zake, bali ni kwamba utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi bado unaendelea nab ado azma ya Serikali ya kutekeleza Sera za Chama Tawala ipo vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba kwa kuzingatia Ibara ya 120 (a) ya Ilani hiyo, *CCM* tayari imewasilisha mapendekezo yake Serikalini ya namna ya kuongeza uwakilishi wa Wanawake kufikia asilimia 50. Serikali zote mbili, Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, sasa zinafanya kazi na wananchi watajulishwa hatua ya utekelezaji wa mapendekezo hayo.

Aidha, napenda kutoa wito kwa Vyama vya Siasa vyote kuona umuhimu wa kutoa elimu kwa Umma ili kuwawezesha wanachama wetu kutafsiri vema Ilani za Vyama vyao wakiwemo Waheshimiwa Wabunge ili tufikie azma hii ya asilimia 50/50 katika eneo hili la uwakilishi.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa, Ilani ndio mwongozo pamoja na Sera ya Chama. Na kwa kuwa, Chama kinachopata ridhaa ya kuongoza basi Ilani yake hutekelezwa na wananchi wote bila kujali itikadi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Waziri anaweza kuliambia Bunge hili ni kwa nini katika mchakato huu Viongozi wa Vyama vingine hawakushirikishwa au wadau wengine na badala yake wakashirikishwa watu wa *CCM* peke yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swal la pili. Kwa kuwa, ile dhana ya “*Ukimwelishwa Mwanamke Umeelimisha Jamii*” na vilevile mwanamke akiwezesha anaweza sana tena kwa ufanisi. Na kwa kuwa, dhana hii imejitokeza wazi pale ambapo tunaona wanawake wengi wakipewa madaraka ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge, wanafanya vizuri.

Lakini zaidi tukiangalia mifano kule Rwanda na Rais wa Kwanza Mwanamke pia ametoka Afrika. Je, Serikali sasa ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba wanawake hasa katika uchaguzi unaokuja wa Serikali za Mitaa na uchaguzi ujao wa Wabunge, basi wanawake wanawezeshwa na hivyo kuweza kushiriki katika chaguzi hizo na kushinda? Serikali ina mikakati gani? (*Makofî*)

#### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Susan Lyimo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ushirikishwaji. Napenda kusema kwamba si muda mrefu sana toka tumpata maelekezo ya kutekeleza haya ambayo yalikuwa kwenye Ilani kwa ukamilifu zaidi kutoka Chama cha Mapinduzi. Na mchakato wenyewe unachkua sura tatu; sura ya kwanza ni kutekeleza masharti ya Katiba ambayo inatakiwa sasa Mkurugenzi wa Uchaguzi kuamua kwasababu mwaka wa 10 umefika hajagawa Majimbo, anatarajia kugawa Majimbo mangapi ya Uchaguzi ambayo yako wazi kwa wanaume na wanawake.

Mchakato wa pili, utahusu nafikiri Tume ya Utumishi wa Bunge, Kamisheni ya Bunge, kuona ni namna gani ukumbi huu utapokea Wabunge watakaoongezeka, kwa sababu Ukumbi huu nao una ukomo wake, nadhani sio zaidi ya Wabunge 360. Na mwisho Serikali, hasa Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Fedha, kuangalia ni namna gani uchumi wa nchi unaweza kubeba uendeshaji wa Bunge. Kwa maana nyingine uchumi wa nchi kwa miaka 10 ijayo unaweza kubeba Wabunge kiasi gani.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Chama cha Mapinduzi kimetekeleza Ilani yake ya 50/50 kwenye Chama na hivi sasa iko katika mikakati ya kufikia 50/50 kwenye nyadhifa mbalimbali. Na kwa kuwa, kwenye Bunge na Madiwani asilimia 50/50 si lazima iwe Viti Maalum tu. Je, kuna mikakati gani hao Wabunge pia waingie kwenye majimbo na madiwani waingie kwenye Kata? (*Makofit*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nijibu Sali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubaliana naye kwa asilimia 100. Kwa kweli utaratibu wa Viti Maalum si utaratibu mzuri sana na wala sio wa kidemokrasia.

Kwahiyo lazima vyama vyaya siasa na jamii iwahamasishe wanawake wagombee katika ngazi zote kuanzia Vitongoji na Mitaa, Serikali za Vijiji, Udiwani, Ubunge na hata Urais. Na ndivyo ilivyofanyika kwa wenzetu ambao wamefikia asilimia 50 hasa kwa nchi za Scandinavia. Kwahiyo mimi nakubaliana naye kabisa kwamba sio lazima asilimia 50 ifikiwe kwa kuwa na Viti Maalum, kwasababu Viti Maalum kwa kweli ni utaratibu ambao kwa sasa sio utaratibu mzuri sana na hasa kwa nchi ambayo Katiba yake haina ile Demokrasia ya uwiano kwa maana ya *proportional representation*, katika Katiba yetu hakuna *proportional representation*. (*Makofit*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hili la Viti Maalum limetumbukia tu, lakini kwa hakika haikutangazwa au haikuelezwau kufafanuliwa moja kwa moja katika Katiba.

Kwa hiyo pia katika mchakato huu kama tukitaka kuhalalisha kabisa Viti Maalum, basi nayo ionekane kwenye Katiba kuliko ilivyo sasa ambapo ni dhamira ya vyama kuona kwamba haki inatendeka. Na kwa hili ni lazima nikisifu sana Chama cha Mapinduzi kwa kutenga asilimia 30 kwa Viti Maalum tena kwa njia ya haki kabisa. Kwa utaratibu ulio wazi na hauna manung'uniko kuliko ambavyo tunapata manung'uniko kutoka kwa wenzetu wengine kuanzia tulipoanza utaratibu huu mwaka wa 1995. (*Makofit*).

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA K.n.y. MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Jimbo la Mbinga Mashariki ni kubwa sana na hivyo hali hiyo kuathiri kasi ya ukuaji wa maendeleo kwa wananchi:-

Je, Serikali haioni kuwa, ni vema sasa ikaligawa Jimbo hilo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nimjibu Mheshimiwa Gaudence cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara ya 74 (6) (c), Tume ya Taifa ya Uchaguzi ndiyo yenye mamlaka ya kuchunguza mipaka na kuigawa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya Uchaguzi wa Wabunge. Aidha, Ibara ya 75 (1) na (4) ya Katiba hiyo imeipa Tume ya Uchaguzi mamlaka ya kuchunguza Majimbo mara kwa mara angalau kila baada ya miaka kumi, kwa namna itakavyoamuliwa na Tume yenye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sehemu ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeshaanza mchakato wa matayarisho ya kufanya uchunguzi wa mipaka ya Majimbo mbalimbali kwa kukusanya takwimu kama vile idadi ya watu, upatikanaji wa mawasiliano, hali ya kiuchumi kwa kila Jimbo na kufanya utafiti katika nchi mbalimbali ili kujuua Vigezo na jinsi nchi hizo zinavyotekeleza zoezi la ugawaji wa Majimbo.

Kwa mara ya mwisho itakumbukwa kwamba hapa nchini Majimbo ya Uchaguzi yaligawanywa mwaka 1995 kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara 75 (3) vya upatikanaji wa mawasiliano na hali ya kijiografia ya eneo linalokusudiwa kugawanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya Uchaguzi itaainisha vigezo vipya vitakavyotumika katika ugawaji wa Majimbo na kuwatangazia wananchi na wadau mbalimbali ili walete maombi na mapendekezo yao.

Maombi na mapendekezo hayo yatafanyiwa uchambuzi na Tume kuona kama yatakidhi vigezo vilivyowekwa ili kufikiriwa kugawanywa au kurekebishwa mipaka ya Majimbo hayo. Aidha itakapofika wakati huo wadau katika Jimbo la Mbinga Mashariki nao watakaribishwa kuleta maombi yao na kama yatakidhi vigezo hivyo basi Jimbo hilo linaweza kugawanywa au kurekebishwa mipaka yake.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini katika kuleta msisitizo na kwa kuwa, suala hili linakabili majimbo mengi ya Tanzania, hususan

Mbinga Mashariki. Mbinga Mashariki, peke yake ina Kata 24 na ina wananchi wanaozidi 400,000 na hata namna ya kuzifikia Kata hizo ni tatizo kubwa ikizingatiwa kwamba Jimbo la Mbinga Mashariki, ndilo linaongoza kiuchumi katika nchi hii na hivi inastahili sana Mbunge wake kuwafikia wapiga kura wake ili kuwahamasisha katika maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Jimbo hili litapewa kipaumbele cha kwanza? Vilevile Mheshimiwa Waziri Mkuu, atakubaliana nami kwamba Majimbo yale ambayo yana jiografia kubwa ya kuyafikia ndiyo mengi yapo nyuma kimaendeleo kwa sababu ya kutokuwa na Wabunge wao mara kwa mara kwa ajili ya ugumu wa kuwafikia? (*Makofi*).

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kumjibu Mheshimiwa Stella Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum, Ruvuma, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekubaliana na yote aliyoyasema, hasa pale aliposema kwamba Majimbo mengi yana sifa ya kugawanywa na maombi ni mengi. Na ninasema ningependa kutaja hapa kwamba hadi sasahivi tunapoongea maombi ya kugawa Majimbo ni 78. Na nirejee kusema yale ambayo niliyasema nilipokuwa ninamjibu Mheshimiwa aliyeuliza swali pale awali kwa kusema kwamba kugawa Majimbo kutategemea mambo matatu muhimu; uwezo wa nchi kubeba ukubwa wa Bunge, utekelezaji wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano, lakini pia uwezo wa Ukumbi wetu Huu kubeba au kuchukua Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikiwa Naibu Spika, kati ya 1995 na 2000 tumechambua michoro ya awali ya jingo hili na tulifikiri kwamba katika muda wa miaka kati ya 50 na 100, itakuwa ikipokea kati ya Wabunge 360 na 380. Na hii ikumbukwe ni pamoja na kuondoa baadhi ya hizi *corridors* munazoziona. (*Makofi*).

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yaliyozungumzwa ya Mbinga Mashariki, yanafanana na yaliyopo Iramba Magharibi, sasa swali langu ni dogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako Majimbo ndani ya nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yana watu 1000 na yapo Majimbo yana watu 400,000; hivi hawa *NEC* ni vigezo gani wanavyovitumia hasa kuweza kugawanya Majimbo yakawa na tofauti ya Idadi kubwa sana ya watu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kumjibu Mheshimiwa Juma Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio tu kwamba kuna Majimbo yana watu chini ya 10,000 na Majimbo mengine yana watu zaidi ya 700,000.

Narudia, kuna Majimbo mengine katika nchi yetu yana watu chini ya 10,000 kuna Majimbo mengine yana watu zaidi ya 700,000 na nadhani Kahama imekaribia, nadhani Bukombe imekaribia kiwango hicho pia. Sasa jibu ni kwamba hii imetokana na historia ya nchi yetu. Tanzania ni Jamhuri ya Muungano na katika yale makubaliano ya Muungano ambayo yamesemwa hapa jana nayo yana sehemu yake katika kuhakikisha kwamba kuna eneo lina wawakilishi pamoja na kwamba watu wake ni wachache. Kwa sababu wanaiwakilisha iliyokuwa nchi, ikaungana na nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa ufupi hili linatokana na historia yetu kwa sababu ni historia ya Bunge la nchi mbili zilizoungana. Na kwa ajili hiyo ni lazima kuwe na uwiano ambao unakidhi haja ya histioria hiyo.

Nimalizie tu kwa kusema kwamba kwa maombi hayo 78 tuliyokuwanayo na kwa uamuzi wa Chama cha Mapinduzi, kuongeza Wabunge wapya; kwanza 26 wanawake na 13 vijana, kwa hiyo tusijidnaganye kwamba tutapata majimbo mengi sana.

Tume ya Uchaguzi ina changamoto kubwa sana kuchambua maombi hayo 78 ili kukidhi kupata Majimbo machache angalao kukidhi zile haja tatu za Ukumbi wetu huu ambao hauwezi kupanuka sana, uchumi wa nchi, lakini pia kukidhi masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Na. 141

### **Wilaya Ya Mbinga Kupewa Bajeti Ndogo**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Mbinga ni Wilaya kubwa yenyewe watoto wengi na ina eneo kubwa Kijiografia; na kwa kuwa, Wilaya hiyo imepewa bajeti ndogo ukilinganisha na hali halisi:-

- (a) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa, hiyo inaweza kuwa ni chanzo kimojawapo cha ufanisi mdogo?
  
- (b) Je, ni hatua zipi zitachukuliwa ili kuondoa tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge amezungumzia Bajeti ya Wilaya ya Mbinga. Kwa hali halisi katika wilaya kuna Bajeti ya ofisi ya mkuu ya Wilaya na Bajeti ya Halmashauri. Kwa mujibu wa dhana ya kupeleka madaraka ya umma kwa wananchi kwa maana ya *D by D* miradi ya maendeleo uratibiwa na kusimamiwa na mamlaka za Serikali za mitaa kwa maana ya Halmashauri za Wilaya na miji. Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ipo kwa ajili ya *cheques and balance* ni dhahiri kwamba Mheshimiwa Mbunge alikuwa na maana ya bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, ndiyo msingi wa majibu nitakayotoa hapa.

Bajeti ya Halmashauri uandaliwa na Halmashauri yenye we kupitia mipango shirikishi, utaratibu wa kuibua miradi kwa kuzingatia mfumo wa fursa na vikwazo kwa maendeleo yaani *O* and *OD* hutumika na vipaumbele huwekwa kwa kuzingatia kiasi halisi cha fedha kilichotengwa na ukomo wa Bajeti yaani *ceiling*. Ili kupata ufanisi katika miradi ya maendeleo inayoendeshwa katika mamlaka ya Serikali za mitaa, ikiwa ni pamoja na Halmashauri za wilaya ya Mbinga rasilimali zinazopelekwa zinapaswa kusimamia kikamilifu ili kupata thamani halisi ya fedha yaani *value for money*. Aidha, ni muhimu vigezo vya kimataifa vinavyotakiwa katika miradi mbalimbali vikazingatiwa ikiwa ni pamoja na na kuzingatia sera, sheria, taratibu kanuni na miongozo ya kisekta.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwa ruzuku inayotolewa kwa Halmashauri nchini haikidhi mahitaji yote, kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoamuliwa katika ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 MKUKUTA na mipango ya kila mkoa na Halmashauri, Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo, katika sekta za kilimo, afya, kilimo, maji na barabara. Fedha za kugharamia miradi ya maendeleo zimekuwa zikitengwa kwa kila sekta kwa kuzingatia uwiano maalum wa fomula kwa kutumia vigezo vilivyowekwa. Ili kuleta uwiano sawa vigezo hivyo ndivyo pia hutumika kwa Halmashauri nyingine Bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbiga imekuwa ikiongezeka kwa awamu mwaka hadi mwaka.

Kwa mwaka 2009/2010 Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga imetegewa shilingi bilioni 10.4 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ikilinganishwa na shilingi bilioni 2.3 kwa mwaka 2006/2007

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwanza nishukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ambayo naamini pamoja na majibu haya bado atazingatia kuwasaidia wilaya ya Mbinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala alilojibu amesema kwamba kuna vigezo ambavyo vinazingatiwa, na kwa utafiti wangu nimegundua kwamba vigezo hivyo vimepitwa na wakati, kwa sababu havikujali hali halisi ya mazingira, kwa mfano hasa kwa upande wa masuala ya kiutawala katika elimu.

Wizara ya Elimu inatambua *taste knowledge* inachangia kidogo sana ukilinganisha na *experiential knowledge*. Sasa kama inapotokea walimu pamoja na

wanafunzi hawaoni kwa vitendo masuala ya kiukaguzi yakiendelea kutokana na ugumu wa Bajeti hizo ni tatizo.

Mheshimiwa Waziri utakubaliana nami iko haja ya kufanya *review* ya hivyo vigezo ili kuweza kukidhi hali halisi ya matatizo ya wilaya kama hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mambo ya msingi ambao ningetaka wote tuelewane hapa ili niweze kuliweka hili vizuri jinsi linavyouulizwa. Ni kwamba Bajeti ya kwetu hii tunayoipitisha hapa inaitwa bajeti tegemezi ni bajeti ambayo *pump* yake ya kuiendesha hiyo Bajeti inategemea pia nguvu za nje imeshuka kutoka asilimia 40 imekuja kwenye asilimia 35 na wenzetu wa fedha wako hapa wanafahamu hilo jambo.

Kwa hiyo, ni bajeti ambayo huwezi kujidai sana ukasema nina nguvu ya kuendesha mimi mwenyewe kwa sababu asilimia 40 inatoka nje na ile ya ndani ndiyo ya kwako.

Sasa kwa vigezo amezungumza habari ya elimu, hapa tunazungumza habari *capitation* kinachofanywa hapa kama unazo shilingi milioni 10 kwa Tanzania nzima unahesabu watoto wote ambao wana umri wa kwenda *primary school*, unajua kwamba wako hawa unawachukua wale watoto unagawanya hizo shilingi milioni 10 kwa idadi ya watoto ulionao.

Unaona kwamba kila mtoto mathalani atapata shilingi 3 unachukua Mbinga, unasema wako watoto wangapi anasema mimi ninao watoto elfu moja unachukua elfu moja unazidisha mara tatu, unakwenda Kilimanjaro pale Siha unakuta kuna watoto 700, unachukua 700 unazidisha mara 3000, ndivyo unavyofanya kwa *NGO* kwa hiyo ukimaliza pale hela imekwisha, kwa sababu utachukua hela iliyopatikana pale na yeze anazungumza.

Mheshimiwa Manyanya anazungumza jambo la msingi sana hapa mimi nimesema hivyo tu ilikuonyesha *dilemma* ambayo Serikali ina-face katika kugawana hizi hela, hakuna hela ambazo zinatoka nje ya hizi ambazo tunazipitisha hapa.

Lakini anachosema hapa ni kwamba yako mambo ambayo kwa kweli lazima uyaangalie zaidi hapo. Na ndiyo maana katika Bajeti hii tumeanza kuzungumza sasa maeneo ambayo yana matatizo maalum na haya yote anayazungumza ambayo ameyaeleza hapa ni mambo ambayo ya msingi na ya kuzingatia. Kwa hiyo, nataka kukiriki hapa niseme kwamba tutafanya hivyo kama anavyoshauri lakini sasa itazingatia pia kwamba ni kiasi gani pesa ambacho tunacho.

Hata hivyo nichukue nafasi hii kuipongeza sana Wilaya ya Mbinga, mimi nimekwenda mpaka Mbinga wanafanya kazi nzuri sana hawa ni wachapa kazi wa hali ya juu na yeze mwenyewe mmemsikia anazungumza hapa wanapanda kahawa wakati

nakwenda nilikuta miche ya kahawa milioni 4 mipyä kupitia takri ndiyo wanalima pale.

Lile ni eneo ambalo linaweza likajilisha lenyewe pale likajiendesa lenyewe. Kwa hiyo, niko tayari kukaa naye tuzingatie haya kwa pamoja. Pia nataka nichukue nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Mbanga kwa kazi nzuri wanayofanya. (*Makofi*)

Na. 142

### **Fedha Zilizokusanywa na TRA Kupelekwa Wilaya Husika**

**MHE. RAYNALD A. MROPE** aliuliza:-

Kwa kuwa, wakati wa Bunge la Bajeti la Mwaka 2008/2009 Serikali iliahidi kwamba asilimia 6.5 ya Fedha zilizokusanywa na TRA kuhusu *Export Levy* ya mauzo ya nje ya korosho zitapelekwa moja kwa moja katika wilaya husika iliyozalisha zao hilo.

- (a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimepatikana kuanzia mwaka 2005 hadi sasa?
- (b) Je, ni fedha kiasi gani zilipelekwa kwa wilaya za Masasi, Newala Tandahimba na Mtwara?
- (c) Je, kwanini Serikali inachelewesha mno malipo ya fedha hizo ambazo Halmashauri zingetumia kuboresha zao hilo na maendeleo ya Wilaya?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge wa Jimbo la Masasi lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ushuru wa mauzo ya nje ya korosho ghafi unatozwa chini ya sheria ya Bodi ya korosho sura za 203 kufuatia marekebisho yaliyofanywa kupitia sheria ya fedha, 2006. Kuanzia Julai, 1, 2006 Mamlaka ya Mapato Tanzania, ilipewa jukumu kisheria la kukusanya kodi hiyo ambayo inatozwa kwa kiwango cha asilimia 10 na kugawanya kama ifuatavyo:-
  - (i) Asilimia 6.5 hupelekwa bodi ya korosho na kugawanywa kwa wilaya zinazozalisha korosho.
  - (ii) Asilimia 3.5 hupelekwa kwenye mfuko mkuu wa Serikali (*Consolidated Fund*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka 2006 baada ya sheria kufanyiwa marekebisho hadi mwisho wa mwaka 2008, jumla ya shilingi 11,817,759,350.20,

zilikusanywa na mamlaka ya mapato kutokana na ushuru wa mauzo ya korosho ghafi nje ya nchi na shilingi 7,681,533,577.78 zililipwa kwa bodi ya korosho kwa mujibu wa sheria.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha malipo kilicholipwa Halmashauri kilitokana na kurekebishwa kwa sheria ya bodi ya korosho ambapo malipo yalifanyika kama ifuatavyo katika ile asilimia 10, 0.25 asimilia - Halmashauri, 0.25 asilimia - Bodi ya Korosho, 0.1 asilimia - kuendeleza *Research Station*, 5 asilimia - Kuendeleza zao la Korosho, 3.5 asilimia - Mfuko Mkuu wa Serikali.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua malengo ya malipo haya juhudii kubwa hufanywa kuhakikisha malipo yanafanyika punde mauzo ya korosho yanapokamilika. Hata hivyo, taratibu za malipo zinaitaka Hazina kulipa katika mwaka huo huo wa fedha na hili linafanyika.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kujibu swalii hili na kama kawaada yake huwa anajibu vizuri. (*Makofii*)

Lakini nataka kutokubaliana naye kwamba sheria ile ya *export levy* na kama jibu la maswali haya ningkuwa nimepewa jana ningeweza kumuonyesha hii sheria lakini kwa bahati mbaya nimepata hii asubuhi. Kwa hiyo sheria hii ya *export levy* inasema kwamba fedha hizi za asilimia 6.5 zilipwe moja kwa moja kwenye Halmashauri, Wilaya zile ambazo zimelima korosho. Na swalii langu limeuliza kwamba ni kiasi gani cha fedha zimekwenda katika wilaya za Masasi, Newala, Nanyumbu, Tandahimba na kadhalika. sasa mbona Waziri hajajibu hili?

Pili, sheria hiyo anayoisema imerekebishwa ililetwa lina hapa Bungeni tukaijadili na kuirekebisha kiasi kwamba kwa kweli watu wa mikoa hii inayolima korosho imepata balaa kubwa kabisa hakuna maendeleo yoyote kwa sababu ya zao hili kutopata ile *export levy*? (*Makofii*).

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mrope kwamba mimi sio mtaalam wa sheria lakini nimesoma sheria, na nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mrope tukimaliza kikao hiki tukae pamoja nimuonyeshe sheria inavyosema.

Lakini nataka nimwambie Mheshimiwa Mrope, Halmashauri zinazozalisha korosho ziko nyingi na kazi ya TRA ni kukusanya zile fedha kuzipeleka Hazina, na Hazina kazi yake kumpelekea chombo ambacho kitagawa kwenye Halmashauri hizo na chombo ambacho kilichoainishwa katika ile sheria ni bodi ya korosho. Nataka nimhakikishie hilo kwamba hili lipo na tutamuonyesha sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza katika jibu langu la msingi sheria hii ilifanyiwa marekebisho na Bunge lako Tukufu mwaka 2006 ikaipa mamlaka *TRA* kukusanya kodi hizi, hapo awali ilikuwa *TRA* haik 1 JULAI, 2009usanyi kodi hizi.

Lakini vilevile nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mrope katika jibu B nadhani hakulifahamu vizuri tu nilijibu kwamba Halmashauri inapewa 0.25 hizo Halmashauri zinazopewa 0.25 percent ya ile kumi na hapa ipo *amount* yote atoe tu yeze atajua Halmashauri hizo alizozitaja zitapata kiasi kiasi gani. Kwa hiyo liko hapa na limejieleza vizuri tu. (*Makofī*)

**MHE. ANNA MAGRETH ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, Waziri atakubali kwamba badala ya kukaa na Mheshimiwa Mrope tu, jambo hili tulijadili tukishakuzungumza, akishazungumza na Mheshimiwa Mrope, lije tena hapa Bungeni kwa sababu tafsiri anayoisema Waziri sivyo ilivyo kwa mujibu wa sheria?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na yeze kwamba tuilet sheria tena Bunge ili tuweze kuiona sote na kama kuna marekebisho tuweze kuifanyia kazi kwa pamoja. (*Makofī*)

Na. 143

#### **PSPF Kuikopesha Serikali**

**MHE. MOHAMMED RISHED ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa, *PSPF* imeikopesha Serikali shilingi 75 bilioni kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na kwamba hilo ni deni hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2008.

- (a) Serikali italipa vipi deni hili na kwa mchanganuo upi?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa utaratibu wa kukopa *PSPF* ni sawa na kuliua shirika hilo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Rished Abdallah, Mbunge wa Jimbo la Pangani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikidhamini Taasisi na Mashirika mbalimbali ya Umma hasa yale yanayotoa huduma zinazogusa jamii moja kwa moja au

kwa njia moja au nyingine. Dhamana hutolewa pale Serikali inaporidhika kwamba kwa wakati huu, hakuna namna nyingine kwa taasisis au shirika kujkwamua kifedha ili kuendelea kutoa huduma husika.

Kwa msingi huo, Serikali mnamo Februari, 2006 hadi Februari, 2007 iliidhamini bodi ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, kukopa kutoka mfuko wa pensheni kwa watumishi wa umma, jumla ya shilingi 53.00 bilioni. Kiwango hicho cha fedha kilitakiwa kulipwa katika kipindi kisichozidi miaka miwili (2). Kutokana na kwamba mkopo huo kuwa na riba na tozo, hadi kufikia mwezi Juni, 2008 mkopo uliongezeka hadi kufikia shilingi 68.60 bilioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa bodi ya mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu walikubaliana na Mfuko wa *PSPF*, baada ya Bodii kuchelewa kulipa fedha hizo kwa wakati, fedha hizo zilipwe kwa ukamilifu ifikapo tarehe 30 Juni, 2009.

Hata hivyo, hadi kufikia Juni, 2009, fedha zilizolipwa ni sh. 13.90 bilioni ambazo ni malimbikizo ya riba na tozo tu. Kutokana na bodi kushindwa kulipa salio la mkopo huo kwa wakati, Serikali kama mdhamini, itaangalia taratibu zinazofaa za kurejesha fedha hizo kulingana na mkataba wa mkopo na udhamini.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, kukubali kwa mfuko wa *PSPF* kukopesha Taasisi za Umma haina maana kwamba mfuko huo utakufa, kwani mkopo huu umedhaminiwa na Serikali, na kwa njia hii, mfuko wa *PSPF* unapata faida ya uhakika kwa njia ya riba na hivyo kujiongezea mapato.

Suala la msingi ni kwa vijana wetu kupata elimu ya juu na wajibu wa vijana wetu ni kuhakikisha wanarejesha mikopo hiyo mara tu wanapopata ajira.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, bodi ya mikopo navyofahamu haitozi riba inachokopesha ndiyo zilezile zinazorudi kutoka kwa wanafunzi. Lakini vilevile vijana wengine hawarudishi mikopo lakini vilevile *centre* ya ajira kwamba mwanafunzi amemaliza anapangiwa akafanye kazi wapi, huoni bado Serikali itaendelea kubeba mzigo kutokana na mfumo wenyele ulivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Serikali itakubaliana na mimi kwamba sasa hivi kuwe na utaratibu wa kutangaza *scholarship* tupate vijana katika fani ambazo ni *priority* kwa maendeleo ya nchi yetu hatimaye uwezo wa Serikali ijue kwamba tunatoa *scholarship* ngapi na hatimaye watangaze hizo *scholarship* na wanaoweza kuchukua mkopo katika fani hizo basi iwe hivyo kwa sababu naona mzigo utaendelea hivyo kila siku na hatimaye wanafunzi watakosa mikopo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI - (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nikubaliane naye katika swali lake la kwanza la nyongeza, kwamba Serikali hatuna utaratibu wa kuwa na *centre* ambazo kila

mwenye ajira atapeleka ajira zake pale na ajira hizo zitatangazwa na baadaye wanaoajiriwa tutawajua wanakwenda wapi. Kwa maana hiyo kuwafuutilia kwa kweli wanafunzi inakuwa ni tatizo. Sasa ushauri huo ambao aliota Mheshimiwa Rished nataka nikubaliane naye na nidhahiri kwamba itakuwa ni jukumu la Serikali kuweza kuhakikisha kwamba haya yanatekelezwa ili hii mikato ya wanafunzi iweze kupatikana kwa urahisi zaidi badala ya Serikali kupoteza fedha zake au kubeba mzigzo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ni suala la Serikali kutanga *scholarship*, nidhahiri kwamba nataka nikubaliane na Mheshimiwa Rished, katika nchi zetu zilizoko kanda ya Afrika Mashariki hawana utaratibu huu wa mikopo kwa wanafunzi. Utaratibu uliopo ni kwamba Serikali zinakuwa na *scholarship*, idadi ile ya *scholarship* ndiyo ambayo inayotangazwa na ndiyo wanafunzi wana-compete katika zile *scholarship*. Mimi nataka nikubaliane naye kwamba na hili nalo Serikali itabidi tuliangalie ili tuweze kuona kwamba ni kiasi gani tutaweza kuwa na scholarship badala ya kuwa na utaratibu wa mikopo kwa vijana.

Na. 144

### **Mauaji ya Wageni Nchini Afrika Kusini.**

#### **MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni tulishuhudia mauaji ya kikatili na ghasia dhidi ya wageni waishio nchini Afrika Kusini na miongoni mwao walikuwepo Watanzania walioathirika na ghasia hizo:-

- (a) Je, Serikali ya Tanzania imefuatilia kwa kiasi gani suala hilo na ni kitu gani kilisababisha ghasia hizo?
- (b) Je, ni Watanzania wangapi waliathirika kwenye ghasia hizo kwa kuumizwa na ni wangapi walipoteza masiha yao?

#### **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan Mbunge wa Kikwajuni lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa ghasia na vurugu zilizuka nchini Afrika Kusini kuanzia tarehe 11 hadi 23 Mei, 2008. Ghasia na vurugu hizo zilianza katika mji mdogo wa Alexandra uliopo Johannesburg na kusambaa katika miji mingine midogo katika jimbo la Gauteng na baadhi ya maeneo ya miji ya Pretoria, Durban, Cape Town. Ghasia na vurugu hizo zilisababisha vifo na uporaji wa mali za wahanga.

Sababu za vurugu hizo kuzuka zilizotokana na hisia zifuatazo:-

- (i) Hisia kuwa wageni walikuwa wakichukua nafasi za ajira za wenyeji kwa sababu wanakubali kufanya kazi yoyote kwa ujira mdogo.
- (ii) Hisia kuwa wageni walikuwa wakipendeleva kwa kugawia nyumba zilizojenga kwa ajili ya watu maskini kwa kutoa rushwa.
- (iii) Dhana kuwa wageni wanajihuisha na vitendo vya uhalifu na hivyo kuchangia kiwango kikubwa cha uhalifu Afrika Kusini. Aidha ilidaiwa kuwa wahalifu wa kigeni walikuwa hawakamatwi kwa vile wanatoa hongo.

Kutokana na hisia hizo, wenyeji waliamini kuwa wageni ndiyo chanzo cha matatizo yao na hivyo kujichukulia jukumu la kuwaondoa nchini mwao.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Watanzania 256 waliathirika kutokana na vurugu hizo. Serikali kwa kupitia ubalozi wake uliopo Pretoria, ilifuatilia kwa makini hatma ya Watanzania hao. Maofisa wa Ubalozi walivitembelea vituo vya polisi katika miji ya Johannesburg, Cape Town na Durban na vitongoji vyake ili kubaini idadi ya Watanzania walioathirika na ghasi hizo. Maofisa hao waliweza kuwatambua Watanzania 98 katika kituo cha polisi cha Jeppe mjini Johannesburg, 120 katika vituo vya Umbilo *Methodist Church* na *Salvation Army* vya mji wa Durban na 32 katika vituo vitano vya mji wa Cape Town.

Serikali pia ilichukua jukumu la kuwarejesha wahanga wote waliokuwa tayari kurejea nyumbani. Watanzania 164 walirejeshwa tarehe 20 Juni, 2008 kwa kutumia mabasi matatu yaliyokodiwa na Serikali. Waathirika 33 walirejeshwa kwa msaada wa shirika la Kimataifa na Uhamiaji (*International Organization on Migration IOM*). (Makofi)

Aidha, kati ya mwezi Mei, vurugu hizo zilipoanza, hadi mwezi Agosti, 2008, Serikali imepokea taarifa ya vifo vya Watanzania wanne, nchini Afrika Kusini, vilivyotokea mwezi Julai, na Agosti, baada ya vurugu kuwa zimepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa miili ya Watanzania hao yote ilirejesha kwa mazishi kwa ushirikiano baina ya Ubalozi wetu na ndugu wa marehemu.

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba ilikuwa ni dhana, na dhana hizo zina msingi na ubaguzi, kwa hiyo Serikali inachukua hatua gani ili wananchi hao waweze kulipwa fidia.

Kuna wananchi wetu ambao wanafanya kazi na wanaoishi kule Afrika Kusini Serikali yetu inawashauri nini wananchi hao? (Makofi)

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuchukulii yaliyotokea Afrika Kusini kwamba ni ubaguzi

lakini kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba tatizo kubwa ilikuwa hisia ya ajira kwamba wageni walikuwa wanapendelewa kuliko wenyewe. Na haya sio jambo geni hata katika miaka ya 90 zilitokea vurugu kama hizo kwa kudhania kwamba wageni walikuwa wanapendelewa kiajira kuliko wenyeti.

Kwa hiyo Serikali ya Jamhuri ya Tanzania haina nia ya kuieleza Serikali ya Afrika Kusini juu ya suala la kulipa fidia. Kwa sababu kwanza wahanga hao walivyoenda kule wenyewe kwa njia zao wenyewe na kwa sababu zao wenyewe na wengine walikuwemo nchini mle visivyo halali. Kwa hiyo Serikali ya Tanzania haiwezi kuzungumza halina nia ya kuzungumza suala hili na Afrika Kusini juu ya suala la fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili sio tu Watanzania wanaoishi Afrika Kusini hivi sasa lakini Watanzania wote wanaoishi nchi za nje ningependa kutoa wito kwao kwamba zinapotokea vurugu wasijiingize katika vurugu hizi.

Watanzania wote wanaoishi nchi za nje ambao bado hawajajiandikisha katika balozi zetu, wafanye hivyo ili zikitokea vurugu kama hizi waweze kujulikana walipo na kupewa msaada utakaohitajika.

Na. 145

### **Matangazo ya Vivutio vya Utalii Kwenye Kituo cha CNN**

#### **MHE. DK. BINILITH S. MAHENGE aliuliza:-**

Kwa kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na utalii ilianza kutoa matangazo ya vivutio vya Utalii vya Tanzania kwenye kituo cha kimataifa cha *CNN* kilichopo Marekani; na kwa kuwa, matangazo hayo hurushwa kwa lugha ya kiingereza na hivyo kushindwa kuwafikia idadi kubwa ya watu kutoka nchi zilizoongea kiingereza:-

(a)Je, ni nini mkakati wa Serikali wa kurusha matangazo ya vivutio kwenye nchi ambazo hazitumii lugha ya kiingereza kama za Ulaya Magharibi na Mashariki, Japan, China na kadhalika?

(b)Je, ni nini mkakati wa kuitangaza hifadhi ya taifa ya Kitulo ambayo ni hifadhi pekee ya Maua Tanzania kama inavyojulikana *The Serengeti of Flowers* au Bustani ya Mungu?

#### **WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Binilith Satano Mahenge Mbunge wa Makete lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Wizara yangu imeendelea kutangaza utalii wetu katika televisheni ya CNN - Marekani (*Domestic*), na WABC - New York, Zote za

Marekani na kwenye viwanja vitano (5) vya ndege Marekani kwa lengo la kuvutia watalii wengi kutoka nchini humo. Mtangazo yameendelea kutolewa hadi Machi, 2009.

Madhumuni ya kutangaza kwenye televisheni ni kuwawezesha watu wengi kuyaona matangazo hayo kwani vipindi vya televisheni hutazamwa na mamilioni ya watu.

Wizara imeanza na Marekani kwa vile soko hilo kwa sasa ndilo linaloipatia nchi yetu watalii wengi. Kwa mfano kiasi cha watalii 58,279 kati ya watalii 719,031 wa kimataifa walitembelea Tanzania mwaka 2007, wote walitoka Marekani, ambao ni sawa na asilimia 8 ya jumla ya watalii wote wa kimataifa waliokuja nchini.

Wizara ilichagua *CNN (Domestic USA)* na baadae *WABC* - New York zinazotumia lugha ya kiingereza na kutazamwa na mamilioni ya Wamarekani ili kufikisha ujumbe wetu kwa wahusika wanaoangalia televisheni hizo.

Mkakati wa Serikali ni kutangaza kwenye televisheni za huko Ulaya Magharibi na Mashariki, Japani, China na Uarabuni, ambapo matangazo yatatolewa kwa lugha husika.

Aidha, napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa, kwa sasa tovuti ya Bodi ya Utalii ([www.tanzaniatouristboard.com](http://www.tanzaniatouristboard.com)) inasomeka kwa lugha ya kiingereza na pia taarifa hizo zimetafsiriwa na kuwekwa kwenye tovuti ya biashara ya utalii China kwa lugha ya Kichina.

Aidha, Wizraa imechapisha majarida yapatayo 200000 kwa lugha za Kiswahili, Kiingereza, Kijerumani, Kiholanzi, Kitaliano, Kihispaniola, Kiarabu, Kijapani, na Kichina na kuyasambaza kuititia balozi zetu na kuititia maonyesho mbalimbali ya utalii.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Kitulo ni mojawapo kati ya Hifadhi 15 za Taifa zilizoko chini ya usimamizi wa hifadhi za taifa la Tanzania. Hifadhi hii ambayo ilianzishwa Juni, 2005 inasifika kwa kuwa na uwingi na aina za uoto mandhari nzuri na maua kuliko hifadhi nyingine yoyote hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kuititia hifadhi za taifa, imetengeneza filamu za video pamoja na DVD zinazoonyesha hifadhi zote za taifa ikiwemo hifadhi ya Kitulo na kuzitangaza ndani na nje ya nchi, ambapo waandishi wa habari wa *ITV*, *TBC1*, *Channel 10*, *Radio One* na *TBC* Taifa wametembelea Kitulo na kutoa makala maalum kuhusu hifadhi hiyo.

Katika vyombo hivi kila kimoja kimetoa wastani wa programu tano. Mwezi Januari, 2009 waandishi na wapiga picha wa *B BC* waliwasili nchini kwa ajili ya kupiga picha kwa lengo la kutangaza hifadhi ya Kitulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuandaa vitabu, vijarida, vipeperushi na kalenda pia diaries na postars kwa ajili ya kutangaza utalii umuhimu wa kipekee unatolewa kwa hifadhi zile ambazo hazijawa maarufu kwa watalii ambapo hifadhi ya Kitulo ni mojawapo.

Sambamba na utoaji taarifa shirika la TANAPA hutengeneza na kugawa hidaya yaani Souvenirs mfano Kofia, mifuko, fulani, T-shirts, vikapu, covers za Matairi, stickers za Magari, key holders na kalamu zenye nembo na majina ya hifadhi mbalimbali kwa watalii watarajiw.

Wizara itaendelea na mikakati ya kutangaza hifadhi zake na kuweka msukumo zaidi kwa hifadhi zilizoko Kanda ya Kusini Magharibi na Ziwa ambazo bado hazijafahamika vizuri kwa wadau wa utalii.

**MHE. BINILITH S. MAHENGE:** Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimwa Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, kivutio kikubwa cha watalii ili kuweza kuifikia hifadhi yoyote mahali ilipo wanaangalia ubora wa miundombinu na kwa kuwa, pale Kitulo kuna hifadhi ya Kitulo yaani Kitulo National Park lakini vilevile kuna shamba la Ng'ombe uwekezaji ambaao ni mkubwa sana kwa Serikali hii katika kujenga uchumi.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha zile barabara zinazoingia kwenye hifadhi ya Kitulo ili ziweze ksaidia Kitulo National Park na Shamba la Ng'ombe la Kitulo kwa ajili ya kusaidia watalii kufika pale kwa haraka kama ilivyo sasa hivi katika Hifadhi za Manyara, Ngorongoro na mahali pengine?

Swali la pili, wakati Mheshimiwa Rais alipoongea na Wazee na Wabunge hapa Dodoma alieleza dhamira yake ya kupunguza visa kutoka dola 100 hadi 50 ili kuvutia Watalii waweze kuja kwa wingi kutoptana na msukosuko huu wa uchumi duniani. Lakini kupunguza visa bado hazitoshi, je Serikali ina mkakati gani kuona kwamba zile huduma nyingine ambazo zitasaidia visa ikipunguzwa kuja watalii waweze kupata huduma nzuri na kwa bei nafuu kama Mahotelini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mahenge kama ifuatavyo:

Swali la kwanza napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti ya TANAPA zimetengwa fedha za kuboresha na kujenga barabara inayokwenda katika hifadhi ya Kitulo kuanzia kwenye kona inapoingilia mpaka katikati ya hifadhi jumla ya kilomita 15 zitajengwa kwa mwaka huu.

Swali la pili ni kwamba zaidi ya kupunguza bei ya visa pia Wizara yangu imefanya mikakati ambapo tumeshirikiana na wadau wetu wa utalii ambao ni Mashirika yanayohusika na huduma za utalii ikiwemo mahoteli, waongoza utalii hali kadhalika ikiwemo na parks zetu za utalii.

tumekubaliana na sasa hivi tuko katika mazungumzo na wameshaniletea mapendekezo ya jinsi ambavyo tutapunguza bei katika sehemu hizo mbalimbali ikiwemo bei za kwenye mahoteli, bei za kuingilia kwenye hifadhi zetu hali kadhalika na bei za kuwatemebeza watalii katika sehemu mbali mbali.

Kwa hiyo, kuna mapendekezo ambayo bado hatumamaliza maongezi, tutakapokubaliana ndipo ambapo tutazitangaza.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Waheshimiwa Wabunge, kulingana na muda Wizara hiyo bado haijasoma bajeti, tutapata muda wa kuchangia. Tunaendelea sasa na swali linalofuata lakini kabla hatuja endelea naomba tu niwape taarifa kwa ku tulitumia muda kwa ajili ya taarifa ya Mheshimiwa Spika hapa Mezani nitaongeza kama dakika kumi hivi kwa ajili y akumalizia maswali yaliyobakia.

Sasa naomba nimuite Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mbunge wa Kibiti, kwa swali linalofuata.

Na. 146

### **Kufungwa kwa Msitu wa Eneo la Delta ya Mto Rufiji na Vibali kwa Wananchi Kutumia Miti**

**MHE. ABDUL JARIB MAROMBWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, eneo lote la Delta la Mto Rufiji limesheheni miti aina ya Mikoko (*Mangroves*) ambayo hutumika kwa ajili ya ujenzi ndani na nje ya nchi yetu na kwa kuwa Serikali imefunga misitu hiyo kwa zaidi ya miaka mitano sasa;

- (a) Je, ni sababu zipi za msingi zilizosababisha misitu hiyo kufungwa?
- (b) Je, ni lini Serikali itaruhusu na kutoa vibali kwa wananchi ili kuweza kukata miti hiyo kwa mpango endelevu?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa Mbunge wa Kibiti lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilizuia uvunaji wa mbao na magogo katika misitu yote ya asili Tanzania Bara ikiwa ni pamoja na Mikoko. Sababu kubwa ya kuzuia uvunaji huo ilitokana na kuwepo kwa ongezeko la uvunaji haramu wa mazao ya misitu bila kufuata utaratibu hususani mikoko, mbao na magogo katika Mikoa mingi nchini. Kasi ya uvunaji katika Mikoa ya Pwani, Lindi na Mtwara ilitishia kuleta uharibifu mkubwa wa mazingira.

Aidha muingiliano wa kimamlaka kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa katika kusimamia rasilimali za misitu ililazimu kusimamisha shughuli za uvunaji kwa muda, ili kuandaa utaratibu utakaowezesha kuwepo kwa uvunaji endelevu katika misitu yote nchini.

Ili kuondoa tatizo tajwa Wizara imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kufanya tathmini ya kujua malighafi ya misitu iliyopo na mahitaji halisi kwa viwanda na uwezo wa misitu kutoa malighafi hiyo.

Aidha, mwongozo wa uvunaji endelevu na biashara ya mazao ya misitu umeandaliwa. Pamoja na mambo mengine mwongozo wa uvunaji unasisitiza kuwa “Ili uvunaji uwe endelevu kila mahali nchini, sharti kuwe na Mpango wa Usimamizi wa Misitu (*Management Plan*) na mpango wa uvunaji kwa kila Wilaya (*Harvesting Plan*)”.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Serikali imepanga kufanya tathmini ya mikoko kwa kutumika picha za anga kwa uhisani wa Benki ya Dunia na Serikali ya Finland kupitia mradi wa kitaifa wa tathmini ya rasilimali za misitu (*National Forest Assessment – NFA*). Tathmini ya mikoko itafanywa kwa muda wa mwaka mmoja na itaanza rasmi mwezi wa Saba mwaka huu (2009).

Kazi hii inakadiriwa kugharimu dola za Kimarekani kati ya 150,000 – 200,000. Baada ya zoezi hilo kukamailika shughuli za uvunaji endelevu wa kibiashara wa Mikoko utaruhusiwa.

Aidha, Wizara yangu imeweka utaratibu maalumu kupitia Kamati za Mazingira za Vijiji wa kuwezesha wananchi kujipatia mahitaji yao ya msingi yasiyo na kibiashara kama kuni na majengo.

Tunamwomba Mheshimiwa Mbunge, tuendelee kushirikiana katika mchakato wa zoezi linaloendelea pamoja nakuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kuendelea kuitunza mikoko kwa ajili ya kuhifadhi ikolojia ya Pwani.

## **Jengo la Polisi Wilayani Nkasi**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA – kny MHE. PONSIANO D. NYAMI** aliuliza:-

Kwa kuwa, mpango wa kuchimba kisima cha maji katika jengo la Polisi Wilaya ya Nkasi haujakamilika;

Je, ni Serikali itakamilisha kisima hico ili kuondoa usumbufu wa maji kwa Askari na Mahabusu wanaokuwepo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ponsiano Nyami Mbunge wa Nkasi kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji katika Wilaya ya Nkasi ni kubwa na kwa kutambua umuhimu wa upatikanaji wa maji, Jeshi la Polisi liliamua kuchimba kisima kirefu cha maji ili uhakikisha Askari, Mahabusu, familia za Askari na Wananchi waishio jirani na kituo hicho wanapta huduma hiyo muhimu katika maisha ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari zoezi la uchimgaji wa Kisima kirefu cha maji atika Kituo cha Polisi Nkasi umekamilika mwezi Aprili, 2009 na maji yamepatikana. Kinachosubiriwa nsasa ni kupata majibu ya utafiti juu ya usalama wa maji hayo kwa matumizi ya binadamu kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mara baada ya kupata majibu ambayo yataidhinisha maji hayo kutumika, Jeshi la Polisi litaweka matenki ya kuhifadhia maji na kutandaza mabomba ya kusambaza maji hayo kuelekea maeneo husika na kufunga mashine ya kusukuma maji itakayotumia umeme wa sua (*Solar Power*) ili kusukuma maji hayo kutoka katika kisima hicho.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa hii kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba kumekuwa na matatizo ya maji katika Gereza hili, na juhudii ambazo zimefanyika wanaishukuru Wizara. Je, ni lini Wizara hii itahangaikia matatizo mengine pia yanayohusu Magereza pamoja na Polisi kwa kukosa vifaa kama magari, vituo vya mipakani kama Kasesha, Pirando, Kipiri, Matai na sehemu nyingine katika Mkoa wa Rukwa ili kuweza kupunguza matatizo ya Askari wetu ambao wanashindwa kufika kwenye matukio na pia kupata huduma nyingine?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mwananzila kama ifuatavyo:

Kwa hakika Wizara yangu na Serikali kwa ujumla tunathamini sana mchango mkubwa unaofanywa na Askari wetu katika taifa letu katika kulinda amani, usalama wa raia na mali zao. Tatizo la vitendea kazi kama alivyosema mambo ya magari na mambo mengine ya kuweza kuwasaidia Polisi katika kufanya kazi zao ni tatizo ambalo ni kubwa tumelisema mara kwa mara na tutapojaaliwa wakati tutakapokuwa tunaweka bajeti ya mapato na matumizi ya Wizara bado tutazidi kueleza matatizo ambayo yanatukabiali.

Kwa hiyo, ninapenda kumjibu Mheshimiwa Mwananzila kwamba matatizo anayoyasema tunayazingatia na tunajitahidi sana kupata bajeti na ningeomba sana mtusaidie pia kuona kwamba pesa zinapatikana ili Askari wetu ambao wana moyo, uzalendo na wana nia kabisa ya kulinda taifa letu wanaweza kupata vifaa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI – MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na kwa mujibu wa taarifa niliyowapa kwamba nitaongeza dakika chache yaani dakika kumi, nafikiri dakika nilizoongeza zinatosha tumebakiza leo swalii moja la Mheshimiwa Godfrey W. Zambi Mbunge wa Mbozi Mashariki na nitaomba tu Ofisi ya Katibu basi swalii hili lizingatiwe siku ya kesho ili liweze kuulizwa pamoa na Maswali mengine.

Kabla hatujaendelea na agenda inayofuata ninayo matangazo machache, kwanza kabisa naomba nitambue uwepo wa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, kwa takribani siku kadhaa hatukuwa naye hapa Bungeni na mliona Mheshimiwa Khamis akikaimu kiti chake, sasa naona leo imempasa kuondoka katika kile kiti na kumuachia mwenyewe. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge mtambue uwepo sasa wa Kiongozi wa Upinzani Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, Matangazo mengine niliyonayo hapa Mezani kwanza kabisa ninaomba muwatambue wageni wa Mheshimiwa Dr. Shukuru J. Kawambwa Mbunge na Waziri wa Miundombinu kama ifuatavyo;

Wa kwanza ni Mrs Saumu Kawambwa mke wa Mheshimiwa Waziri akiambatana na watoto wake Mariam, Karim na Malik, naomba wasimame. Karibuni sana mmewaona kwenye eneo maalum la Mheshimiwa Spika.

Wa pili ni Viongozi nane wa CCM wa Wilaya ya Bagamoyo na Jumuiya za CCM Wilaya wakiongozwa na Katibu wa CCM Wilaya Ndugu Fikiri Masokola.

Wamo pia Mzee Mohamed Mbagulwa aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM Wilaya Ndugu Margareth Mtalilo Katibu wa Waziri, Ndugu Mohamete Kikwete Mjumbe wa Kamati ya CCM Wilaya na Ndugu Swala Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM Wilaya na Mzee Ally Nassir Muasisi wa CCM Wilaya. Karibuni sana na tumefurahi sana kuwaona.

Wageni wengine wa Dr. Shukuru ni Walimu Wakuu wa shule za msingi 15 wa Wilaya ya Bagamoyo wakiongozwa na Ndugu Joyce Haule Mwalimu Mkoo wa Shule ya Msingi Kizuiani. Karibuni sana. Huyu Joyce Haule anawenza kuwa anatoka Mkoa wa Ruvuma, karibuni sana.

Lakini wengine ni Ndugu Margareth Masenga ambaye ni Katibu wa Mbunge wa Jimbo, Margareth Masenga karibu sana. vilevile yuko Ndugu Mtumwa Kondo Katibu Msaidizi wa Mbunge. Pia yuko Ndugu Francis Bolizozo Katibu wa BFA Wilaya ya Bagamoyo na pia yuko Bwana Patric Mwilongo ambayo ni Mwandishi wa Habari na ni rafiki mkubwa wa Mheshimiwa Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa.

Waheshimiwa Wabunge hao ndiyo wageni wa Mheshimiwa Dr. Kawambwa na tunamshukuru sana Dr. Kawambwa kwa kweli kwa kujali suala la jinsia kwa sababu Katibu wake ni mwanamke na Msaidizi wake pia, basi kwa kweli tunakushukuru sana hiyo ndiyo fifty-fifty.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wanafunzi 36 ambao wanasoma udaktari kutoka Herbert Kariuka Memorial University wako hapa ndani naomba wasimame. Ahasnte sana na karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, nimepatiwa pia mwaliko wa kutembelea maonyesho ya 33 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam yatakayoanza tarehe 28 Juni.

Kwa niaba ya Wizara yangu waandaaji wa maonyesho haya Halmashauri ya Biashara ya Nje *BET* ninayo heshima kukutumia mwaliko kukuomba wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote mje kutembelea maonyesho ya 33 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam yaani Dar es Salaam International Trade Fair hivyo naomba kama utakuwa umeridhia utusaidie kuwaalika kupitia matangazo ya Bunge.

Kwa hiyo, tunalo tangazo hili ambalo linaalika Wabunge wote na nitaomba Mheshimiwa Spika atakapoliridhia basi litalolewa ufanuzi ndani ya ukumbi wa Bunge lakini tumepokea barua hii kutoka Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na nitaliwasilisha Mezani kwa Spika.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo haya naona sina tangazo lingine lolote hapa mezani, kwa hiyo naomba nimuite Katibu atupe Mwongozo wa shughuli inayofuta.

## **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010  
Wizara ya Miundombinu**

**MWENYEKITI – MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Waziri wa Miundombinu Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, tafadhali.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kupidisha Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Miundombinu kwa mwaka wa fedha 2009/10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa uadilifu mkubwa na kudumisha umoja, amani na utulivu tangu amekabidhiwa madaraka ya kuliongoza Taifa letu. Kwa umahiri mkubwa ameendelea kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na kuendelea kutekeleza yale ambayo ameahidi kwa wananchi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amjalie afya njema, hekima na busara ili aendelee kuliongoza Taifa letu kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa nachukua fursa hii kutoa pole kwako binafsi na Bunge lako tukufu kutohana na vifo vya Waheshimiwa Wabunge waliofariki katika kipindi cha mwaka mmoja tangu bunge la Bajeti lililopita. Marehemu hawa ni Mheshimiwa Zakayo Chacha Wangwe, Mheshimiwa Richard Nyaulawa na Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba. Vifo vya Wabunge hawa vimeleta majonzi makubwa kwa Bunge, wananchi wa majimbo ya Tarime, Mbeya Vijijini na Busanda, familia za marehemu na Taifa kwa ujumla. Aidha, natoa pole nydingi kwa familia na wananchi kwa ujumla kwa kifo cha Marehemu Kaimu Sheikh Mkuu wa Tanzania, Sheikh Suleiman Mohamed Gorogosi. Pia natoa pole kwa familia na wanachuo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kifo cha Prof. Haroub Othman, ambaye niliwhi kufanya naye kazi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa miaka kadhaa. Tutawakumbuka marehemu hao kwa michango yao mikubwa katika maendeleo ya nchi yetu. Mungu azilaze roho za marehemu hawa mahali pema peponi, Amin!

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kutoa pole kwako binafsi na Bunge lako tukufu kutohana na vifo vya Waheshimiwa Wabunge wafuatao: Mheshimiwa Zakayo Chacha Wangwe, Mheshimiwa Richard Nyaulawa na Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba. Vifo vya Wabunge hawa vimeleta majonzi makubwa kwa Bunge, wananchi wa majimbo ya Tarime, Mbeya Vijijini na Busanda, familia za marehemu na Taifa kwa ujumla. Tutawakumbuka marehemu Wabunge hawa kwa michango yao mikubwa katika maendeleo ya nchi yetu. Mungu azilaze roho za marehemu Wabunge hawa mahali pema peponi - Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia nafasi hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwapongeza Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale (Mb) kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini kupiditia Chama cha Mapinduzi (CCM), Mheshimiwa Charles Nyanguru Mwera (Mb) kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Tarime kupiditia Chama cha Demokrasia na

Maendeleo (CHADEMA) na Mheshimiwa Lolensia Bukwimba (Mb) kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Busanda kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM). Ushindi walioupara ni ushahidi wa imani waliyo nayo wananchi wa majimbo yao ya uchaguzi. Naamini kwamba kuchaguliwa kwao kwa kura nyingi kutakuwa ni kichocheo cha kutekeleza kwa umakini majukumu yao kama wawakilishi wa wananchi katika Bunge hili tukufu. Aidha, napenda kuwashukuru wananchi wa jimbo la Bagamoyo kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa katika kazi zangu mbalimbali za utumishi wa jimbo. Ushirikiano wao pamoja na wa Watanzania wote kwa ujumla umenisaidia kutekeleza majukumu yangu ya kila siku katika ujenzi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa namna ya pekee kumshukuru Mwenyekiti na wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa kutosha katika kuiongoza Sekta hii. Ushirikiano wao umesaidia sana kuboresha utendaji wa sekta ya Miundombinu. Kamati hii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Alhaj Mohamed Hamisi Missanga (Mb), Mbunge wa Jimbo la Singida Kusini, imechambua na kuijadili kwa kina bajeti ya Wizara. Kamati ilitembelea miradi mbalimbali ili kuelewa maendeleo na changamoto zilizopo katika sekta zetu. Ushauri na maelekezo ya Kamati hii yameiwezesha Wizara kukamilisha bajeti yake katika muda muafaka. Aidha, ushauri, maoni na maelekezo ya Kamati yamechangia katika kuboresha sekta za ujenzi, uchukuzi na hali ya hewa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao, hususan Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), Mbunge wa Jimbo la Mpanda Mashariki na Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo (Mb), Mbunge wa Jimbo la Kilosa kwa hotuba zao ambazo zimetoa mwelekeo wa ujumla katika masuala ya Mipango, Uchumi, Mapato na Matumizi kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010.

Aidha, naomba kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba za Mawaziri waliotangulia. Maoni ya Waheshimiwa Wabunge hao yamesaidia kuboresha mipango ya Serikali katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda sasa kuchukua nafasi hii kufanya mapitio ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, majukumu ya kisera na kiutendaji, ahadi za viongozi, utekelezaji wa mpango wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na makadirio ya bajeti kwa mwaka 2009/10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maelekezo Ya Ilani Ya Uchaguzi Ya Ccm Ya Mwaka 2005 Na Utekelezaji Wake. Katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, sekta ya Miundombinu ilielekezwa kutekeleza yafuatayo Ibara ya 44: Barabara

(a) Kuendelea kuimarisha Mfuko wa Barabara (Tanzania Road Fund)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia Serikali kuidhinisha mapendekezo ya jinsi ya kuongeza mapato ya Mfuko kwa ajili ya matumizi endelevu ya barabara, katika mwaka wa fedha 2008/09, hadi kufikia mwezi Mei 2009, Serikali imekusanya Shilingi bilioni 189.225 ambapo matarajio ni kukusanya Shilingi bilioni 218.474 ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha 2008/2009.

Kabla ya utekelezaji wa mapendekezo ya kuboresha Mfuko wa Barabara, makusanyo yalikuwa shilingi bilioni 73.082 katika mwaka wa fedha 2005/2006.

(b) Kukamilisha ukarabati wa barabara zote ambao unaendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami ambao umekwishaanza katika Barabara Kuu. Barabara hizo ni Dodoma – Manyoni, Manyoni – Singida, Singida – Shelui, Shelui – Igunga, Igunga – Nzega – Ilula; Muhutwe – Kagoma; Nangurukuru – Mbwemkulu – Mingoyo; Mkuranga – Kibiti; Pugu – Kisarawe; Chalinze – Morogoro – Melela; Tunduma – Songwe; Kiabakari – Butiama; Dodoma – Morogoro; Kagoma – Biharamulo – Lusahunga; Tabora – Kaliua – Malagarasi – Uvinza – Kigoma; Usagara – Chato – Biharamulo na Ndundu – Somanga

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya barabara iliyoelekezwa kukamilishwa ambayo utekelezaji wake ulianza toka Serikali ya awamu ya tatu ni 17. Kati ya miradi hiyo, miradi 11 imekamilika kwa kiwango cha lami. Hii ni sawa na asilimia 65 ya miradi iliyopangwa kutekelezwa.

Aidha, miradi 6 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Miradi iliyokamilika ujenzi ni barabara zifuatazo: Singida – Shelui (km 110), Shelui – Igunga (km 32), Igunga – Nzega – Ilula (km 215), Muhutwe – Kagoma (km 24), Nangurukuru – Mbwemkulu – Mingoyo (km 190), Mkuranga – Kibiti (km 79), Pugu – Kisarawe (km 6), Chalinze – Morogoro – Melela (km 130), Tunduma – Songwe (km 104), Kiabakari – Butiama (km 17), Dodoma – Morogoro (km 256), Manyoni – Singida sehemu ya Isuna – Singida (km 63) na Usagara – Chato – Biharamulo sehemu ya Geita – Kyamiorwa (km 220).

Miradi sita (6) ambayo imeanza na inaendelea kujengwa ni: Dodoma – Manyoni (km 127); Manyoni – Singida (sehemu ya Manyoni – Isuna (km 55)); Kagoma – Biharamulo – Lusahunga (km 154); Tabora – Kaliua – Malagarasi – Uvinza – Kigoma (km 246); Usagara – Chato – Biharamulo (sehemu ya Usagara - Geita ( km 92)) na Ndundu – Somanga (km 60).

(c) Kuendelea kuimarisha barabara nchini zitakazouunganisha nchi yetu na nchi jirani kwa barabara za lami; Makao Makuu ya Mikoa yote pia kwa barabara za lami na kuunganisha Makao Makuu ya Wilaya zote kwa barabara zinazopitika wakati wote. (*Makofi*)

(d) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuimarisha barabara zinazouunganisha nchi yetu na nchi jirani. Nchi jirani zilizokwisha unganishwa na nchi yetu kwa barabara za lami ni nchi 7 kati ya 8 ambazo ni: Zambia na DRC Kongo katika

eneo la Tunduma, Malawi eneo la Kasumulo, Uganda eneo la Mutukula, Kenya eneo la Sirari na Namanga, Burundi eneo la Kobero na Rwanda eneo la Rusumo. Ili kuiunganisha nchi yetu na nchi ya Msumbiji, miradi wa ujenzi wa Daraja la Umoja na ujenzi wa barabara ya Masasi – Mangaka – Mtambaswala (km 119) inatekelezwa.

Aidha, sehemu ya Masasi – Mangaka (km 54) inaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami kwa ufadhili wa Serikali ya Japan ambapo kilometra 15 za awamu ya kwanza zimekamilika. Kazi ya usanifu wa mradi wa barabara ya Mangaka – Mtambaswala (km 65) nayo imekamilika. Miradi mingine inayoendelea kutekelezwa ili kuunganisha nchi yetu na nchi jirani kwa barabara za lami ni pamoja na ujenzi wa barabara za Arusha – Namanga (km105), Tanga – Horohoro (km 65) na Mwandiga – Manyovu (km 60).

Makao Makuu ya Mikoa yote nchini yamekwishaunganishwa kwa barabara za lami isipokuwa mikoa minne tu ambayo mipango ya kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa hiyo inaendelea. Mikoa hiyo ni Rukwa, Kigoma, Tabora na Manyara. Ujenzi wa Barabara ya Tunduma – Sumbawanga itakayounganisha Makao Makuu ya mikoa ya Mbeya na Rukwa upo katika hatua ya kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi

Ujenzi wa barabara ya Kigoma - Tabora itakayounganisha makao makuu ya mikoa hiyo upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Daraja la mto Malagarasi na Ujenzi unaoendelea kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kigoma - Kidahwe (km 36); Ujenzi wa barabara ya Tabora - Itigi - Manyoni – Singida itakayounganisha mikoa ya Tabora na Singida ambao upo katika hatua mbali mbali za utekelezaji. Ujenzi wa barabara ya Singida - Babati - Minjingu itakayounganisha mikoa ya Singida, Manyara na Arusha umeanza. Aidha, ujenzi wa barabara ya Dodoma - Babati itakayounganisha mikoa ya Dodoma na Manyara umepangwa kuanza mwaka wa fedha 2009/10. Katika azma ya kuunganisha mikoa ya Rukwa na Kigoma, mikataba miwili ya ujenzi wa barabara ya Sumbawanga –Mpanda – Uvinza – Nyakanazi, sehemu ya Sumbawanga – Chizi – Kibaoni (km 150) imesainiwa na Makandarasi wameanza matayarisho ya kuanza kazi. (*Makofi*)

Kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara zifuatazo; Tunduma – Sumbawanga; Marangu – Tarakea – Rongai; Minjingu – Babati – Singida; Rujewa – Madibira – Mafinga; Mbeya – Chunya – Makongorosi; Msimba – Ikokoto – Mafinga; Arusha – Namanga; Tanga – Horohoro na ukarabati wa Barabara ya Kilwa (Dar es Salaam), Barabara ya Mandela (Dar es Salaam) na Barabara ya Sam Nujoma (Dar es Salaam).

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mipy ya barabara ilioainishwa kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami ni 11. Kati ya miradi hiyo, mradi mmoja umekamilika, ambao ni ujenzi wa Barabara ya Sam Nujoma. Mradi wa ukarabati wa Barabara ya Kilwa (km 10.1) unakaribia kukamilika. Miradi sita ambayo inaendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami ni Marangu – Tarakea – Rongai (sehemu ya Tarakea – Rongai (km 32) imekamilika), Nelson Mandela, Arusha – Namanga, Mbeya – Chunya – Makongolosi, (sehemu ya Mbeya – Lwanjilo), Msimba – Ikokoto – Mafinga (sehemu ya Iyovi - Kitonga na Ikokoto - Iringa) na Minjingu – Babati – Singida. Aidha, Mkataba wa Ujenzi

wa Barabara ya Mbeya – Chunya – Makongolosi, (sehemu ya Lwanjilo – Chunya (km 40)) umeshasainiwa na Mkandarasi anafanya matayarisho ya ujenzi.

Miradi mitatu ambayo ipo katika hatua za awali za utekelezaji ni Tunduma – Sumbawanga (km 231) na Tanga – Horohoro (km 65), ambapo mchakato wa kuwapata Makandarasi watakaojenga barabara hizi unaendelea. Kwa Mradi wa Rujewa – Madibira – Mafinga (km 151), awamu ya kwanza itahusisha ujenzi wa madaraja makubwa ya barabara yote na itanza mwaka wa fedha 2009/10.

Ilani inaelekeza kuzifanyia upembuzi yakinifu na usanifu barabara zifuatazo kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami: Maganzo – Maswa – Bariadi – Mkula – Lamadi; Babati – Dodoma – Iringa; Sumbawanga – Kigoma – Nyakanazi; Musoma – Fort Ikoma; Korogwe – Handeni – Kilosa – Mikumi; Nzega – Tabora – Sikonge – Chunya; Mtwara – Masasi – Songea – Mbamba Bay; Manyoni – Itigi – Tabora; Ipole – Mpanda – Kigoma na Bagamoyo – Saadani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara za Dodoma – Iringa (km 266), Dodoma – Babati (km 261) na Musoma – Fort Ikoma Gate (km 140) umekamilika. Pia barabara iliyokamilika upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ni Maganzo – Maswa – Bariadi – Mkula – Lamadi (km 171). Aidha, ili kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, Serikali imepanga kuanza ujenzi wa madaraja makubwa katika Barabara ya Dodoma – Babati, ujenzi wa Barabara ya Maganzo – Maswa – Bariadi – Lamadi (sehemu ya Lamadi – Bariadi (km 71)) na barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (sehemu ya Tabora - Nyahua (km 80)), kwa kiwango cha lami. Kazi hii inatarajiwa kuanza Mwaka wa Fedha 2009/10, baada ya taratibu za manunuvi ya Makandarasi kukamilika.

Kuhusu Barabara ya Mtwara – Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 820), mazungumzo kati ya Serikali na Benki ya Maendeleo ya Afrika yanaendelea, kwa ajili ya kupata fedha za kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu, usanifu na ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Mangaka – Tunduru (km 146). Sehemu ya Tunduru - Namtumbo usanifu wa kina umekamilika na Serikali inaendelea na mazungumzo na Serikali ya Japan ili kupata fedha za ujenzi. Mapitio ya ripoti ya mazingira na tathmini ya fidia kwa watu watakaoathirika na Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Namtumbo - Songea – Mbinga (km 139) yanaendelea na mchakato wa kumpata Mkandarasi atakayetekeliza Mradi huu unaendelea. Sehemu za barabara zinazoendelea kufanyiwa usanifu wa kina na maandalizi ya nyaraka za zabuni ni Mpanda – Kigoma – Nyakanazi (km 562), Nzega – Tabora – Sikonge – Chunya (km 599), Manyoni – Itigi – Tabora (sehemu ya Tabora - Chaya (km 159)), Mpanda – Ipole – Tabora (km 359) na Bagamoyo – Saadani – Tanga (km 178).

Ilani inaelekeza kuhimiza maandalizi na ujenzi wa Daraja la Kigamboni chini ya Uongozi wa Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) ili kuunganisha Kigamboni na Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF), kwa kushirikiana na Wizara yangu na wadau wengine, linaendelea na maandalizi ya ujenzi wa daraja hilo. Wabia sita wameonesha nia ya kushirikiana na NSSF katika kujenga Daraja la Kigamboni. Mchakato wa kumpata mbia wa kushirikiana na NSSF unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2010. Aidha, ujenzi wa daraja hilo unatarajiwa kuanza katika Mwaka wa Fedha 2010/11.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kivuko kipy Cha Kigongo - Busisi kinachoitwa M.V. Misungwi chenye uwezo wa kubeba tani 250 kimepatikana na kimeshaanza kufanya kazi tangu Mwezi Mei, 2008. Ilani inaelekeza kukamilisha ujenzi wa daraja jipya la Mpiji, ambalo litawezesha njia badala ya Dar es Salaam – Tanga. Ujenzi wa daraja hili umekamilika.

Ilani inaelekeza kufanya upembuzi yakinifu, usanifu na ujenzi wa daraja la Mto Kilombero na kukamilisha ujenzi wa Daraja la Mto Mwatisi katika Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya upembuzi yakinifu wa Daraja la Mto Kilombero imekamilika. Kazi ya usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni za ujenzi wa daraja hilo, inatarajiwa kukamilika katika Mwaka wa Fedha 2009/10. Kuhusu Daraja la Mto Mwatisi, kazi ya usanifu wa kina imekamilika na mchakato wa kumpata Mkandarasi wa ujenzi upo katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Daraja la Mto Ruvu umekamilika mwezi Agosti, 2008 na daraja hili limefunguliwa rasmi na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, tarehe 20 Mei, 2009.

Ilani inaelekeza kuendelea kuandaa mazingira mazuri ya kuishirikisha sekta binafsi katika ujenzi na matengenezo ya barabara kwa kutumia mfumo wa Jenga, Endesha na Kabidhi (BOT).

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasimu ya Sera ya Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi katika ujenzi na matengenezo ya miundombinu kwa kutumia mfumo wa Jenga, Endesha na Kabidhi (BOT) imekamilika. Sera hii itatoa mwongozo wa jinsi ya kuishirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa kuwa Sera hii ni mtambuka, kwa sasa iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kufuatia mapendekezo ya Kamati ya Wataalam katika ngazi ya Makatibu Wakuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za ujenzi wa Daraja la Umoja, kati ya Tanzania na Msumbiji, imekamilika kwa asilimia 85. Ujenzi wa daraja hili, unategemewa kukamilika mwezi Oktoba, 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea kutoa mafunzo ya matumizi ya nguvu kazi katika ujenzi wa barabara za vijijini (Upscaling of Labour Based Technology Programme).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Usafiri na Uchukuzi, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, ilielekeza sekta hii kuchukua hatua zifuatazo:-

Ilani inaelekeza kuendelea kuliimarisha Shirika la Reli Tanzania (TRC), kwa lengo la kulipa uwezo wa kutoa huduma bora kwa bidhaa na abiria wa ndani na wa nchi jirani. Pia, Shirika litaendelezwa kama mhimili wa mpango wa maendeleo wa eneo la Ukanda wa Kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na Kampuni ya RITES ya India, ina mpango wa kuiongezea mtaji Kampuni ya Reli Tanzania (TRL) ili iweze kuiongeza uwezo wa uchukuzi. Aidha, Serikali kupitia Kampuni ya Rasilimali za Reli (RAHCO), inaendelea kusimamia TRL kufanya matengenezo ya njia ya reli kwa lengo la kuiboresha, kukarabati na kununua injini na mabehewa ya treni. Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Nchi Kavu na Majini (SUMATRA), imeendelea kusimamia usalama wa usafiri wa reli.

Ilani inaelekeza kuendelea kuliimarisha Shirika la Reli la Tanzania na Zambia (TAZARA) ili liweze kuhimili kwa uwezo mkubwa zaidi, majukumu ya kuiboresha huduma kwa bidhaa na abiria na kusaidia shughuli za uendelezaji wa mpango wa eneo la Ukanda wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali za Tanzania na Zambia, kwa pamoja zimeandaa mapendekezo ya kuwasilisha kwa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, kuhusu kushirikisha sekta binafsi katika uendeshaji wa shughuli za TAZARA. Aidha, Itifaki ya 14 ya mkopo wa masharti nafuu wa jumla ya Dola za Marekani takriban millioni 39.3 kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, utasainiwa katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2009/2010, kwa ajili ya kuimarisha TAZARA kwa kuiongezea uwezo wa injini, mabehewa, nyenzo mbalimbali za uendeshaji na mafunzo kwa wafanyakazi. Vile vile kutokana na ziara ya Mheshimiwa Hu Jintao, Rais wa Jamhuri ya Watu wa China, nchini mwezi Februari, 2009, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ilikubali kuendelea kusaidia TAZARA kwa kuipa vitendea kazi na wataalam wa kiufundi.

Ilani inaelekeza kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa reli mpya za Arusha – Musoma, Isaka – Kigali na eneo la Ukanda wa Mtwara, ambayo itaunganisha Bandari ya Mtwara, Songea, Mbamba Bay, Mchuchuma na Liganga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya miradi iliyo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ni ujenzi wa Reli ya Arusha – Musoma. Mradi huu umejumuishwa katika Mpango Kamambe wa Reli ya Afrika Mashariki (East African Railway Master Plan). Mpango huo umekamilika na kuidhinishwa na Mawaziri wenye dhamana ya Reli Machi, 2009. Kazi inayoendelea sasa ni nchi wanachama kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa reli hiyo. Kuhusu reli ya Isaka – Kigali, Mawaziri, wenye dhamana ya reli wa nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi, walisaini makubaliano (MoU) ya kujenga reli ya Isaka – Kigali/Keza – Gitega – Musongati nchini Burundi, tarehe 23 Januari, 2009. Aidha, kazi

ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya reli ya Isaka – Kigali/Keza – Musongati ilikamilika Disemba, 2008.

Kazi ya upembuzi yakinifu wa reli kati ya Dar es Salaam – Isaka imeanza Januari, 2009, baada ya Serikali ya Tanzania kupata msaada wa fedha wa Dola za Kimarekani 943,100 kutoka Serikali ya Marekani kuitia Wakala wake wa Maendeleo na Biashara unaoitwa United States Trade and Development Agency (USTDA). Msaada huo ni kwa ajili ya kuboresha reli hiyo kufikia kiwango cha standard gauge kutoka mita moja kwenda mita 1.435. Upembuzi huu unatarajiwaa kukamilika Septemba, 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuziboresha Bandari za Kigoma na Kasanga katika Ziwa Tanganyika ili ziweze kusafirisha abiria na mizigo kwa wingi kutoka ndani na nchi jirani za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Zambia na Burundi. Katika Bandari ya Kigoma, mtambo wa kuondoa mchanga na kuongeza kina cha maji (Dredger), ulinunuliwa mwezi Disemba, 2008 na umeanza kazi ambayo itakamilika Disemba 2009. Ujenzi wa jengo jipya la abiria, utaanza katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2009/10. Mkandarasi wa kujenga Cherezo (docking yard) katika Bandari ya Kigoma, amepatikana na ujenzi utaanza Julai, 2009. Kuhusu Bandari ya Kasanga, kazi ya kukarabati gati imekamilika. Utafiti wa kujenga gati mbili ili kuwezesha meli mbili kutia nanga kwa wakati mmoja umekamilika na ujenzi utaanza Julai, 2009 na kukamilika mwaka 2011. Aidha, ujenzi wa maghala mawili ya kuhifadhi shehena pamoja na barabara ya kuingia ndani ya Bandari ya Kasanga utaanza Julai, 2009.

Ilani inaelekeza kuvutia uwekezaji katika miundombinu ya usafiri na uchukuzi wa reli, barabara, maji na anga katika Kanda za Maendeleo ili kuimarisha biashara kati ya nchi yetu na nchi jirani na kuwafanya wawekezaji kuvutiwa na soko kubwa la bidhaa na huduma zitakazozalishwa. Aidha, uwekezaji katika kanda hizi utaiwezesha Tanzania kutumia nafasi yake ya kijiografia na kuendeleza wajibu wake wa kuzihudumia nchi jirani zisizo na bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatua mojawapo ya kuvutia uwekezaji, Serikali imekamilisha uandaaji wa Rasimu ya Sera ya Ushirikishaji wa Sekta Binafsi na Umma katika uendelezaji wa miundombinu. Wizara yangu kuitia Mamlaka ya Bandari (TPA), imeandaa Mpango Kamambe wa Bandari (Port Master Plan), ambao umebainisha miradi mbalimbali ya uendeshaji na upanuzi wa huduma za bandari. Aidha, Wizara imekamilisha uanzishaji wa Wakala za Uwezeshaji wa Biashara na Uchukuzi katika Ukanda wa Kati (Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency – TTFA) na Ukanda wa TANZAM (Dar es Salaam Corridor), ambazo zitakuwa zikiratibu huduma za usafirishaji ili kuleta ufanisi wa shughuli za kibiashara zinazopitishwa nchini na hivyo kuvutia wafanyabiashara kutumia miundombinu ya uchukuzi na usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua hizo mbalimbali, Wizara yangu imeendelea kutangaza fursa za uwekezaji katika miundombinu nchini kwa kuwa na mazungumzo na Serikali na Wahisani mbalimbali. Mazungumzo hayo yameweza kutoa fursa ya kuboresha miundombinu ya reli, barabara, viwanja vya ndege na bandari.

Ilani inaelekeza kuitengenezea mazingira mazuri ya kibiashara Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Dar es Salaam yatakayoweza kuundeleza kuwa kiungo (hub) cha usafiri wa anga kitaifa, kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya Kwanza ya Mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) imekamilika. Awamu ya Pili ya ukarabati huo wa miundombinu inayohusisha ukarabati na ujenzi wa barabara za viungio na maegesho, kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege, kuweka taa za kuongozea ndege, ukarabati wa maegesho ya ndege ya Terminal I, maegesho ya ndege za mizigo pamoja na masuala yanayohusiana na mazingira inaendelea. Miradi mingine inayoendelea ni upembuzi yakinifu na usanifu wa jengo jipya la abiria Na. III (Terminal III), jengo la mapokezi ya viongozi wakuu na jengo jipya la mapokezi ya ugeni wa kitaifa (State Reception Building).

Ilani inaelekeza kukamilisha ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe na kuimarisha viwanja vya ndege vya Kigoma, Tabora na Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya Kwanza na ya Pili ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe imekamilika. Awamu ya Tatu na ya mwisho ya ujenzi wa Kiwanja hicho inaendelea. Awamu hii, inajumuisha kumalizia ujenzi wa njia ya kuruka na kutua ndege, pamoja na viungio vyake kwa kiwango cha lami, kujenga mfumo wa kuondoa maji ya mvua kiwanjani, ujenzi wa jengo jipya la abiria, ununuzi na ufungaji wa mitambo ya X-ray kwa ajili ya ukaguzi, kununua samani za jengo la abiria, mifumo ya urahisishaji wa utoaji mizigo kwenye ndege, mtambo wa kuzalisha umeme wa dharura, mitambo ya hali ya hewa (Public Address System), pamoja na ujenzi wa miundombinu ya maji safi na maji taka. Kuhusu viwanja vya ndege vya Kigoma, Tabora na Shinyanga, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa viwanja hivyo sasa zimekamilika. Kazi za kuimarisha barabara ya kuruka na kutua ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Kigoma, Tabora na Shinyanga inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa mabasi yaendayo kasi Jijini Dar es Salaam (DART), utatekelezwa katika awamu sita. Awamu ya kwanza ya mradi huo inajumuisha upanuzi wa barabara za Morogoro, Kawawa na Msimbazi; zote kwa pamoja zikiwa na urefu wa kilometra 20.9. Mchakato wa kumpata Mtaalamu Mwelekezi wa kusimamia ujenzi wa miundombinu ya mradi huu, unaendelea. Aidha, ulipaji wa fidia katika Manispaa ya Kinondoni kulingana na tathmini na malipo ya fidia kwa ajili ya Viwanja vya Gerezani umekamilika. Ujenzi wa miundombinu hii unatarajiwa kuanza rasmi katika Mwaka wa Fedha 2009/10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mawasiliano, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, ilielekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-

Kuimarisha uwezo wa utabiri wa hali ya hewa nchini kwa kutumia vyombo vya kisasa. Hivi sasa tuna vituo vya hali ya hewa 27 nchini. Hatua hii inakamilisha mikoa yote nchini kuwa na kituo kikuu kimoja cha uchunguzi wa hali ya hewa. Vituo 360 vya kupima mvua nchini vimefufuliwa na vituo vipyta 197 kuanzishwa. Vifaa mbalimbali

vya hali ya hewa vilinunuliwa na kufungwa. Taratibu za ununuzi wa Radar mpya zinaendelea na Radar hiyo inatarajiwa kupatikana katika mwaka wa fedha 2009/10.

Ilani inaelekeza kulisaidia Shirika la Ndege la Tanzania ili lichukue nafasi yake ipasavyo ya kuwa Shirika la Ndege la Taifa (National Flag Carrier), kwa lengo la kuliwezesha Taifa kufaidika zaidi na mapato yatokanayo na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imechukua hatua za kujitoa kutoka kwenye ubia na Shirika la Ndege la Afrika Kusini (SAA) na kutoa fedha kiasi cha shilingi bilioni 13.0 katika mwaka wa fedha 2006/07 kwa ajili ya kuiwezesha ATCL kurejesha huduma ambazo zilikuwa zinafanywa na SAA. Katika mwaka wa fedha 2007/08, Serikali ilibadili deni la Shilingi bilioni 17.5 ndani ya ATCL kuwa mtaji ili kuimarisha mizania ya Kampuni hiyo. Aidha, hadi mwezi Juni, 2009, Serikali imetua Shilingi bilioni 12.25 katika mwaka wa fedha 2008/09 kwa ajili ya uendeshaji wa Kampuni na kulipia baadhi ya madeni ya ATCL. Serikali pia inaendelea na mazungumzo na mwekezaji kutoka Jamhuri ya Watu wa China ili aweze kununua asilimia 49 ya hisa za Serikali ndani ya ATCL. Madhumuni ya hatua hizi ni kusaidia Kampuni ya Ndege ya Tanzania kuendelea kupeperusha bendera ya Taifa.

Ilani inaelekeza kujenga mwamko wa kuzingatia mahitaji maalum ya watu wenyewe ulemavu, katika ujenzi na utengenezaji wa majengo yanayotumiwa na Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuwapatia haki watu wenyewe ulemavu. Katika kutekeleza hili, Wizara kupitia Wakala wa Majengo Tanzania imeendelea kuhakikisha kuwa majengo yote ya Serikali yanayojengwa sasa yanabuniwa kwa kuzingatia mahitaji maalum ya watu wenyewe ulemavu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), imeendelea kujenga nyumba za kuwauzia watumishi wa umma. Katika mwaka 2008/09, Wizara imejenga nyumba 21 Jijini Dar es Salaam. Aidha, Serikali imefanikiwa kununua viwanja vipatavyo 429 kwa ajili ya kujenga nyumba za kuwauzia watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, hali ya miundombinu ya barabara, reli, vivuko, usafiri wa anga na usafiri majini, imeendelea kuimarika. Kuimarika kwa miundombinu hii kunatokana na Sera nzuri za CCM katika kutekeleza Ilani yake ya Uchaguzi na jitihada za makusudi zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Nne katika kuboresha miundombinu ya uchukuzi. Maeleo ya kina kuhusu hali ya Sekta ya miundombinu yanapatikana katika Kitabu cha Hotuba, aya ya 37 – 43.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ubunifu na utekelezaji wa Sera za Sekta katika kipindi cha mwaka 2008/09, Wizara imeendelea na utekelezaji wa mikakati ya sera za kisekta. Utekelezaji wa mikakati hiyo, umezingatia ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kuendeleza miundombinu ya uchukuzi na kuboresha huduma zitolewazo na sekta binafsi. Aidha, Wizara imeendelea kuandaa Sera za Sekta, ikiwa ni pamoja na Sera ya Taifa ya Huduma za Hali ya Hewa na Sera ya Taifa ya Majengo ya Umma. Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani ipo katika hatua za mwisho za ukamilishwaji na inatarajiwa

kukamilika mwezi huu wa Julai, 2009. Sera hizi zitaoanishwa na Sera ya Uchukuzi na ile ya Ujenzi ili kuondoa mgongano wa kisheria na kiutendaji katika sekta. Maelezo ya kina kuhusu ubunifu na utekelezaji wa Sera za Sekta yanapatikana katika Kitabu cha Hotuba aya ya 45 – 47.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2008/09, Sekta ya Usafiri na Uchukuzi kwa njia ya barabara, imeendelea kuimarika. Kwa kiasi kikubwa, sekta binafsi imeendelea kutoa huduma za usafiri na usafirishaji kwa njia ya barabara. Wizara ya Miundombinu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Wizara nyingine na taasisi mbalimbali, ziliendelea kuimarisha huduma ya usafiri wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajali za barabarani zinaleta athari kubwa za kiuchumi na kijamii katika nchi yetu. Kwa wastani Taifa linapoteza asilimia 3.4 ya pato lake (GDP) kutokana na upotevu wa Raslimali Watu, mali, gharama za mazishi, matibabu na za utawala. Kiasi hiki cha hasara hakijumuishi simanzi na maumivu katika jamii. Aidha, Serikali imeendelea kutekeleza mipango ya kupunguza msongamano wa magari katika miji mikubwa. Mipango hiyo ni pamoja na kupunguza mabasi madogo katikati ya miji, kufanya ukarabati wa barabara na uanzishaji wa barabara mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2008/09, Wizara ilipanga kujenga na kukamilisha barabara zenyeturefu wa kilometra 242.6 kwa kiwango cha lami. Hadi kufikia mwezi Machi, 2009, jumla ya kilometra 94.0 za barabara ziliwuwa zimejengwa kwa kiwango cha lami. Kilomita zilizobaki zinaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara kupitia TANROADS itaendelea kuzifanyia matengenezo Barabara Kuu, Barabara za Mikoa na Madaraja. Lengo ni kuzifanyia matengenezo Barabara Kuu zenyeturefu wa kilometra 9,552.72 na madaraja 1,026 na Barabara za Mikoa zenyeturefu wa kilomita 19,209.96 na madaraja 1,207. Kwa upande wa Barabara Kuu, jumla ya kilomita 111.8 zitafanyiwa ukarabati kwa kiwango cha lami na kilomita 261.3 zitajengwa kwa kiwango cha lami. Utekelezaji wa miradi hii unajumuisha pia barabara zitakazofadhiliwa na washirika mbalimbali wa maendeleo, ikiwa ni pamoja na Mfuko wa Millennium Challenge Corporation (MCC) wa Marekani. Kuhusu Barabara za Mikoa, jumla ya kilomita 1,006 zitafanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe na jumla ya kilomita 60.3 zitajengwa kwa kiwango cha lami. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa Miradi ya Barabara yameoneshwa katika Kitabu cha Hotuba aya ya 70 – 75.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ambazo mikataba ya ujenzi imetiwa saini hivi karibuni na Makandarasi wapo katika matayarisho ya kuanza ujenzi ni Handeni – Korogwe (km 65), Dumila – Rudewa (km.45), Magole – Turiani (km 48.6), Kagoma – Lusahunga (km 154), Lwanjilo – Chunya (km 40), Masasi – Mangaka awamu ya pili (km17.5), na Bagamoyo – Msata (km 64).

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ambayo ipo katika mchakato wa kuwapata Makandarasi ni Sumbawanga – Kasesya/Kasanga Port (km 105), Tanga – Horohoro (km 65), Songea – Namtumbo (km 70), Tunduma – Sumbawanga (km 231), Songea – Mbinga

(km 78), Dodoma – Babati (ujenzi wa madaraja makubwa), Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi (sehemu ya Bariadi – Lamadi (71km), Tabora – Nyahua (km 80), Same –Mkumbara – Korogwe (km 172), Kitumbi – Segera – Tanga (120km), Isaka – Lusahunga (km 245), Sumbawanga – Chizi – Kibaoni (km 150), Daraja la mto Malagarasi pamoja na Approach Roads (km48), Nzega – Tabora (km116) na barabara ya Tabora – Urambo – Kaliua (sehemu ya Tabora – Tumbi (km 15)).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2008/09, vivuko vipyta vya MV Magogoni (Dar es Salaam) na MV Kome II (Mwanza) vilikamilika na kuanza kutumika. Ukarabati wa vivuko vya zamani vya MV Kigamboni (Dar es Salaam) na MV Sengerema (Mwanza) unaendelea na unatarajiwu kukamilika mwezi Oktoba, 2009. Ujenzi wa Kivuko cha Pangani umeanza mwezi Mei, 2009 na utakamilika mwezi Oktoba, 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara ina mpango wa kununua vivuko vipyta vyenye uwezo wa tani 50 kila kimoja katika maeneo ya Msanga Mkuu (Mtwara), Rusumo (Kagera) na Kivuko cha Kilambo (Mtwara), kitakachotoa huduma kati ya Tanzania na Msumbiji. Kazi nyingine ni kuendelea kukamilisha ununuzi wa vivuko vipyta vya Utete (Rufiji), Rugezi - Kisorya (Mwanza) na Musoma - Kinesi (Mara) ambavyo vitakamilika mwezi Oktoba, 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafiri na uchukuzi katika maziwa, katika mwaka wa fedha 2008/09, Wizara kupitia Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL), ikishirikiana na sekta binafsi iliendelea kutoa huduma za uchukuzi na usafiri katika Maziwa ya Viktoria, Tanganyika na Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2008/09, Kampuni ya Meli inayomilikiwa kwa pamoja na Serikali ya Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China (SINOTASHIP), imeendelea kutoa huduma hiyo. Katika mwaka wa fedha 2009/10, SINOTASHIP inatarajia kukamilisha ujenzi wa meli moja kubwa yenye uzito wa tani (DWT) 57,000 na hivyo kuwa na idadi ya meli tatu ifikapo mwishoni mwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Usalama wa Vyombo vya Majini Wizara kupitia SUMATRA imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria Na. 21 ya Usafiri Majini ya Mwaka 2003, kwa kuboresha ulinzi na usalama wa vyombo vya majini. Katika mwaka wa fedha 2008/09, jumla ya vyombo vidogo 302 katika Mwambao wa Bahari ya Hindi na vyombo vya usafiri 17, vyenye uzito wa zaidi ya tani 50 vilikaguliwa ili kubaini ubora wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha usalama wa usafiri majini hususan mawasiliano na vyombo vya usafiri majini, Serikali imefungua Kituo cha Utafutaji na Uokoaji tarehe 25 Machi, 2009, kwa ajili ya kutoa taarifa kwenye Taasisi za uokoaji wakati wa matukio ya majanga kwa vyombo vya majini. Kwa kupitia uratibu wa kituo hiki, jumla ya maisha ya watu 209 kati ya watu 234 yaliokolewa katika matukio sita yaliyotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2008/09, Serikali imeendelea na jitihada za kuongeza uwezo wa bandari zetu ili kuhudumia mizigo zaidi, hususan shehena ya kontena. Aidha, Mpango Kamambe wa Uendelezaji wa Bandari zote nchini ulikamilika mwezi Disemba, 2008. Mpango huu umeainisha mahitaji halisi na mikakati ya utekelezaji kwa bandari zote katika kipindi cha miaka 20 ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha huduma za bandari katika mwaka 2009/10, Wizara kupitia Mamlaka ya Bandari, itajenga jengo la ghorofa kumi kwa ajili ya kuegesha magari. Eneo linalotumika kuweka magari sasa litatumika kuweka kontena. Kazi nyine itakayotekelawa ni ujenzi wa kituo kipywa cha kuhudumia kontena katika gati namba 13 na 14 katika Bandari ya Dar es Salaam, pamoja na ujenzi wa Bandari Kavu huko Kisarawe. Miradi mingine itakayotekelawa ni ujenzi wa kituo cha kuhudumia shehena ya majimaji cha SPM, kuendeleza fukwe na kufanya ujenzi wa gati katika Bandari za Mafia na Kasanga na ujenzi wa jengo la bandari (One Stop Shop).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2008/09, Kampuni ya TRL imeendelea kutoa huduma ya usafiri wa abiria na mizigo. Kampuni hii imekuwa ikitabiliwa na ubovu wa njia na upungufu wa injini na mabehewa. Katika kuongeza uwezo wa uendeshaji, TRL ilikarabati injini kumi, ilifanya matengenezo ya kawaida kwa mabehewa 25 ya mizigo na mabehewa 22 ya abiria, matengenezo makubwa (Overhaul) ya injini 4 (88xx class), kukarabati (rehabilitation) injini mbili za aina ya “88xx class” na kukodisha injini 25 za 73R na mabehewa 23 ya abiria ya daraja la kati. Aidha, mabehewa 15 yalikarabatiwa na radio za mawasiliano ya VHF zilifungwa katika stesheni za reli kati ya Tabora - Kigoma na Tabora - Mwanza. Katika mwaka wa fedha 2009/10, TRL imepanga kufanya ukarabati wa mabehewa 82 ya abiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2008/09, Kampuni ya RAHCO ilikamilisha kazi ya kubadilisha mataruma ya uzito wa ratili 80 kwa yadi ya reli kati ya Malongwe na Itigi (km 47) na upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Reli mpya ya Isaka – Kigali – Musongati kwa kiwango cha Standard Gauge, ni ununuzi wa reli na mataruma kwa ajili ya ukarabati wa kilomita 150 za reli kati ya Dodoma na Tabora. Reli na mataruma haya yanatarajiwa kuwasili nchini mwezi Julai, 2009. Maelezo ya kina kuhusu utendaji wa RAHCO yanapatikana katika aya ya 93 - 94. Aidha, RAHCO imenunua mashine za kupakia na kupakua mizigo Reachstackers tano. Mashine hizo zinatarajiwa kuwasili nchini mwezi Septemba, 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2008/09, TAZARA imeandaa Mpango Biashara (Business Plan) wa miaka mitatu, unaolenga kukwamua utendaji wa mamlaka na kuongeza mapato. Aidha, TAZARA imepokea injini mbili za Sogea na mabehewa 100 ya kusafirishia shehena na mafuta na vifaa mbalimbali vyta kutengeneza njia kuu ya reli kupitia itifaki ya 13 ya ushirikiano wa kiufundi baina ya nchi tatu za China, Tanzania na Zambia. Katika mwaka wa fedha 2009/10, TAZARA ina mpango wa kukarabati vichwa sita, mabehewa ya mizigo 300 na mabehewa ya abiria 72. Mpango mwengine ni kuboresha njia kuu na miundombinu ya mawasiliano ili kuongeza ufanisi na usalama wa treni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA), imeendelea kutoa huduma za uongozaji ndege kwenye anga na viwanja vya JNIA, Arusha, Dodoma, Iringa, Mbeya, Mtwara, Mwanza, Tabora, Kigoma, Pemba, Zanzibar, Tanga na Songea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2008/09, Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga, imekamilisha kanuni za kuanzisha Mfuko wa Mafunzo kwa Marubani na Wahandisi wa Ndege (Aviation Training Fund). Katika mwaka wa fedha 2009/10, Mamlaka ina mpango wa kubadilisha mitambo ya mawasiliano ya ndege kwenye anga ambayo iko katika Mikoa ya Mwanza, Tabora, Ruvuma, Arusha, Mbeya, Morogoro na Mtwara. Mitambo hii mipya itaimarisha mawasiliano kwa ndege zinazopita kwenye anga la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2008/09, Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA), imeendelea kuboresha hali ya viwanja vya ndege nchini. Katika mwaka wa fedha 2009/10, kazi zitakazotekelawa ni pamoja na ujenzi wa uzio wa viwanja vya ndege vya Mafia, Lake Manyara na Arusha; kununua mitambo ya X-ray kwa ajili ya Viwanja vya Tabora, Shinyanga na Musoma; Kununua Walk Through Metal Detectors, kwa viwanja vya Arusha, Mwanza, Shinyanga, Tabora na Musoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Wizara kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), imenunua na kufunga vifaa mbalimbali vya kupimia hali ya hewa pamoja na mtambo wa kuzalisha hewa ya hydrogen na kifaa cha kuhakiki mgandamizo wa hali ya hewa. Mitambo ya kupima hali ya hewa inayojiendesha yenyewe katika vituo vya Mtwara, Babati, Tabora, Kigoma, Kibondo, Tukuyu na Bukoba iliboreshw. Katika mwaka wa fedha 2009/10, Mamlaka itaongeza vituo vya kupima hali ya hewa, kuimarisha vituo vilivyopo kwa kuviongezea vifaa, kuanza kutoa huduma katika kituo cha hali ya hewa cha Mpanda na pia kuanza ujenzi wa kituo cha hali hewa Babati na Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2008/09, Wizara kupitia TBA iliendelea kushauri na kusimamia ujenzi wa nyumba za viongozi na watumishi wa umma, ujenzi na ukarabati wa majengo ya ofisi za serikali, kuweka samani katika nyumba za viongozi. Maelezo ya kina kuhusu utendaji wa TBA kwa mwaka wa fedha 2008/09 na malengo ya mwaka 2009/10 yametolewa katika Kitabu cha Hotuba aya ya 117 – 120.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2008/09, Wizara kupitia TEMESA imeendelea kufanya matengenezo ya magari ya Serikali 4,288 katika karakana zake zilizopo nchi nzima katika Makao Makuu ya kila Mkoo Tanzania Bara, kusimamia usimikaji wa mifumo ya umeme katika majengo ya Serikali, matengenezo ya umeme, mifumo ya elektroniki, Mitambo na Vivuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kusimamia Taasisi mbalimbali zinazohusika na uratibu wa shughuli za kisekta. Taasisi hizo ni pamoja na Baraza la Taifa

la Ujenzi (NCC), Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB), Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB), Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) na Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB). Maelezo ya kina kuhusu utendaji wa Taasisi hizo yanetolewa katika Kitabu cha Hotuba aya ya 123 – 138.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2008/09 Wizara iliendelea kushiriki katika mikutano, semina, kongamano na warsha mbalimbali za kitaifa na kimataifa, zenyelengo la kukuza mashirikiano ili kuendeleza miundombinu na huduma zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2008/09, Wizara imeendelea na jukumu lake la kuwaendeleza na kuwahudumia watumishi wake kijamii na kitaaluma. Katika kipindi hiki, Wizara imeweza kuwapandisha vyeo Watumishi 75 wa kada mbalimbali, kuwathibitisha kazini watumishi 11 na kuwaajiri katika masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni watumishi 46. Katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara itaendelea na utaratibu wa kupima utendaji kazi wa watumishi wake kwa njia ya uwazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2008/09, Wizara imeendelea kupambana na rushwa ikiwa ni pamoja na kuziba mianya ya rushwa. Kwa kutambua athari na matokeo ya rushwa, Wizara imeendelea kufanya kazi zake kwa uwazi na uaminifu. Katika kuimarisha suala hili, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), iliweza kuendesha mafunzo elekezi kwa Wakuu wa Idara na Watendaji Wakuu wa Taasisi ili kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2008/09, jumla ya Wafanyakazi 480 katika makundi tofauti walipata mafunzo ya jinsi ya kujikinga na Ukimwi, matumizi ya dawa za kuongeza kinga mwilini, kuishi kwa matumaini, vifaa vya kinga na kupima kwa hiari. Katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara imepanga kuandaa na kutekeleza mikakati ya ufuatilaji na kutathmini hali ya Ukimwi katika Wizara, kusaidia kugharimia chakula chenye lishe bora kwa waathirika, pamoja na madawa kwa watumishi watakaopima afya zao kwa hiari na kubainika kuwa wameathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inasimamia vyuo vinavyotoa mafunzo yanayohusu sekta. Vyuo hivyo ni pamoja na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam, Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma, Chuo cha Ujenzi Morogoro na Chuo cha Matumizi ya Teknolojia Stahili ya Nguvu Kazi (Appropriate Technology Training Institute – ATT) – Mbeya. Vyuo hivi vimesaidia katika kutoa wataalam wa Sekta za Ujenzi, Uchukuzi na Hali ya Hewa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wizara ya Miundombinu, napenda kuwashukuru kwa dhati, wadau wote wa sekta za ujenzi, uchukuzi na hali ya hewa, kwa ushirikiano wao katika kutimiza malengo yetu. Shukrani zetu pia ziwaendee Washirika wenzetu wa maendeleo katika kutekeleza programu na mipango yetu ya Sekta. Washirika hao ni pamoja na mashirika na taasisi za kimataifa zinazochangia katika kuboresha utoaji huduma na miundombinu ya sekta zetu. Nchi na mashirika hayo ni

pamoja na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini (IMO), Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO), Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (BADEA), Kuwait Fund, Jamhuri ya Korea, OPEC Fund, Umoja wa nchi za Ulaya, Third World Organization for Women in Science (TWOVS), UNESCO, Nchi za Urusi, Jamhuri ya Korea, Afrika Kusini, Uingereza, Marekani, Uhlanzi, Japan, India, China, Denmark, Norway, Ubeligiji, Ujerumani na Washirika wengi wengine ambao sijawataja hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa michango na ushirikiano mlionipa katika kuimarisha huduma zitolewazo na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia Hotuba yangu kwa kuwashukuru viongozi wenzangu katika Wizara, nikianza na Naibu Waziri, Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje (Mb.), Katibu Mkuu Mhandisi Omar Abdallah Chambo, Wakuu wa Idara, Wakuu wa Vitengo, Watendaji Wakuu na Viongozi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, pamoja na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi. Wote kwa pamoja, wamenipa ushirikiano mkubwa ambao umenisaidia kutekeleza majukumu niliyopewa ya kusimamia uendelezaji wa sekta za ujenzi, uchukuzi na hali ya hewa.

Michango yao ya mawazo na utendaji mzuri yameweza kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi na mafanikio ya kutia moyo. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua fursa hii, kutoa shukurani zangu nydingi na za dhati kwa mke wangu na watoto wetu, kwa upendo, kwa kunipa moyo na kwa ushirikiano na kunivumilia pale ninaposhindwa kuwa nao kutokana na majukumu mbalimbali ya kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Wizara ya Miundombinu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ipasavyo, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/10, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 841,298,364,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 270,767,330,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaada, ambapo Shilingi 28,126,496,000 ni mishahara ya watumishi na Shilingi 242,640,834,000 ni fedha za Matumizi Mengineyo (OC). Bajeti ya Miradi ya Maendeleo ni Shilingi 570,531,034,000 ambapo kati ya hizo, Shilingi 340,130,302,000 ni fedha za ndani na Shilingi 230,400,732,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tena nitoe shukurani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya [www.infrastructure.go.tz](http://www.infrastructure.go.tz).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba hii, nimeambatisha majedwali ya miradi yote itakayotekelawa katika mwaka wa fedha 2009/10, pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa kutekeleza miradi hiyo. Naomba viambatanisho hivyo, vichukuliwe kama ni sehemu ya vielelezo vyaya hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Dr. Shukuru Kawambwa, kwa hotuba yako. Waheshimiwa Wabunge, kama Mheshimiwa Waziri alivyotoa maelekezo, viambatanisho vya miradi hiyo yote itakayofanyika katika Wizara hiyo, vinaanza ukurasa wa 118 kwenye kitabu chake mpaka ukurasa wa mwisho. Kwa hiyo, katika kipindi hiki ambacho Waheshimiwa Wabunge mnaendelea kuchangia, anayependa kupata picha halisi ya miradi hiyo ya maendeleo kupitia Wizara ya Miundombinu, anaweza akaona pale mgawanyo wa fedha, maeneo yatakayoshughulikiwa Kitaifa, Kimkoa, kwa hiyo, nilikuwa naomba tu niwape ufanuzi huo.

Baada ya kumsikiliza Mheshimiwa Waziri, akiwasilisha hotuba yake, basi sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati iliyohusika kuchambua bajeti hii, Kamati ya Miundombinu. Mheshimiwa Alhaji Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, karibu sana uweze kutoa maoni ya Kamati.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii, ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu, kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/2009, pamoja na Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Miundombinu, Fungu Namba 98, kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010; pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuwasilisha maoni ya Kamati, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kumpongeza Mheshimiwa Lolesia J. M. Bukwimba (Mb), kwa ushindi mkubwa alioupata katika uchaguzi wa Jimbo la Busanda hivi karibuni. Tunapongeza sana. (Makofi)

Aidha, Kamati yangu inatoa pole na rambirambi zake kwa Mufti Sheikh Mkuu wa BAKWATA, Sheikh Issa bin Simba, kwa msiba mkubwa alioupata kwa kufiwa na msaidizi wake wa karibu, Sheikh Suleiman Gorogosi, ambaye pia alikuwa Kaimu Mufti wa Tanzania. Pia tunatoa pole kwa familia na ndugu wa karibu wa Marehemu Profesa Haroub Othman. aliyefariki tarehe 28 Juni, 2009 huko Zanzibar. Kifo chake kimeacha pengo kubwa kwa Watanzania na Wanazuoni duniani kote, tunawaombea Mwenyezi Mungu, aziweke mahali pema Peponi roho za marehemu wote wawili. (Amin)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati, naipongeza Wizara ya Miundombinu, kwa maandalizi na mawasilisho yaliyofanywa na Wizara hiyo mbele ya Kamati yangu kuhusu Mpango na Makadirio ya Bajeti ya mwaka 2009/2010. Aidha,

Wizara iliwasilisha Taarifa kuhusu utekelezaji wa Mipango ya Mwaka 2008/2009 na kazi zilizopangwa kufanyika katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2009/2010 na maombi ya fedha kwa ajili ya kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii, kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati yangu imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Wizara katika kutekeleza maelekezo yote yaliyotolewa na Kamati kwa mwaka 2008/2009.

Pamoja na kwamba, kuna baadhi ya maeneo ya miradi, ambayo hayakuweza kutekelezwa kutokana na uhaba wa fedha, lakini kwa ujumla, Wizara hii imejitahidi kutekeleza asilimia kubwa ya maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala na pia sehemu kubwa ya ahadi za Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliwasilisha taarifa ya mafanikio na changamoto zilizojitokeza kwa kipindi cha Mwaka 2008/2009 kama ifuatavyo:-

- Kukamilika kwa Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani iliyopitishwa Januari, 2009 pamoja na kutunga Kanuni na Sheria mbalimbali.

- Kuongezeka kwa abiria na idadi ya ndege katika viwanja vyetu kwa asilimia 9.9 kwa mwaka 2008/2009 kulinganisha na asilimia 8.8 kwa mwaka 2007/2008.

- Kukamilika kwa ujenzi wa Kivuko kipycha MV Magogoni chenye uwezo wa kubeba tani 500 sawa na abiria 2,000 na magari madogo 60 kwa wakati mmoja; pamoja na Kivuko cha MV Kome II.

- Kuwaendeleza Watumishi katika mafunzo mbalimbali pamoja na kuwapandisha vyeo waliostahili.

- Kuendelea na ujenzi wa nyumba za Watumishi wa Umma pamoja na majengo mbalimbali ya Ofisi za Serikali, kununua viwanja vya kujenga nyumba na Ofisi za Serikali na kukarabati baadhi ya nyumba za Watumishi.

- Ukosefu wa fedha kulingana na mahitaji halisi ya miradi ya maendeleo.  
- Uwezo mdogo wa Makandarasi kumudu gharama za kazi za barabara na uduni wa vitendea kazi.

- Mrundikano wa madeni ya miradi ya barabara, ambayo iliathiri utekelezaji wa mipango ya maendeleo kwa mwaka 2008/2009.

- Uvamizi katika maeneo ya hifadhi ya barabara.  
- Makandarasi kuchelewa kukamilisha kazi za barabara kwa mujibu wa mikataba iliyowekwa.

- Urasimu kwa baadhi ya Wafadhili/Wahisani katika kutoa fedha kwa mujibu wa ratiba zinazowekwa na hivyo kuchelewesha kuanza kwa miradi hiyo.
- Urasimu katika kutoa zabuni hasa kwa miradi ya Wahisani katika baadhi ya miradi.
- Uwezo mdogo wa Sekta binafsi katika ujenzi na matengenezo ya barabara.
- Hujuma katika njia za reli, ajali na wizi wa nyaya za simu hasa katika njia za reli na kuharibu mfumo wa mawasiliano ya treni.
- Hujuma za wizi na uharibifu wa alama za barabarani unaofanywa na baadhi ya wananchi na kusababisha ajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2008/2009, malengo ya Wizara kwa upande wa mapato yalikuwa shilingi 100,178,000, lakini hadi kufikia mwezi Mei, 2009 jumla ya shilingi 62,959,303 zilikuwa zimekusanya na hivyo kutofikia lengo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009, Wizara ilitengewa kiasi cha shilingi 218,603,264,903 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, lakini hadi kufikia mwezi Mei, 2009 kiasi walichopatiwa ni shilingi 200,562,966,144, sawa na asilimia 91.7 ya Bajeti nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miradi ya maendeleo, kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/2009, Wizara ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 593.177, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 356.150 zilikuwa ni fedha za ndani na shilingi bilioni 237.026 zilikuwa za nje. Hadi Mei, 2009, jumla ya fedha zilizopokelewa ni shilingi bilioni 311.338 ambazo ni sawa na asilimia 52.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii kwa mwaka ujao wa fedha, inakadiriwa kukusanya kiasi cha shilingi 30,503,000 kutoka katika vyanzo vyake vya mapato, ikiwa ni pamoja na idara zinazokusanya maduhuli, utawala, ugavi na huduma, pamoja na sehemu ya ufundi umeme. Makusanyo yamekadiriwa pungufu kutokana na uamuzi wa Serikali wa kudhibiti ununuzi wa magari yake kwa kuwa mapato yatokanayo na usajili na ukaguzi wa magari ya hayo yatapunga sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka ujao wa fedha wa 2009/2010, Wizara hii imetengewa kiasi cha shilingi 9,957,522,100 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, zinazojumuisha mishahara ya watumishi wa Wizara, wakati Taasisi zake zimetengewa kiasi cha shilingi 260,809,807,900 na kwamba, jumla ya matumizi ni shilingi 270,767,330,000. Mfuko wa Barabara unategemewa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 284,100, ambapo Wizara ya Miundombinu itapewa 198.87 kutoka katika mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, kiasi kilichotengwa kwa ajili Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Miundombinu ni

shilingi bilioni 570.531, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 340.13 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 230.4 ni fedha za kigeni.

Jumla ya madeni ya Makandarasi hadi tarehe 30 Juni, 2009 ilikuwa ni shilingi bilioni 86, ambazo hazionekani katika bajeti ya mwaka 2009/2010, jambo ambalo litakuwa na athari kubwa kwani baadhi ya miradi itasimama na kusababisha ucheleweshaji mkubwa wa miradi husika. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kutenga fedha kwa ajili ya madai hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kushauri kuwa, Serikali itekeleze mipango ya kazi zake kwa kuzingatia vipaumbele ili kuepuka kushughulikia miradi mingi kwa wakati mmoja na hatimaye kujikuta baadhi yake haitekelezeki kwa kukosa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati bado inaishauri Serikali kubuni vyanzo vypya vya kuongeza pato na kijiwekea mikakati ya kupata fedha za ndani ili kuziwezesha Wizara zake kutekeleza mipango ya Miradi ya Maendeleo kama ilivyojipangia, kwani uzoefu umedhihirisha kuwa fedha za kutoka nje kwa Wafadhili huchelewa kupatikana kwa muda muafaka au kupatikana kiasi kidigo hivyo kuchelewesha baadhi ya miradi inayokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mikataba mingi ambayo Serikali imekuwa ikiingiwa na Wawekezaji au katika michakato ya ubinafsishaji, imedhihirika kuwa ni mibovu kama vile Mkataba wa TICTS, ATCL/SAA, TRL, IPTL na kadhalika; Kamati inaona kuwa, wakati umefika sasa wa Serikali iwachukulie hatua wale wote wanaoshindwa kuishauri ipasavyo na kuiingiza katika Mikataba mibovu isiyozingatia maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa matatizo ya usafiri wa reli nchini yamekuwa sugu; na kutohana na ukweli kuwa wananchi walio wengi wanategemea usafiri huo, Kamati inaishauri Serikali kutafuta fedha za kuimarisha Reli ya Kati na kufufua usafiri wa reli ya Dar es salaam – Tanga – Arusha na kuimarisha ile ya Tabora – Mpanda na Manyoni – Singida. Aidha, Serikali itoe kipaumbele hasa kwa reli ya Tabora – Mpanda, kwani wananchi wa eneo hilo hawana usafiri wa kuaminika unaoweza kuitika mwaka mzima, kwani barabara zao ni mbovu na wanaathirika kiuchumi kwa kukosa miundombinu ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Shirika la Reli Tanzania (TRL), limeshindwa kutoa huduma kwa ufanisi kama yalivyokuwa makubaliano ya Mkataba kati ya Serikali na Wabia hao; na kwa kuwa Serikali katika Bajeti yake hii ya mwaka 2009/2010 imetenga shilingi bilioni moja badala ya shilingi bilioni 91.4 zilizoombwba na RAHCO; ni dhahiri kuwa mipango na malengo ya kuwaondolea wananchi kero za usafiri wa reli nchini hazitafanikiwa.

Aidha, kwa kutokutengewa fedha za kutosha, miundombinu ya reli itazidi kuharibika kwani haitaboreshwaa na kufanyiwa ukarabati wa mara kwa mara. Kwa hali

hiyo tutashindwa kufaidika na fursa ya kijiografia tuliyonayo ya kuhudumia nchi jirani (land locked countries) na hivyo kujikosesa mapato ambayo tunastahili kuyapata. Aidha, hali mbaya ya Reli ambayo inachangiwa kwa kiasi kikubwa na utendaji mbovu wa Kampuni ya TRL utaendelea kusababisha msongamamo wa Makontena katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeelezwa hatua zinazochukuliwa na Serikali za kutafuta fedha kutoka IFC na Benki ya Dunia, kwa ajili ya Ujenzi na kuimarisha Reli, pamoja na shughuli za uendeshaji wa Kampuni ya TRL. Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada hizo, lakini inashauri kuwa fedha zitakazopatikana kamwe zisikabidhiwe kwa Menejimenti ya sasa ya TRL mpaka marekebisho ya uongozi wa juu yatakapofanyika kwa kuhusisha Watanzania katika safu ya uongozi wa juu, kwani Menejimenti iliyopo sasa ya TRL inafanya matumizi makubwa bila ya kushirikisha Serikali ya Tanzania, ambayo ina hisa asilimia 49 na kwamba, manunuzi mengi yanafanyika India bila ya sababu za msingi na bila kufuata taratibu za zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano wa Bunge uliopita, Kamati ilishauri Serikali kukamilisha majadiliano kati yake na TRL katika kipindi kisichozidi miezi mitatu na muda huo umeisha. Bado ufumbuzi wa hatma ya TRL haujapatikana licha ya kwamba, huduma za TRL zinaendelea kulalamikiwa na wananchi hasa wale wanaotumia reli ya Kati kutoka na kwenda Tabora, Mwanza na Kigoma. Tunasisitiza ushauri wa Kamati tulioutoa hapo awali kuwa kama TRL hawako tayari kutoa ushirikiano kwa Serikali juu ya Marekebisho ya Mkataba mbovu uliopo sasa, basi Serikali ichukue hatua ya kuvunja Mkataba wa Ukodishaji wa TRL na kuanza mkakati mpya wa kumtafuta Mwekezaji mwengine. Wakati Mwekezaji mpya anatafutwa, uendeshaji wa Huduma za Usafiri wa Reli ukabidhiwe Kampuni ya Serikali RAHCO na kwamba, iwezeshwe kwa mtaji wa Kutosha badala ya kuendelea kuipa fedha Kampuni ya TRL. Aidha, kuna haja kubwa kwa Serikali kuiwezesha RAHCO kutekeleza majukumu yake kikamilifu, kwani kwa hali ilivyo sasa haiwezi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa sababu ya kutolipwa concession fees kutoka TRL kulingana na Sheria ya RAHCO na Mkataba baina ya Serikali na TRL.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudini zinazofanywa na Serikali katika kulinusuru Shirika la Reli la Tanzania na Zambia (TAZARA), bado kuna matatizo lukuki, ambayo yanahitaji Serikali zetu hizi mbili zikae chini na kubuni mikakati endelevu ya kuiimarisha reli hii ya kihistoria ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi na faida ya nchi hizi mbili. Kamati inaishauri Serikali ione uwezekano wa kuunganisha reli kutoka Tunduma hadi Bandari ya Kasanga ili kuboresha matumizi ya reli hii na kufungua milango ya biashara na nchi jirani ya DRC na hivyo kuweza kuitumia vizuri fursa ya uchumi wa kijiografia kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Sambamba na hilo, kupanua Bandari ya Kasanga kwa kiwango cha kubeba mizigo mikubwa kutoka Kongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu, Kamati ya Miundombinu imekuwa ikisikiliza kilio cha Wafanyakazi wa TAZARA kuhusu maslahi yao duni hasa Wafanyakazi wa TAZARA upande wa Tanzania, mbali na kufanya kazi katika mazingira magumu, lakini mishahara yao ni midogo mno ikilinganishwa na wenzao wa upande wa

pili. Serikali iangalie upya mishahara ya Wafanyakazi wa TAZARA, hasa upande wa Tanzania na kuiboresha. Aidha, kwa wanaodai malimbikizo ya Pensheni baada ya kupunguzwa au kustaaful, nao walipwe mafao yao kwa wakati. Imekuwa ni adha kubwa kwa Wastaafu na wanaofuutilia mirathi za jamaa zao waliokuwa TAZARA, kuzungushwa bila kupata ufumbuzi. Kamati inaishauri Serikali itafute njia ya kuhakikisha kuwa, Watanzania hao wanalipwa pensheni na mirathi yao, kwani wanapata mateso wao pamoja na familia zao kwa miaka mingi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa Serikali imerudisha umiliki wa ATCL kwa Serikali ya Tanzania, hali ya kifedha katika Shirika hilo sio nzuri. Katika Bajeti hii ya Mwaka 2009/2010, Serikali imetenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuboresha huduma za Usafiri wa Anga badala ya fedha zilizoombwa shilingi bilioni 20. Kamati ya Miundombinu ina wasiiasi na namna Serikali inavyoliendesha Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL), kwani liko katika hali tete kwa kukosa fedha za kuendeshea huduma ya usafiri wa anga nchini. Ili kuiwezesha ATCL kujiendesha na kuingia katika soko la ushindani, Kamati inaishauri Serikali, iiongezee ATCL fedha za kutosha kama zilivyoombwa kulingana na mahitaji yao halisi kama ilivyooneshwa katika Mpango Mkakati wa Biashara (Business Plan) ya Shirika na kwamba, matumizi ya fedha hizo yadhibitiwe na CAG.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua kuwa, Serikali inafanya majadiliano na muwekezaji wa Kichina – China SONANGAL, kwa minajili ya kuifufua na Kuiimarisha ATCL ambayo ipo katika hali mbaya kifedha na kiuendeshaji. Kamati inaitaka Serikali kuharakisha majadiliano hayo, kwani yamechukua muda mrefu na hali ya ATCL inazidi kuwa mbaya, vinginevyo Serikali ichukue hatua ya kukaribisha wawekezaji wengine badala ya kumng'ang'ania Mwekezaji mmoja.

Kamati inasisitiza ushauri wake wa awali kuwa idadi ya Wafanyakazi hailingani na Ndege za ATCL inazomiliki hivi sasa, kwa maana ya kwamba ni wengi mno, jambo ambalo linachangia ATCL kuwa na hali mbaya ya kifedha. Kwa hiyo, tunashauri Wafanyakazi wa ziada wanaokadirwa kuwa 364 hawana budi kupunguzwa kwa shabaha ya kuiokoa ATCL na kuharakisha kuwa, wanalipwa maslahi au stahili zao zinazotokana na kuachishwa kazi kwao. Aidha, tunasisitiza kuwa makubaliano yakifikiwa kati ya Serikali na Mwekezaji, Serikali ihakikishe kuwa na umakini mkubwa ili Mkataba utakaofungwa, uweke mbele maslahi ya nchi na kuepukana kabisa na mikataba mibovu, isiyozingatia maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati vile vile inatoa angalizo na kusisitiza kuwa tatizo la kunyanganywa Cheti cha Kuruka na uendeshaji kwa Ndege za ATCL lisirudiwe tena kwani ni aibu na fedheha kubwa kwa nchi. Aidha, Mamlaka ya Udhibiti na Usalama wa Anga Tanzania (TCAA), ihakikishe kuwa kunakuwepo programu za ukaguzi wa mara kwa mara wa shughuli za Shirika. Serikali pia ifanye uchambuzi na uchunguzi wa kina, kisha ichukue hatua kali kwa wazembe waliolifikisha Shirika katika hali iliyokuwa imejitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA), wamekuwa wakiomba Watumishi hasa Marubani na Wahandisi waboreshewe maslahi yao, pamoja na fedha kwa ajili ya uendeshaji na matengenezo kwa ndege walizo nazo. Kamati inashauri Serikali isikie kilio hicho ili kulinda usalama wa viongozi wetu. Aidha, Serikali ilipe madeni inayodaiwa na TGFA, ambayo hadi sasa yamefikia kiasi cha shilingi bilioni 3.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usalama wa anga, Kamati inaitaka Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), kuhakikisha kuwa, Wataalamu wake wanachukua hatua za makusudi za kuhakikisha ndege zinazonunuliwa na Mashirika ya Serikali na yale ya binafsi kuwa ni za usalama. Aidha, TCAA wafanye ukaguzi wa mara kwa mara na kutoa taarifa yake kwa umma ili kuwaondolea mashaka watumiaji wa usafiri wa anga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa, Serikali itengete fedha za kutosha kwa ajili ya kazi za ukarabati wa viwanja vyta ndege na nyingine kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vipyta kama ambavyo ilisisitizwa wakati wa kuwasilishwa kwa Bajeti ya Wizara ya Miundombinu kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Kwa miradi ya viwanja ambavyo Benki ya Dunia imekwishatoa fedha kwa ajili ya usanifu na upembuzi yakinifu kama Kigoma, Tabora, Sumbawanga, Mafia, Arusha, Shinyanga na Bukoba, Serikali ihakikishe kuwa inakamilika. Aidha, ujenzi wa viwanja vipyta vyta Msalato, Dodoma na uboreshaji wa kile cha Mwanza ambavyo vinafadhiliwa na BADEA na OPEC, Kamati ingependa kuona sasa kazi inafanyika pamoja na kukamilishwa kwa Uwanja wa Ndege wa Songwe, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa, fedha za ndani zinatolewa ili kuwezesha Wafadhili nao watoe zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kuwa, juhudini zinazofanywa katika kuendeleza miundombinu hasa ya barabara ni vyema mkazo huo huo ukawekwa kwenye miundombinu mingine ya reli na viwanja vyta ndege ili kukuza uchumi wa nchi kwani miundombinu ya barabara, reli, bandari na viwanja vyta ndege, inatumika kwa kutegemeana. Suala la ujenzi wa Kiwanja kipyta cha Kimataifa ama Bagamoyo au Mkuranga, nalo lifanyiwe maamuzi mapema iwezekanavyo na kwamba, Uwanja wa Mwalimu Julius Nyerere ubaki kutumika kwa safari za ndani (domestic flights).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati kwa mara nyingine tena, inaisisitizia Serikali kutafuta fedha na kukamilisha zoezi la ulipaji wa fidia kwa wakazi wa maeneo yanayozunguka Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere, kama vile Kipawa, Kipunguni na Kigilagila na kuondokana na kero hii, ambayo sasa imechukua muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasikitishwa sana na ongezeko la ajali za majini na nchi kavu, zinazopoteza mali na maisha ya watu, ambao ni nguvu kazi ya Taifa hili. Kamati inaitaka SUMATRA, kwa kushirikiana na mamlaka nyinginezo, kutafuta namna ya kupunguza ajali hizo, ambazo kwa takwimu zilizopo, nyingi huchangiwa na uzembe wa wamiliki wa vyombo vyta usafiri pamoja na madereva. Changamoto iliyopo ni kuvifanyia ukaguzi wa mara kwa mara vyombo hivyo vyta usafiri na kudhibiti ujazo wa

abiria na mizigo. Aidha, kwa vile vyombo vitakavyobainika kusababisha ajali kwa uzembe, adhabu kali zitolewe kwa wahusika ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ya Miundombinu, ilifanya ziara Mkoani Kigoma mwezi Mei, 2009, ambapo pamoja na shughuli nyinginezo, Kamati ilipata fursa pia ya kutembelea Bandari ya Kigoma. Wananchi wa Kigoma wanategemea zaidi usafiri wa reli na wa majini. Kamati haikuridhishwa na miundombinu ya Bandari ya Kigoma, kwani haiendelezwi na hakuna mipaka ya kuonesha eneo la bandari. Kukosekana kwa mipaka hiyo, kumesababisha watu binafsi kuvamia na kijichukulia maeneo yaliyo karibu na bandari, ambayo yangeweza kutumika katika upanuzi na kuendeleza bandari. Kamati inaishauri Serikali kuiboresha Bandari ya Kigoma, kwani ikiboreshwaa na kutumiwa vizuri itakuwa chanzo kingine cha mapato ya nchi yetu. Vile vile Serikali inashauriwa kuhakikisha kuwa, eneo la Bandari lililochukuliwa na watu binafsi linarejeshwa mapema iwezekanavyo,

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilisikitishwa na hali ya Gati la Mafuta katika Bandari ya Kigoma, ambalo halitumiki na hata limefikia hatua ya kufungwa. Kamati inaishauri Wizara ya Miundombinu, kuangalia uwezekano wa kulitumia Gati hilo kwani miundombinu yake bado ipo katika hali nzuri. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania, kukamilisha mchakato wa ujenzi wa Dry Ports katika eneo la Katosho na kujengea mitambo ya kisasa. Hii itasaidia katika kukuza biashara kati ya Tanzania na nchi jirani za Burundi, Congo DRC na kwingineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tatizo la msongamano wa makontena katika Bandari ya Dar es Salaam, Kamati inaishauri Serikali kufanya maamuzi na kutekeleza Maazimio ya Bunge yaliyotolewa katika Mkutano wa Bunge wa Kumi na Moja kuhusu marekebisho ya baadhi ya vipengele vya Mikataba wa TICTS vyenye upungufu, ikiwa ni kusitisha nyongeza ya miaka 15 iliyoongezwa bila kufuata Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2004; kuondoa ukiritimba wa TICTS na kufungua wigo wa huduma hiyo bandarini na kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria, wote walioiingiza Serikali katika kusaini Mikataba yenyе upungufu kama huu wa TICTS.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tatizo la msongamano wa makontena na mizigo bandarini mbali na TICTS kuna mamlaka nyinginezo zinazochangia ucheleweshaji wa mizigo bandarini kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), T-Scan, Mawakala wa kutoa mizigo, pamoja na wenyе mizigo, Kamati inaishauri Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania, kuweka mikakati ya makusudi ikiwa ni pamoja na kuwakutanisha wadau wote na kuelimishana namna ya kupunguza urasimu usio wa lazima bandarini na kuleta ufanisi katika bandari hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza msongamano bandarini, Kamati imekuwa ikisisitiza umuhimu wa kutumia Bandari za Mtwara na Tanga, badala ya kung'ang'anía Bandari ya Dar es salaam tu, lakini Kamati iliwahi kuelezwa kuwa, hilo haliwezekani kwa kuwa TRA wanahofia kupoteza mapato. Kwa kuwa sasa Serikali imefanya uamuzi wake kuondoa VAT kwa ajili ya upakiaji na upakuaji katika Bandari ya Tanga na Mtwara, Kamati inaishauri Serikali (TPA na TRA), kuweka utaratibu mzuri

utakaowezesha meli za mizigo kushushia makasha katika bandari hizo na hivyo kuzitumia bandari hizo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inarudia kusisitiza kuwa, suala la kutoza VAT kwa wenge meli kwa kazi za kupakia na kupakua mizigo, linahitaji kutazamwa kwa uangalifu kwani litafanya Bandari za Tanzania kuwa ghali mno, ukilinganisha na Bandari za nchi jirani na hivyo kukimbiwa na wenge meli. Ni vyema kuzingatia kuwa, Bandari za wenzetu kama vile Mombasa, Beira na kadhalika, hazitozi kodi ya VAT kwa wenge meli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati vile vile inashauri kuwa ni vyema Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kutafuta eneo lao nje ya bandari, ambalo litatumika kuhifadhi mizigo/bidhaa ambazo zimekaa muda mrefu bandarini hasa magari, zinazotakiwa kupigwa mnada baada ya wenge mali kushindwa kuzikomboa au kujitokeza. Hii itapunguza msongamano wa mizigo bandarini, badala ya TRA kutumia eneo la bandari kama ghalo yao ya kuhifadhia bidhaa hizo. Aidha, TRA wawe makini katika kufanya tathmini ya viwango vya kodi kulingana na bidhaa husika na si kubambikiza kodi za ziada, zinazosababisha malalamiko na usumbufu kwa wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Mamlaka ya Bandari kwa kushirikiana na Serikali na Wadau/Wawekezaji wengine, kuangalia uanzishaji wa mradi wa Multistorage Car Park katika maeneo mengine nje ya eneo la Bandari katika Jiji la Dar es Salaam ili kupunguza msongamano bandarini. Aidha, agizo la Rais, Mheshimiwa Jakaya Kikwete la kuwapa TPA eneo la NASACO, litekelezwe kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri TRA/TPA kuhakikisha kuwa, T/SCAN wanaongeza vifaa na magari yanayotumika kufanya ukaguzi na upekuzi wa mizigo inayopitia bandarini ili kupunguza ucheleweshaji na msongamano wa mizigo bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu za Tanzania Trucks Owners' Association (TATOA), kusafirisha mizigo kutoka Dar es Salaam kwenda Tunduma, Kigali na Bujumbura, huchukua wastani wa siku 15 - 20. Hii ni kutohana na vizuizi mbalimbali vilivyoko barabarani, jambo ambalo linapunguza kasi ya uondoaji wa mizigo bandarini. Hivyo, Kamati inashauri kuwa ili kuharakisha usafirishaji wa makasha, uangaliwe uwezekano wa kupunguza vizuizi barabani na kuanzisha eneo moja (One Stop Centre), litakalosimamiwa kwa pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wizara na Idara ya Usalama Barabarani nje ya Mji wa Dar es Salaam kama vile Ruvu, Mikese, Morogoro, Mikumi, Makambaku na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inampongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa jitihada anazofanya za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Barabara mbalimbali. Barabara hizo ni pamoja na Manyoni – Itigi – Tabora, ambayo katika Bajeti ya Mwaka ujao, imetengewa kiasi cha shilingi bilioni 6.7.

Barabara nyingine ni Dodoma – Iringa pamoja na Dodoma – Babati, ambazo Benki ya ADB imeonesha nia ya kusaidia. Aidha, Kamati imeridhika na maelezo ya Serikali kwamba, ujenzi wa Barabara ya Bagamoyo hadi Msata, utasaidia sana kuondoa msongamano katika Barabara Kuu ya Morogoro hasa kutoka Chalinze hadi Dar es Salaam. Huu pia ni mkakati wa kiusalama, kwani kwa sasa tatizo kubwa likitokea katika Daraja la Ruvu (jambo ambalo hatuliombei), litasababisha mawasiliano kukatika baina ya Dar es Salaam na Mikoa ya Ziwa, Kati na Kaskazini, pamoja na nchi jirani na hivyo kuathirika kiuchumi.

Kamati vile vile imeridhishwa na uamuvi wa Serikali wa kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami, barabara ya kutoka Tabora hadi Urambo. Kamati pia inaipongeza Serikali kwa kutiliana saini mikataba na wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa barabara kumi muhimu katika Mikoa ya Rukwa, Tanga, Dar es Salaam na Kagera tarehe 29 Juni, 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa barabara zinazohitajika kujengwa ni nyingi; na kwa kuwa Serikali haina fedha za kutosha; Kamati inaendelea kuishauri Serikali kukamilisha mapema Sera na Mpango wa Build - Operate and Transfer (BOT), Build – Own - Operate and Transfer (BOOT) na ule wa Public Private Partnership (PPP). Hii itahamasisha Wawekezaji kujitokeza kushiriki katika ujenzi wa miundombinu. Vile vile tunasisitiza ushauri wetu wa awali kwamba, kwa kuwa sasa Serikali ya Awamu ya Nne imefanya kazi nzuri, kiasi kwamba nchi sasa inakopesheka, Serikali isiogope kukopa kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa barabara, kwani baadhi ya madeni tunayolipa sasa ni ya miaka 1960 iliyokopwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za Serikali za kuongeza Mfuko wa Barabara, bado ujenzi wa barabara zilizopo chini ya Halmashauri zetu, hauridhishi na kukosekana kwa thamani ya kazi (value for money). Kamati inashauri liwepo fungu maalum kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ili kusaidia ujenzi wa barabara hizo pale wanapoombwa na Halmashauri za Wilaya zenye matatizo, kwani barabara nyingine ni ndefu na mbovu sana wakati uwezo wa Halmashauri ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati bado inaendelea kuishauri Serikali kuangalia upya Sera ya Ujenzi wa Barabara ili kuiwezesha TANROADS kushughulikia Miradi ya Ujenzi na ukarabati wa barabara zote nchini (za Kitaifa, Mikoa na Wilayani), kwa kuwa uwezo wanao na wataalam wa kutosha wapo. Hii itaokoa fedha nyingi, ambazo hupelekwa katika Halmashauri, ambako hakuna ufanisi kutokana na kutokuwa na wataalam wenye sifa na viwango stahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na marekebisho ya sheria hii, ambayo inatoa fursa kwa Makandarasi wa kigeni kusajiliwa na Bodi ya Makandarasi; Kamati inashauri na kusisitiza kuwa, kila kazi itakayotolewa kwa Makandarasi wa kigeni, Makandarasi wazalendo washirikishwe katika kazi hizo na watumike sambamba na Wataalam hao wa kigeni ili wapate usoefu zaidi na kunufaika kimapato. Aidha, kabla ya Wageni hao kupata usajili, uwepo utaratibu wa kubaini uwezo wao wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwepo na sheria rasmi ya majenzi kunachangia kuwepo kwa matukio ya ujenzi usiokuwa na viwango. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuharakisha kutunga sheria hiyo. Aidha, Kamati inaishauri serikali kuwawezesha Wahandisi Wazalendo kupewa kazi kwa upendeleo maalum, hasa kwa miradi inayogharimiwa na Serikali ili waweze kupata vifaa, mtaji na ushindani wa kibashara katika sekta ya uhandisi na ujenzi. Hili likifanyika litawahamasisha Wataalam wetu katika kujijengea uwezo na kuleta ushindani, ambao kwa hivi sasa haupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa Kivuko kipycha M. V. Magogoni, kilichozinduliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Kivuko hicho cha kisasa kitasaidia kutatua kero za Wananchi na kurahisisha shughuli zao za kila siku. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuisisitizia Serikali kukamilisha mchakato wa ujenzi wa Daraja la Kigamboni na kutoa kipaumbele kama ilivyoahidiwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu kumekuwa na utaratibu wa Serikali kupeleka magari kwenye makampuni binafsi kwa ajili ya matengenezo. Kamati inaishauri kuwa, Serikali iwezeshe Wakala wa Ufundu na Umeme (TEMESA) ili ijijengee uwezo na kutumika kama kituo cha matengenezo ya magari yote ya Serikali. Kamati haioni mantiki yoyote ya Serikali kutenga fedha lukuki kwa ajili ya matengenezo ya magari kwenye Kampuni binafsi na kuinyima fedha TEMESA, ambayo ni karakana ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa Chuo cha Usafirishaji (NIT) kimekuwa hakipewi kipaumbele cha kutosha na Serikali. Katika Bajeti ya mwaka huu wa 2009/10, NIT iliomba shilingi 3,093,316,000 kwa ajili ya uendeshaji wa Chuo, lakini kimetengewa shilingi 1,480,946,000. Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha ili mipango ya NIT isikwame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipotembelea Chuo cha Hali ya Hewa kilichopo Kigoma, ilisikitishwa sana na matatizo lukuki yanayokikabili Chuo hicho. Wanafunzi ni wachache sana, kwani wengi wanakikimbia kutohana na mazingira mabaya ya Chuo hicho. Hakuna umeme wa uhakika na jenereta iliyopo haiwashwi kwa muda mrefu. Kamati inaishauri Serikali kukiimarisha Chuo hicho ili wanafunzi wengi wavutike na kufaidika na elimu inayotolewa Chuoni hapo. Aidha, ujenzi uliokwama wa Hosteli ya Chuo upatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Mabaharia (DMI), kinahitaji fedha zaidi kwani kipo katika mchakato wa kuanzisha programu ya masomo ya Shahada ya kwanza, pamoja na kukarabati majengo yao ya chuo. Kamati inaishauri Serikali kuipatia DMI fedha kama zilizoombwa katika bajeti hii ya 2009/2010 ya shilingi 1,562,369,280, badala ya shilingi 811,809,400 zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipitia na kujadili kwa kina mawasilisho ya Wizara ya Miundombinu na hatimaye kupitia Makadirio ya Bajeti hiyo kifungu kwa kifungu. Kamati yangu imeridhika na Malengo, Mipango na Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2009/2010 na sasa Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu, kujadili na kukubali

kupitisha kiasi kilichoombwa cha Shilingi 570,531,030,000, ambazo kati ya hizo, Shilingi 340,150,300,000 zikiwa ni za ndani na Shilingi 230,380,730,000 ni za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii na kuwashukuru pia Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje (Mb) na Katibu Mkuu wa Miundombinu Mhandisi Omar A. Chambo. Aidha, tunampongeza Ndugu Ephraim C. Mrema, Mkurugenzi Mkuu wa TANROADS, kwa kusimamia ujenzi wa barabara kwa ufanisi mkubwa akishirikiana na Wataalam wenzake. Ushirikiano, ushauri na utaalam wao, umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania katika ibara ya 63(3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati hii, kwa kujituma wakati wote wa kutekeleza ratiba za Kamati na hasa kwa mchango wao mkubwa wa kupitia na kuchambua Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii kwa umakini mkubwa na hivyo kufanikisha na kuiboresha taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwatambua Wajumbe wanaounda Kamati ya Miundombinu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Alhaji Mohammed Hamisi Missanga – Mwenyekiti, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela – Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mheshimiwa Pascal Constatine Degera, Mheshimiwa Bakari Said Faki, Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mheshimiwa Dkt. Festus Bulugu Limbu, Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Joyce Martin Masunga, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Dkt. Getrude Ibengwe Mongella, Mheshimiwa Alhaj Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, Mheshimiwa Sigfrid Said Ng'itu, Mheshimiwa Mwaka Abdulrahman Ramadhan, Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi na Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Didimu Kashililah, Katibu wa Kamati ya Miundombinu, Bibi Justina Mwaja Shauri na Bwana James John Warburg, kwa kuandaa Taarifa hii. Aidha, naomba niwashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa bidii na utendaji wao mzuri katika hatua zote za maandalizi ya Taarifa hii na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba fedha zilizombwa na Mheshimiwa Waziri, zihadiliwe na ziidhinishwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Alhaj Missanga, kwa kutoa maoni na ushauri kutoka Kamati ya Miundombinu, iliyochambua mapendekezo na mawasilisho ya bajeti hii.

Sasa naomba Waheshimiwa Wabunge, nimwite Msemaji Mkoo wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii na ninamwona Mheshimiwa Zitto Kabwe. Mheshimiwa Zitto Kabwe, tafadhali maoni ya Kambi ya Upinzani.

**MHE. KABWE Z. ZITTO - MSEMADI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni ya 99(7), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kuwa siku chache zilizopita, tumepata misiba mikubwa miwili. Kwanza ni msiba wa Kaimu Mufti, Sheikh Gorogosi na wa pili ni wa Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa Haroub Othman. Misiba hii miwili ni mizito sana kwa Taifa letu, kutokana na michango ya watu hawa katika jamii. Sheikh Gorogosi, amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha ustawi wa Jamii ya Waislamu kama Kiongozi wa Dini na ametoa mchango mkubwa sana katika kueneza maadili ya Dini. Mungu aziweke roho za marehemu mahala pema peponi. (Amin)

Profesa Haroub Othman, mmoja wa wasomi waandamizi hapa nchini ni mwalimu wangu na mlezi wangu katika masuala ya uongozi. Taifa limepoteza, Zanzibar imepoteza na Vijana wamepoteza. Wamepoteza msomi mahiri, mwanataluma aliyebobea na Mzalendo asiye na mashaka. Kwa niaba wa vijana wote waliosomeshwa na Haroub na tuliokuwa tunalelewa na Haroub kiuongozi, natoa salamu za pole kwa Profesa Saida Yahya Othman, kwa kuondokewa na rafiki yake kipenzi. Kama alivyoandika mwanaharakati Ali Saleh; Haroub amekwenda, Haroub anaishi. Tutajitahidi kuishi kwa hazina ya maarifa uliyotuachia kupitia maandiko yako na aina ya maisha yake ni shule ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed (Mb.) na Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Willibrod Peter Slaa (Mb.), kwa kazi kubwa na nzuri ya kuongoza Kambi yetu kwa mafanikio makubwa sana. Vile vile napenda kumshukuru kwa dhati, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki (Mb.), kama Naibu Waziri Kivuli wa Miundombinu. Hotuba hii imefika hapa kwa msaada mkubwa sana wa Mheshimiwa Bakari Shamis Faki.

Nawashukuru pia Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani walio katika Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Khadija Al-Qassmy, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mkiwa Kiwanga, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, kwa msaada mkubwa walionipa katika kuandaa hotuba hii. Ninamhakikishia Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni na Watanzania wote

Wazalendo kuwa, nitaendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote ili kusogeza mbele maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Kamati ya Miundombinu, kwa ziara waliofanya katika Mkoa wa Kigoma, kwani ziara ile imeleta mafanikio makubwa sana toka wameondoka kuna mabadiliko makubwa sana ambayo yamefanyika. Kwa hiyo, napenda kwa niaba ya Wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu, kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu Mheshimiwa Missanga, kwa ziara ile ya Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru Wananchi wa Jimbo langu la Kigoma Kaskazini, kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kazi zangu. Kama nilivyosema, mwaka jana nilipokuwa nawasilisha hotuba yangu, tumefarijika sana sisi watu wa Kigoma Kaskazini, kupata barabara mbili za lami. Barabara ya Mwandiga – Manvovu na ile ya Kigoma Kidahwe. Ninajua ujenzi wa barabara hizi utaleta maneno mengi ya kisiasa, lakini ukweli utabaki pale pale kuwa Barabara hizi zimejengwa katika kipindi ambacho mimi ni Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kaskazini. Barabara hii haijengwi kwa fedha za chama chochote cha siasa. Fedha za walipa kodi wa nchi ndio zinajenga barabara. Hakuna chama cha siasa chenye fedha!

Sasa watajitokeza watu kusema kwamba, Ilani ya Uchaguzi ya CCM, inatekelezwa kwa ujenzi wa barabara hii. Hizi barabara zimetokana na juhudzi za Wabunge wa Kigoma na Viongozi wa Mkoa wa Kigoma, kwa pamoja bila kujali itikadi zao. Kiongozi yejote anayetaka kutugawa kwa kuanza kusema Serikali ya CCM imejenga barabara hizi, nataka kumhakikishia kwamba, sisi watu wa Kigoma hatugawiki kwenye masuala ya watu wa Kigoma. Tuliachwa nyuma sana na kutengwa, hivi sasa hatupewi hisani kwa miradi hii. Walio kwenye madaraka wanatekeleza wajibu wao, ambao hawakuwa wanatekeleza miaka yote toka nchi yetu ipate uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mamlaka ya Bandari Tanzania, kwa kuanza mchakato wa ujenzi wa ICD pale Kigoma ili kuanza utekelezaji wa Kigoma kuwa eneo maalumu la kiuchumi (SEZ). Vile vile kuanza ujenzi wa gati katika Kijiji cha Kagunga ili kuimarisha Biashara katika mpaka huu na Nchi ya Burundi. Ninapenda pia kuwashukuru kwa dhati, Shirika la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), kwa kuona mapema faida zitakazotokana na kufunguka kwa Mkoa wa Kigoma na kuanza mchakato wa Mradi Kabambe wa Kituo cha Biashara eneo la Mwandiga (Mwandiga International Motel). Ninachukua fursa hii, kuwataka Watanzania na Mashirika mengine ya Umma na Binafsi waje kuwekeza Kigoma na hasa katika eneo hili ambalo tayari NSSF wamefungua njia. Kigoma ni njema, wawekezaji wa ndani na nje mnakaribishwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika hotuba yangu mwaka jana, katika Taarifa ya Hali ya Umaskini ya Mwaka 2007 (Poverty and Human Development Report 2007), imeonekana kuwa itakuwa ni vigumu sana kwa Tanzania kufikia malengo ya MKUKUTA, kwani kasi ya ukuaji wa uchumi imekuwa chini ya viwango vinavyotakiwa. Moja ya suala ambalo limeainishwa katika Sura ya Tatu ya Taarifa hiyo

ni kuwa, kama Taifa tumekuwa na rasilimali chache sana za kuweza kufikia malengo ya ukuaji uchumi, lakini zaidi ni kuwa rasilimali chache tulizonazo tunazitawanya kila mahali ilimradi kila mtu apate bila mkakati maalumu. Tunaridhishana! Hali hii imedhihirika hapa Bungeni katika mjadala wa Bajeti ambapo Wabunge wanaona ni bora kila mtu apate kamradi bila kujali mipango mikubwa zaidi ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hiyo ilionya kuwa, bila kuweka mkakati mpya wa kutumia rasilimali za nchi kwa malengo mahususi, hatutapiga hatua katika maendeleo ya uchumi (given our limited resources there is need for a clear direction for resource mobilization and a concentration of efforts – Tanzania needs a well focused national growth strategy).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inatambua kuwa, sekta ya ujenzi imekua ikichangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Ukiangalia Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2008, utakutana na takwimu ambazo zinaonesha kuwa Sekta ya Ujenzi imekuwa zaidi, ukilinganisha na kipindi kama hicho kwa mwaka 2006 na Mwaka 2007. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za ujenzi kwa mwaka 2008, kilikuwa asilimia 10.5 ikilinganishwa na asilimia 9.7 mwaka 2007. Ukuaji huu ulichangiwa na kuongezeka kwa ujenzi wa barabara na madaraja, ujenzi wa majengo ya kuishi na yasiyo ya kuishi na upanuzi wa miundombinu ya maji. Aidha, mchango wa shughuli za ujenzi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 7.7 mwaka 2008, ikilinganishwa na asilimia 7.8 mwaka 2007. Hapa inaonesha kuwa, mchango wa Sekta ya Ujenzi katika Pato la Taifa umeshuka kwa asilimia 0.1 kwa kulinganisha na mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha 2009/2010, Kambi ya Upinzani itajikita tena katika maeneo yenye umuhimu wa kipekee katika Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti ya Mwaka 2008/2009, fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa na Hazina kwa Wizara ya Miundombinu ni shilingi 230 bilioni katika fedha za ndani, ambazo ni asilimia 64 tu ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Kwa Upande wa fedha za wafadhili, zimetoka shilingi 80 bilioni tu ambazo ni sawa na asilimia 34. Hata hivyo, kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida, 91% ya fedha ziliweza kutoka. Hii inaonesha ni jinsi gani ambavyo Serikali inajali zaidi matumizi ya kawaida na kutotoa kipaumbele kwa matumizi ya maendeleo, ambapo zaidi ya asilimia 40 ya fedha haijatolewa na kutumika. Hali hii inarudisha nyuma juhudzi za uboreshaji wa miundombinu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu wa fedha 2009/2010, fedha zinazoombwani shilingi 570.531billioni, kati ya hizo shilingi 340.13 billioni ni fedha za ndani na shilingi 230.4 billioni ni fedha za nje. Kwa kuangalia uwiano wa bajeti hizi za miaka miwili ni dhahiri kuwa, bajeti ya mwaka huu inapewa fedha pungufu ya ile ya mwaka jana kwa shilingi 21.651 billioni. Aidha, mahitaji halisi ya Wizara kwa fedha za ndani yalikuwa shilingi 514.047 billioni, lakini ikatengewa shilingi 340.15 billioni ikiwa ni pungufu ya shilingi 75.897 billioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Hotuba ya Waziri wa Fedha na sura ya bajeti, inaonesha kuwa fedha za maendeleo ni shilingi 2.825 trillion, ambazo zote ni fedha za nje. Kambi ya Upinzani inaomba kufafanuliwa kama ndiyo hivyo, hizi fedha za maendeleo kwa Wizara ya Miundombinu shilingi 340.13 billioni za ndani zinatoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu ya mwaka uliopita, nilionesa kuwa, matengenezo ya kawaida ya barabara kuu ya kilometra 4,677.7 yalikamilishwa mwaka 2007, ikilinganishwa na kilometra 5,080.3 mwaka 2006. Hapa panaonesha upungufu wa kilometra zipatazo 402.6, ukilinganisha na mwaka 2006. Hoja iliyotolewa na Serikali kwenye upungufu huu wa kupungua kwa ujenzi kwenye Sekta ya Barabara ni kutokana na utekelezaji wa sheria mpya ya manunuzi, ambapo mchakato wa kutafuta makandarasi unachukua muda mrefu. Ninaomba majibu ya serikali kuhusiana na hali ya sasa ya ujenzi wa barabara na kama upungufu wa mwaka jana tayari umekwisha shughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko sana kutoka kwa makandarasi kuwa malipo ya fedha zao yanachelewa mno na wakati mwingine hawapati kabisa. Licha ya juhudini ambazo zimeonekana za kuibua miradi mipyä ya barabara na hasa hasa ufunguzi wa barabara za Magharibi katika Mikoa ya Kigoma, Tabora na Rukwa, kama wakandarasi hawalipwi vizuri watakata tamaa na nchi kupata hasara. Suala hili la madeni ya wakandarasi lishughulikiwe haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika siku za hivi karibuni, kumekuwa na malalamiko mengi ya makandarasi kunyanganywa kazi zao baada ya kushindwa kutimiza masharti ya mikataba. Malalamiko hayo yamepelekea vyombo vyä habari kutoa habari mbalimbali kuhusiana na hasara ambayo inasemekana TANROADS watapata kutokana na kuvunjwa kwa mikataba yao. Ninachotahadharisha ni kwamba, tukikumbatia makandarasi wasiotimiza masharti na kujenga barabara ambazo hazina viwango au zenye viwango vyä ovyo ovyo, Taifa litapata hasara. Ninaitaka TANROADS iendelee kuwabana makandarasi ili kutimiza masharti ya mikataba yao na hivyo kupelekeea nchi kupata barabara nzuri na salama ili kukuza uchumi wa Taifa. Pasiwe na uonevu dhidi ya Mkandarasi yejote, bali Mkandarasi yejote anaebabaisha kazi, asivumiliwe hata kidogo. Vyombo vyä habari vijaribu kuhakikisha kuwa, habari zinazoandikwa ni sahihi bila mawaa kwani ni rahisi sana Makandarasi wababaishaji kutumia media kuhalalisha maovu yao.

Kambi ya Upinzani inaitahadharisha Serikali kwamba, miradi ya miundombinu iangalie sana maeneo ambayo bado hayajafunguliwa na kuyafungua. Kipaumbele cha Barabara za Manyoni – Itigi – Tabora – Urambo mpaka Kigoma na Iringa – Dodoma – Kondoa – Babati mpaka Arusha, hakipaswi kupuuzwa katika suala la miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Dodoma – Iringa yenye km 267 bado ipo kwenye hatua ya upembusi yakinifu na usanifu na mwaka 2008/09, Serikali ilitenga fedha za ndani shilingi 50m tu! Huu upembusi yakinifu unaisha lini na Barabara hii itaanza kujengwa lini mbona tunaona mabilioni ya fedha yanatolewa kwenye barabara

ambazo wala hatujawahi kusikia kama upembuzi yakinifu umewahi kufanyika katika miaka ya hivi karibuni sembuse barabara hii ambayo inaimbwu kila mwaka? Kuna kigugumizi gani katika kujenga barabara zinazounganisha nchi na Makao Makuu Dodoma (Great North Road). Kambi ya Upinzani inataka maelezo ya kina, kuhusu barabara hii muhimu sana kwa Taifa na ninamtaka Waziri atuletee ratiba ya ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ya Dodoma Babati yeny e km 261, Serikali imetenga shilingi 10 bilioni ili kupitia kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu. Ninamwomba Waziri alifafanulie Bunge; upembuzi yakinifu umekwishafanyika miaka iliyopita halafu serikali inatenga fedha kupitia upya upembuzi yakinifu; nini kimetokea hapa kati kati? Wakati mwaka 2008/09, Serikali ilitumia shilingi 574 millioni kufanya upembuzi yakinifu kwa Barabara ya Dodoma – Iringa, mwaka 2009/10 serikali inapanga kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu wa Barabara ya Dodoma – Babati kwa sh 10 bilioni. Ninaomba maelezo ya kina kuhusu suala hili kutoka kwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Serikali ilichukua fedha kutoka TCRA kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya Msata – Bagamoyo (Wazo Hill – Bagamoyo – Msata, 107 km). Barabara hii ni muhimu sana kwa ajili ya kukuza utalii katika Mji wa Bagamoyo. Hata hivyo, fedha hizi bado hazijatumika na zipo Benki Kuu, huku gharama za ujenzi zikizidi kupanda. Naomba Waziri aliye maelezo Bunge, fedha jumla ya shilingi 3bn ambazo zilitolewa TCRA toka mwaka 2006/2007 na kuwekwa katika akaunti Benki Kuu; kwa nini hazijatumika na Taifa limepata hasara kiasi gani kwa kuchelewa huku? Vile vile fedha zinazoombwa katika mwaka huu wa fedha jumla ya shilingi 6.3 bilioni imejumuisha fedha hizo za TCRA? Nina mashaka sana na tabia ya kuchukua fedha na kuzisahafulisha! Ninaomba maelezo ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilisema, nchi yetu imejaliwa na Mungu kwa kuzungukwa na Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu matatu, ambayo ni Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria. Mungu angeweza kutunyima rasilimali nyingine zote na akatuacha na rasilimali hizi tu na tungeweza kukua kama Taifa kutohana na utajiri unaoweza kuzalishwa na Rasilimali hizi. Hata hivyo, Mungu ametujaalia mengine mengi sana kama Madini, Mito yeny e kuzalisha Umeme na Watu wapenda amani na wakarimu. Hata hivyo, bado hatujaweza kutumia rasilimali hizi kujiendeze inavyopaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tuko katika ushindani wa kibiashara ndani ya Jumuiya yetu ya Afrika ya Mashariki na SADC, Bandari yetu ya Dar es Salaam, mwaka 2008 ilihudumia shehena yeny e jumla ya tani 2,316,000 ikilinganishwa na tani 5,703,000 mwaka 2007, sawa na upungufu wa asilimia 59.4, sababu kubwa ikiwa ni kushuka kwa tija ya kupakua na kupakia mizigo na ushindani wa bandari za jirani, Mombasa, Beira na Durban. Meli zilizohudumiwa mwaka 2008 ni 697, ukilinganisha na 3,038 mwaka 2007, sawa na asilimia 77.1. Hivyo hivyo kwa Bandari ya Mtwara, ilihudumia tani 82,000 mwaka 2008 kulinganisha na tani 112,000 mwaka 2007, sawa na upungufu wa asilimia 26.8. Meli zilizofika ni 36 mwaka 2008, ukilinganisha na 99 mwaka 2007, sawa na upungufu wa asilimia 63.6. Bandari ya Tanga ilihudumia shehena ya tani 178,000 mwaka 2008, ukilinganisha na tani 542,000 mwaka 2007, sawa na upungufu wa asilimia 67.2

(Hali ya Uchumi Uk.196/197). Meli zilizokuwa zinasafirisha mizigo na abiria na kutumia Bandari ya Dar es Salaam zimepungua toka 5232 mwaka 2000 na kufikia meli 4154 mwaka 2006 na 697 mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati washindani wetu wanapanua na kuboresha bandari zao, mfano, Kenya wamewekeza US\$200 milioni kwa upanuzi wa Bandari ya Mombasa na ina uwezo wa kuingiza meli zenyenye uzito wa tani 100,000; sisi Bandari ya Dar es salaam haiwezi kuingiza meli yenye ukubwa huo, hivyo hata ule mpango wetu wa kuleta mafuta in bulk, unaweza kuwa ghali ukilinganisha na Kenya, kutokana na ukubwa wa meli inayoweza kufunga gati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kurejea shukrani zangu za dhati kwa Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa kuanza mradi wa kujenga gati katika maziwa. Shukrani za dhati kwa magati ya Ziwa Tanganyika na hasa yale ya Kalya (Kigoma Kusini) na Kagunga (Kigoma Kaskazini). Magati haya yataongeza juhudzi za uzalishaji mali za watu wa Kigoma na hivyo kukuza uchumi. Gati ya Kagunga ni ukombozi mkubwa sana kwa watu wa Kagunga, kwani Kagunga ni mpaka na nchi jirani ya Burundi. Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma inajenga soko pale Kagunga na hivyo uamuzi wa TPA kujenga magati katika Ziwa Tanganyika na hasa hili Gati la Kagunga, unaunga mkono juhudzi za Halmashauri ya Wilaya katika kupanua shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda Serikali na hasa Waziri wa Miundombinu, alieleze Bunge sababu zilizopelekea kufanya mabadiliko ya Sheria ya Bandari na kuziondoa Bandari za Maziwa katika Kampuni ya Huduma za Meli (Marine Services Company). Ninapata wasiwasi kuwa, Kampuni hii itashindwa kabisa kufanya kazi kwa faida kwani umiliki wa Bandari kama zile za Mwanza na Kigoma, ungeweza kuwasaidia kupata mapato zaidi. Ninapenda kupata ufanuzi wa Waziri katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima pawepo na mkakati madhubuti wa kuziimarisha Bandari za Mtwara na Tanga ili kuhakikisha kuwa, meli kubwa za mizigo zinaweza kutia nanga kwenye maeneo hayo. Hatua hii inalenga kwenye kuongeza mapato zaidi na hata kupanua wigo wa soko la malighafi zinazozalishwa hapa nchini, kwa mfano, kama Bandari ya Tanga itaimarishwa, itawezesha usafirishaji wa malighafi yatokanayo na mkonge kusafirishwa kwa urahisi zaidi kuliko hali ilivyo hivi sasa, kwani ni lazima malighafi hizo zisafirishwe kwanza kwa njia ya Barabara hadi Dar es Salaam ndipo zipakiwe kwenye meli. Mkakati wa Bandari ya Tanga ni lazima ufungamanishwe na Mkakati wa Sekta ya Madini. Nimeona juhudzi za kuimarisha Bandari ya Tanga. Kambi ya Upinzani inataka juhudzi hizo ziimarishwe ili kuhahakikisha kuwa, Bandari ya Tanga inachukua nafasi yake muhimu katika uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Mtwara maelezo yake hayatofautiani na ya Tanga. Licha ya kusafirisha Korosho na mazao ya misitu, Bandari ya Mtwara ni muhimu sana kufungamanishwa na Miradi ya Mchuchuma na Liganga. Vile vile Bandari hii yaweza kuwa ni bandari ya nanga kwa uvuvi wa Bahari Kuu. Kambi ya Upinzani inataka maelezo ya serikali kuhusiana na maendeleo ya upanuzi wa Bandari ya Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri na hasa kwa njia ya maji Ziwa Victoria, umekuwa hauridhishi kwani meli ambazo zinatumika kuwasafirisha abiria zimekuwa zikilalamikiwa kila mara kutokana na meli hizo kuwa ama ni chakavu sana kutokana na kukaa muda mrefu bila kufanyiwa matengenezo au kutokana na kuwa ni za zamani sana. Meli hizi zinahatarisha maisha ya wananchi wetu kila wanaposafiri, hivyo Kambi ya Upinzani inaitaka serikali kutoa maelezo ya kina juu ya hali hii ya kuhatarisha maisha ya wananchi wetu na kuna mkakati gani wa kuhakikisha kuwa, wananchi wetu wanakuwa salama kila wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko kuhusu usafiri wa Reli ya Kati ni makubwa mno kutoka kwa wananchi. Malalamiko hayo niliyaeleza mwaka jana katika hotuba yangu ya Kambi ya Upinzani. Wabunge wamezugumza humu Bungeni, kuhusiana na adha ya usafiri wa Reli. Waziri Mkuu, alitoa majibu kuhusiana na suala hili na kueleza kwamba, kwa kiasi kikubwa sisi ni chanzo cha matatizo haya na siyo mwekezaji ambaye amekodisha Reli hii kwa ubia kati ya Serikali ya Tanzania na Kampuni ya Rites ya India. Toka mwaka jana hadi sasa, Waziri Mkuu ameanza kukubaliana na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kuwa, Mwekezaji ana matatizo makubwa kuliko ya kwetu sisi, kwani hali ya TRL kiutendaji inazidi kuwa mbaya kila kukicha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuona kuwa, usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya reli umeteremka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, usafirishaji wa mizigo wa TRL umepungua toka tani 1,169,000 mwaka 2005 mpaka tani 429,000 mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu hizi hivi kweli Serikali iko makini katika kutumia jiografia yetu kujiongezea mapato kama programu zetu za Vision 2025, Mkukuta, Mini Tiger na kadhalika zinavyofafanua. Je, nchi yetu itatokana na kilema cha kutegemea mikopo na misaada?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na udhaifu huu, Serikali ililipa shilingi 4.4 billion kwa RAHCO ili kufuta madeni mbalimbali ya lilikokuwa Shirika la Reli bila idhini ya Kamati ya Madeni ya Taifa (NDMC) na hakuna ushahidi kuwa kampuni hizo zilirejesha kiasi hiki (Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali Uk.17).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali inatafuta fedha kuokoa Shirika (TRL), huku tunatoa fedha bila ya nyaraka muhimu za kuthibitisha malipo, Serikali hajatueleza ni fedha kiasi gani wawezekaji wamewekeza hadi sasa, kwani ukisoma Taarifa ya Utekelezaji wa Ahadi za Serikali inasema, Serikali kwa kushirikiana na mwekezaji, inaendelea kutafuta fedha ili kutekeleza miradi hii (uk.227).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge la 11, Mheshimiwa Said Amour Arfi, alitoa hoja binafsi hapa Bungeni kuhusu hali ya Shirika la Reli na Serikali iliahidi kutoa majibu. Malalamiko kuhusu Mkataba kati ya Serikali na RITES, yamekuwa makubwa sana. Serikali imeamua sasa kutoa fedha kama sehemu ya mtaji wake ili kuwa na haki

sawa katika Kampuni ya TRL. Kambi ya Upinzani inaitaka serikali kuharakisha mazungumzo ya kurekebisha Mkataba huo na kuzingatia kuwa ni lazima nafasi za Uongozi wa Kampuni (Menejimenti), zizingatie uwiano wa Hisa za kila Mhisa. Kwa mfano, Kambi ya Upinzani inatarajia kuwa, iwapo Mtendaji Mkuu wa Kampuni atakuwa anatoka RITES, basi Mkurugenzi wa Fedha atoke Serikali ya Tanzania. Hii itasaidia sana kuweza kushiriki moja kwa moja kulinda maslahi ya Tanzania kama mwenye 49% ya hisa katika TRL.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilizungumzia Stesheni za Reli kutumika kama vituo vya biashara kama ilivyo viwanja vya ndege kwa usafiri wa anga. Stesheni za Reli zina umuhimu mkubwa sana kwa usafiri wa Reli. Kwa muda mrefu sana, Stesheni za Reli zimekuwa ndio maofisi ya Shirika la Reli na pia zimekuwa zinamilikiwa kwa pamoja na Reli. Stesheni za Reli, hasa zile stesheni kubwa kama vile Tabora, Kigoma, Urambo, Mpanda, Kilosa, Dodoma, Morogoro, Tanga, Mwanza na Dar es Salaam, zimekuwa hazitumiki kwa asilimia 100 na kwa kweli stesheni nyingine zimekuwa chafu na hazihudumiwi ipasavyo. Sijui katika mkataba wa kukodisha Reli na pia makubaliano ya wanahisa wamesema nini kuhusu Stesheni hizi na hasa umilliki wake? Kambi ya Upinzani inaomba kupata ufanuzi kuhusu suala hili na kama mkakati wa kutumia Stesheni za Reli kama vituo vya biashara umeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, RAHCO ambao ndio wenyewe jukumu la kuendeleza miundombinu ya Reli, katika mwaka huu wa fedha imepewa jumla ya shilingi bilioni moja tu wakati maombi yao yanazidi shilingi 80 bilioni. Kambi ya Upinzani inaitaka serikali iwe makini katika vipaumbele vyake, kwani muundombinu wa Reli ni muhimu sana kwa Uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza mwaka uliopita, nafasi ya Tanzania kijiografia inatoa fursa kubwa kwa usafiri wa anga kuwa na manufaa kwa Taifa. Hivi sasa Taifa letu lina viwanja vya ndege viwili vya Kimataifa, yaani Julius Nyerere International Airport na Kilimanjaro International Airport. Kiwanja cha Songwe kinamaliziwa kujengwa. Viwanja vya Ndege vya Mwanza, Kigoma, Tanga, Mtwara na Mafia ni muhimu sana kwa ukuaaji wa sekta na uchumi kwa ujumla. Vile vile Taifa linamiliki Shirika la Ndege, yaani ATCL.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya Shirika la ATCL ni tete na kumekuwa kuna kutupiana mpira katika ya Uongozi wa Shirika la Serikali. Katika mwaka wa Fedha wa 2009/10, Serikali imeitengea ATCL shilingi bilioni moja, katika shilingi 20 zinazotakiwa. Katika hali hii, Shirika haliwezi kuinuka. Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kama imeshindwa kutoa mtaji kwa Shirika hili, tena mtaji wa kutosha, hakuna sababu ya kuendelea kuwa Shirika. Serikali itoe tamko Bungeni kuna mkakati gani wa kunusuru ATCL? Watanzania wamechoshwa na maneno ya kurushiana mpira, wakati mwenye hisa ameshindwa kutoa mtaji wa kutosha. Kwa hali ya Tanzania ilivyo kijiografia, ATCL ikipewa mtaji wa kutosha na mwenye hisa, Watanzania waliopo katika Shirika hawatashindwa kuliendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu kuhusu maoni ya Upinzani katika Wizara hii mwaka uliopita, nilizungumzia suala la miundombinu ya viwanja vyao ndege.

Upanuzi wa viwanja vyao ndege ni eneo ambalo halijatiliwa mkazo wa kutosha na pia halipewi kipaumbele cha kutosha. Kutokana na kukua kwa kasi ya usafiri wa anga hapa nchini na ikizingatiwa kuwa Sekta ya Utalii inakua kwa kasi kubwa, basi haina budi kuboresha viwanja vyetu vyao ndege na kuviendesha kibiashara. Hili litawezesha kuvutia watalii wengi kuja nchini moja kwa moja, kwani kwa sasa watalii wengi kutoka Ulaya na Marekani, huwa wanaishia nchini Kenya kutokana na ubora wa viwanja vyao vyao ndege na hata mashirika mengi ya kimataifa huwa safari zake zinaishia Nchini Kenya na ndipo wanabadilisha ama wanaamua kubakia huko moja kwa moja.

Mheshmiwa Spika, upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam bado imekuwa ni hadithi za alinacha. Wakazi wa Kipawa ambao wanapaswa kulipwa fidia ya nyumba zao, wamekuwa katika tataruki muda wote. Mradi unapochelewa, maana yake gharama za mradi zinaongezeka sana. Serikali ililiambia Bunge kuwa, kuna mwekezaji kutoka China. Taarifa nilizonazo ni kwamba, mazungumzo na mwekezaji huyu yanachukua muda mrefu. Ninaomba Waziri aliambie Bunge lako Tukufu ni lini mradi huu wa upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam unaanza? Ujenzi wa Terminal III una umuhimu mkubwa sana kwa Uchumi wa Taifa na ingawa Kambi ya Upinzani ilifikiria vinginevyo mwaka jana, lakini baadae tuliona umuhimu wa mradi huu. Ninamwomba Waziri, alieleze Bunge hatma ya Wakazi wa Kipawa katika malipo yao katika maelezo ya hatma ya Mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inapenda pia kusisitiza umuhimu wa viwanja vyao ndege vyao pembezoni mwa nchi. Uwanja wa Ndege wa Mwanza na ule wa Kigoma ni viwanja muhimu sana katika eneo la Maziwa Makuu. Ni muhimu Uwanja wa Ndege wa Kigoma, ukapewa kipaumbele pekee kwani Uwanja huu ukitangazwa vizuri utakuwa ni stop over ya ndege kutoka Congo na Burundi, kwa ajili ya kuleta abiria Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam na kwenda ughaibuni. Mamlaka ya Viwanja vyao Ndege, iliangulari suala hili kuweka mkakati wa pekee wa uendeshaji wa Uwanja huu ili Taifa lifaidike lakini pia makampuni ya ndege nchini nayo yafaidike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano wa Nne wa Bunge la Tisa, niliuliza swali namba 61, kuhusu Mkataba wa Uendeshaji wa Uwanja wa Ndege wa KIA. Serikali iliingia Mkataba na Kampuni ya KADCO (Serikali ni mhisa katika kampuni hii, ikiwa na hisa 24%) wa kuendesha Uwanja wa Ndege wa KIA kwa miaka 25 kwa tozo ya Dola 1000 kila Mwaka. Pamoja na Serikali, wanahisa wengine katika Kampuni hii ya KADCO ni Mott-Mcdonald Ltd, SA Infrastructure na Inter Consult Ltd.

Katika swali langu, nilitaka Serikali iulete Bungeni Mkataba huu wa KIA na kutazamwa na Bunge kama unakidhi maslahi ya Taifa. Serikali ilijibu kwa kusema kuwa, kipengele cha 30.4 kinazuia watu wasiohusika kuona Mkataba huo (kwamba Bunge lako tukufu halihusiki na Mikataba hii). Hata hivyo, Serikali ilikiri kuwa inafanya mapitio ya Mkataba huo; mpaka sasa mapitio ya Mkataba huo hayajafahamika.

Mheshimiwa Spika, Taarifa nilizo ni kwamba, hivi sasa Serikali inafanya utaratibu wa kununua hisa zote za Mott-McDonald na hivyo kurejesha KIA mikononi mwa Serikali. Kambi ya Upinzani inapenda kwanza, kujua matokeo ya mazungumzo ya kubadili mkataba ule ambao tunaamini haukuwa na maslahi kwa Taifa. Serikali inapata wapi nguvu za kwenda kununua hisa za kampuni ambayo imeingia nayo mkataba ambao Wabunge wana mashaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Taarifa za Serikali (Treasury Registrar Statement of Loans and Guarantees), Serikali inaidai Kampuni ya KADCO shilingi bilioni tano, mkopo ambao walipewa kwa ajili ya vifaa vyta huduma za kuogoza ndege. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze kinagaubaga kuhusu ni nini kinaendelea katika ukodishwaji wa Uwanja wa KIA kwa miaka 25 kwa tozo ya dola 1000 kwa mwaka na ni kwa nini Serikali inataka sasa kununua hisa za mmoja wa wabia? Nini kinaendelea KIA?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi hii uliyonipa na naomba kuwasilisha. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Naomba nichukue nafasi hii, nikushukuru Mheshimiwa Zitto Kabwe, kwa kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, kwa maana ya Msemaji Mkuu wa Wizara hiyo. Waheshimiwa Wabunge, sasa baada ya kusikiliza Hotuba ya Bajeti kutoka kwa Mheshimiwa Waziri na baada ya kusikiliza Maoni na Ushauri kutoka kwenye Kamati inayohusika na Wizara hiyo, kwa maana ya Kamati ya Miundombinu na baada ya kusikia Maoni na Ushauri kutoka Kambi ya Upinzani, yaliyowasilishwa muda mfupi uliopita na Mheshimiwa Zitto Kabwe; sasa tutaingia kwenye mchango wa pamoja.

Nichukue nafasi hii, kusema yafuatayo: Waheshimiwa Wabunge, orodha niliyonayo ina wachangiaji 49 na Wizara hii kwa mujibu wa ratiba yetu, itatupasa tuhitimishe hoja hii kesho. Sasa katika wachangiaji hao, wachangiaji 20 ni wale ambao hawajachangia hata mara moja na wao waliamua kuomba rasmi kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu na hivyo wakaacha hotuba zile zote zilizotangulia na kwa mujibu wa Kiti, tulikubaliana hao wapewe kipaumbele kwanza. Kwa hiyo, ninaomba mkubali kwamba, orodha hii ya wachangiaji 20 ndiyo itakayopewa kipaumbele. Baada ya hapo kama muda ukituruhusu, tutaingia kwenye kundi lile la pili la wale waliochangia mara moja na hao wapo Wabunge 28, akiwemo Seneta Mheshimiwa Masilingi yupo katika kundi hilo. Baada ya hapo, tutaangalia kama nafasi itaturuhusu tutabakiwa na mchangiaji mmoja ambaye amechangia mara tatu, Mheshimiwa Mohammed Mnyaa na yeche ameomba tena kuchangia kwenye Hotuba ya Wizara hii.

Kwa hiyo, niliomba niyaseme hayo Waheshimiwa Wabunge ili wote muelewe Kiti kitakuwa kinaongozaje mchango wa hotuba kupitia kwenu. Sasa niseme yafuatayo katika wachangiaji hawa 20. Orodha ya wachangiaji hawa 28 tutaendelea kuizingatia kwa mujibu wa jinsia lakini vilevile na masuala mengine yatazingatiwa. Sasa wachangiaji wangu wa kwanza kabisa tutaanza na Mheshimiwa Said Nkumba, atafatiwa na Mheshimiwa Zabein Muhita, atafuata Aziza Sleyum Ally, atafuatiwa na Mheshimiwa Benson Mpesa, halafu Mheshimiwa Annia Chaurembo ajiandae.

**MHE. JUMA S. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza, naomba niipongeze Serikali ya CCM, kwa utekelezaji wa Ilani katika maeneo yote nchini bila kujali Wabunge waliopo ni wa Chama Tawala au ni Vyama vya Upinzani. Naipongeza kwa Utawala Bora, hasa ilipoamua kujenga Barabara ya Kigoma – Kidawa na Manyovu –Mwandiga. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishukuru Serikali kwa niaba ya Wananchi wa Sikonge, kwa kukubali maombi ya kupandisha hadhi Barabara ya Tutuo – Mole – Ibumba – Urambo yenye km 72, lakini vile vile Barabara ya Sikonge – Mibono – Kipili. Kwenye barabara ya kwanza sina matatizo, lakini barabara ile ya pili, naiomba sana Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu, barabara hii ina urefu wa km 192, km 144 bado hazijafunguliwa. Kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali na nimeangalia kwenye vitabu vyote sioni kama imepangiwa fedha mwaka huu. Kwa hiyo, naomba taratibu za kuipangia fedha ili iweze kufunguliwa zifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Nzega – Ipole – Rungwa, Kigoma – Tabora – Manyoni na Ipole – Mpanda ni barabara za vumbi. Sasa kila mara zinatengenezwa na wenzetu wa TANROAD, mimi huwa mara chache sana natoa pongezi kutokana na kazi nzuri ambayo wanaifanya, angalau kutufanya tuendelee kupita katika kipindi hasa cha masika. Napenda niwapongeze sana watu wa TANROAD kupitia CEO, pamoja na wasaidizi wake wa mikoani, ambao wanafanya kazi nzuri. Ndugu zangu, pokeeni hizi salamu ambazo huwa zinatolewa mara chache sana. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nilizozitaja hapo juu zote kitovu chake ni Tabora, lakini zimeunganishwa kwa vumbi kama nilivyosema. Pamoja na jitihada za Wananchi wa Tabora kulima mazao mbalimbali; pamba, tumbaku, mpunga alizeti na mahindi, hawawezi kufanya biashara kwa sababu barabara ni mbaya. Ikifika wakati wa masika, barabara zinajifunga huwezi kutoka Mbeya kuja Tabora, huwezi ukatoka Nzega kuja Tabora, barabara ni matatizo, huwezi ukatoka Kigoma kuja Tabora. Kwa hiyo, mwaka jana tulipokuwa hapa tunalalamikia bajeti kwa mwaka 2008/2009. Waziri Mkuu alituahidi kwamba, Serikali itatupatia kwa dharura shilingi bilioni 10. Sasa nimeangalia kwenye kitabu cha maendeleo, naona zipo shilingi bilioni 6.76, zile shilingi bilioni 3.24 hazipo. Nitakuomba Mheshimiwa Waziri wakati unatoa maelezo yako ya mwisho, unapofunga hoja yako, basi tupate maelezo ya hizi hela nyininge ziko wapi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wa maeneo ya Magharibi; Tabora, Kigoma, Rukwa, pamoja na Singida, wanazungumzia sana suala la upendeleo wa ugawaji wa fedha hasa za barabara. Sasa tukizungumza suala hili la upendeleo, wengine wanununa wanatupachika majina kwamba tunagawa nchi. Mnaigawa nchi ninyi ambao mnagawa keki hii ya taifa vibaya. Mifano ninayo; mwaka 2008/2009, Wizara ilitengewa jumla ya shilingi 356.156 bilioni, fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 191.6 bilioni zilikuwa kwa ajili ya kulipa madeni makandarasi na shilingi 164.556 bilioni kwa ajili ya kazi zilizokuwa zinaendelea. Zikaonekana fedha hizo hazitoshi, Wizara ikaleta maoni ya bajeti ya ziada. Sasa wakati inaleta maombi haya ya ziada, iliorodhesha barabara ambazo fedha zile zingepatakina

shilingi bilioni 100 za ziada basi zingeweza zikafanya kazi za kuendeleza kazi ambazo ziko kwenye zile barabara ambazo nitazitaja hapa. (Makofi)

Barabara ya Dumila – Kilosa, Melela – Kilosa, Handeni – Nkata, Shinyanga – Lamadi, Manyo – Itigi – Tabora, Makurunge – Pangani, Dodoma – Babati na matengenezo dharura ya Barabara za Dar es Salaam na Sumbawanga – Mpanda, jumla ilikuwa shilingi bilioni mia moja. Fedha hizo ziliombwa na Bunge likaidhinisha. Huu ni upendeleo wa kwanza, lakini fedha zile zilipotolewa, barabara zilizopewa fedha hizo zikawa nyingine tofauti na zile ambazo ziliombewa. Barabara zilizopewa ni Handeni – Mkata, Korogwe – Handeni, Magole – Turiani, Sumbawanga – Namanyere – Mpanda, Kigoma – Lusahunga na Barabara za Dar es Salaam ziko kwa namna mbili. Mbeya – Chunya na Dumila – Ludewa – Mikumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za Shinyanga – Lamadi, Dodoma – Babati, Manyoni – Itigi na Tabora nje, huu ni upendeleo mbaya na sisi hatuwezi kukubali jambo la namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kusema hatuna utakatifu katika suala la namna hii, huo ni upendeleo wa kwanza. Upendeleo wa pili, Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora, design yake iliisha Aprili, 2009. Barabara ya Mikumi – Kilosa – Dumila design yake iliisha Mei, 2009, lakini ile ya Manyoni – Itigi – Tabora, kwa sababu watu wa kule wakiambiwa subiri wanasubiri, tunaendelea kusubiri mpaka leo. Hii ambayo design yake imeisha mwezi mmoja mbele ya Mikumi – Kilosa – Dumila, kazi imekwishaanza ni matatizo na juzi juzi hapa wameshapewa makandarasi waanze kazi, mambo ya namna hii hayawezi kuvumilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha maendeleo cha mwaka 2009/2010, ambacho kinalezea Sekta ya Barabara, zimeorodheshwa barabara zinazojengwa ikiwemo ile ya kutoka Ipole – Koga kwenda Mpanda. Naomba nitoe ushauri tu, huwezi kuanzia kujenga mkiani, hebu turudi Tabora; tunahitaji Tabora ifunguke, barabara hizi zianzie Tabora iende huko Ipole, ikifika huko itakwenda Mpanda na nyingine itakwenda Rungwa mpaka Mbeya. Naomba huo ushauri uzingatiwe, bahati nzuri Waheshimiwa Mawaziri wote, watani zangu; Mheshimiwa Kawambwa na Mheshimiwa Chibulunje, lazima muutekeleze huo ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi, napenda nimpongeze sana Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, anahangaikia sana, uwezekano wa kupata pesa ili barabara hasa inayotoka Manyoni mpaka Kigoma iweze kupata fedha na iwe ya lami. Naomba niendelee kusema haya yaliyojitekeza nyuma tusiyarudie, Rais akipata keki, itakuwa ya watu wa Magharibi, isitawanywe tena ikaenda maeneo mengine, patakuwa hapatoshi hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nilihudhuria mazishi siku moja, nikamwona kiongozi mmoja wa dini, akashika yumbi akaelekea kwenye jeneza akasema ulitoka kwa mavumbi na mavumbini utarudi. Hakusema kwamba, katika maisha yako ya duniani nako ulikuwa na mavumbi, alitenganisha mwanzo na mwisho katikati kuna likizo ya

kuwa na vumbi. Sasa sisi watu wa Tabora, Kigoma, Rukwa, hatuna likizo ya vumbi, unazaliwa ni vumbi, wakati wa maisha yako yote duniani ni mavumbi tu na wakati wa kufa ni mavumbi. Mheshimiwa Kawambwa na Mheshimiwa Chibulunje, sisi hapa tunawategemea sana mtuondolee hii adha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, naunga mkono hoja. (Makofsi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge huyo ndiye Said Nkumba, Mbunge wa Jimbo la Sikonge, Mkoani Tabora. Nakushukuru sana kwa mchango wako, kama nilivyo sema atakayefuatia ni Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Mbunge wa Jimbo la Kondo Kaskazini.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona na kunipa nafasi hii ya pili ili nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu, ambayo ni hoja ya Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii, kuwashukuru kwa dhati kabisa, Wananchi wote wa Jimbo la Kondo Kaskazini, kwa jinsi ambavyo wanani msaada wa hali ya juu na msaada wa karibu sana katika kuleta maendeleo endelevu katika Jimbo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nawapongeza kwa dhati, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kujiletea maendeleo yao na Mungu atakuwa nao na atawasaidia. Aidha, naomba nikupongeze kwa dhati, Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa; Kalumbu wangu Hezekia Chibulunje, Naibu Waziri; Injinia Omar Chambo, Katibu Mkuu; na Wakurugenzi wote wa Wizara ya Miundombinu, kwa hotuba nzuri ambayo wameitayarisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kondo Kaskazini, mimi nitaelekeza mchango wangu kwenye tatizo sugu, ambalo ni la barabara mbovu, iliy katika hali duni ya kutoka Dodoma kuititia Haneti. Haneti naisisitiza kwa sababu iko katika Jimbo la Mheshimiwa Hezekia Chibulunje, Naibu Waziri wa Miundombinu. Inapita Kondo mpaka Babati na hatimaye kufika Mijingu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara hii iko katika hali mbaya sana na katika hali ya kusikitisha kabisa, licha ya kuwa tunaizungumzia kila mwaka. Barabara hii si tu kuwa inaunganisha Mkoa wa Dodoma na Mikoa mingine, lakini pia inaunganisha nchi yetu na nchi nyininge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ndiyo hiyo inayotoka Cairo - Egypt mpaka Capetown Afrika ya Kusini (The Great North Road), ndiyo hii ninayoizungumzia. Kwa hiyo, utaona kwamba, barabara hii ina umuhimu wa kipekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara ni ya *The Great North Road*, katika nchi zote inapopita, imejengwa kwa kiwango cha lami, isipokuwa katika maeneo ambayo nimeyazungumzia. Maeneo niliyozungumzia katika barabara hii, ninaweza kuyaita *the*

*old out.* Ukiulizwa ni eneo gani katika barabara inayotoka Cairo mpaka Afrika Kusini, Capetown ambalo ni *the old out*, utasema ni hiyo ya kutoka Iringa, Dodoma, Kondoa mpaka Babati. Hata mtu akipewa mtihani, anaweza kufaulu kwa haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kuna mwenzetu amefiwa Arusha na alikuwa anakwenda kuwahi mazishi. Mimi nimemuuliza unapita njia gani ndugu yangu? Akaniambia anatoka hapa, Chalinze, Korogwe, Moshi mpaka afike Arusha. Je, mtu huyu atawahi mazishi ambayo ni leo? Haiwezekani kabisa! Wakati njia fupi ilikuwa ni kutoka hapa Dodoma, Kondoa, Babati anaingia Arusha na kwa kweli angeweza kuwahi mazishi. Lakini nampa pole ndugu yangu huyu hataweza kuwahi, barabara ina hali mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba barabara hii ni mbovu na ina hali mbaya, lakini ina madaraja mabovu kupita kiasi. Naomba nitoe mfano wa daraja moja ambalo liko katika kijiji cha Kolo. Daraja hili lilivunjika tangu mwaka 1997. Hii leo ni takriban miaka 32, daraja hili bado halijajengwa. Adha yake sasa, wakati wa masika mto unapokuwa umejaa, kutokana na daraja kuvunjika, wamejenga *drift*, kwa hiyo, watu wanapita kwenye *drift*. Sasa maji yakiwa yamejaa hayapiti magari wala waenda kwa miguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano wa Mheshimiwa Nsanzugwanko alipokuwa Naibu Waziri wa Habari, alitembelea Wilaya ya Kondoa lakini wakati akirudi, alikuta mto umejaa na alisubiri pale kwa zaidi ya saa nne mpaka maji yakapungua ndipo alipopita. Sasa hii ina maana kwamba hata wasafiri katika mabasi iwapo watakuta mto ule umejaa nao inabidi wasubiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine wasafiri hawa wanakuja Dodoma ili waweze kuunganisha na mabasi mengi kabisa hapa katikati ambayo hayana kingo. Barabara kuu, madaraja yake hayana kingo! Ni hatari kabisa hasa wakati wa usiku, magari mengi yameshapata ajali na watu wengi wameshapoteza maisha yao.

Vile vile wakati wa masika mvua ikinyesha na mito ikawa imejaa, maji yanakuwa *level* na madaraja kiasi kwamba Madereva hawawezi kuona mwisho wa daraja, kwa hiyo ajali pia zimekwishatoa nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vikwazo vikubwa vinavyokwamisha na kudumaza harakati za maendeleo, ni miundombinu duni na hususan barabara hii. Kwa hiyo, barabara hii inadumaza maendeleo ya wananchi wa Kondoa na maeneo yote ambayo barabara hiyo inapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano wa 12, Kikao cha 16 tarehe 2 Julai, 2008, nilichangia kuhusu tatizo hili la ubovu wa barabara hii pamoja na madaraja yake. Naomba ninukuu nilichosema, halafu ninukuu na majibu niliyoyapata.

*“Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya Wizara ya Mundombinu zimetengwa shilingi bilioni 12.1 kwa ajili ya barabara kutoka Dodoma mpaka Babati. Tunaomba sana fedha iliyotengwa ifanye kazi iliyokusudiwa na kazi hiyo ioneckane, isiwe tu ni pesa katika kitabu, lakini haionekani. Tunamba sana fedha hizo isiwe ni kiini macho”. Mwisho wa kunukuu na niliomba kufahamu ujenzi huo wa barabara utaanza lini.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikupe majibu ya Serikali, yalikuwa kama ifuatavyo na naomba ninukuu:-

*“Mheshimiwa Naibu Spika, majibu yetu ni kwamba, kipande cha Dodoma, Kondoa, Babati hadi Minjingu, usanifu wa kina ulishakamilika na ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka huu wa fedha, 2008/2009 kwa sababu zimetengwa shilingi bilioni 12.1 kwa ajili ya kuanza ujenzi”. Mwisho wa kunukuu na makofii yakapigwa sana. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tarehe 1 Julai, 2009, mwaka wa fedha 2008/2009 umekwisha. Kazi ya ujenzi wa barabara hii kutoka Dodoma mpaka Minjingu haijaanza wala hakuna dalili yoyote ya kuanza. Hakuna kabisa kilichofanyika, wakati tumeambiwa fedha zimetengwa, upembuzi yakinifu umeishakamilika na ujenzi kwa kiwango cha lami utaanza. Hamna kilichofanyika mpaka nukta hii mwaka mzima umepita, sasa hiki sio kiini macho? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waswahili wanasesma:-

*“Hata Bubu alisema kwa uchungu wa mwanae”.*

Sasa naona kuna watu wananihangaa kwamba leo imekuwaje Hajat anaongea hivyo? Lakini naongea kwa uchungu. Je, hizi shilingi bilioni 12.1 ziko wapi wakati katika kipindi cha mwaka fedha 2008/2009 hakuna kilichofanyika? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu Wizara imepanga shilingi bilioni 5.6 tu kwa ajili ya madaraja makubwa, imeandikwa hivyo. Sasa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami hamna tena, tunaambiwa ni ujenzi wa madaraja makubwa. Kiasi hiki kwanza ni kidogo sana, tulikuwa tunategemea kwamba, kwa kuwa mwaka jana ilitengwa shilingi bilioni 12.1, basi mwaka huu angalau inaweza kuwa pengine shilingi bilioni 20 lakini tumerudi tena chini shilingi bilioni 5.6. Je, kweli Serikali ina dhamira thabiti ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami? Inatia wasiwasi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ninayoizungumzia ipo katika Ilani ya Uchaguzi. Pia Mheshimiwa Rais wetu mpendwa alitoa ahadi Kondoa Mjini wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu mwaka 2005, aliwaambia wananchi wa Kondoa kwamba

barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami. Alitoa ahadi mwaka 2005, hii leo tunazungumza ni mwaka 2009!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba.....

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ni kengele ya pili!

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono nitakapopata majibu ambayo yataridhisha wananchi wa Kondoa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Zabein Mhita, Mbunge wa Jimbo la Uchaguzi Kondoa Kaskazini. Nafikiri, wana-Kondoa wamekusikia.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Nilisema baada tu ya Mheshimiwa Zabein Mhita, Mbunge wa Jimbo la Kondoa Kaskazini, sasa nitamwita Mheshimiwa Aziza Ally, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Tabora. (*Makofi*)

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuongea. Pia napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri na Naibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, awali ya yote, naomba nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kufanya ziara katika Mkoa wa Tabora. Nina imani, haya ambayo yameorodheshwa katika vitabu hivi, ni kutokana na matunda ya ziara yake ambayo ameifanya katika Mkoa wetu. Tunashukuru sana wananchi wa Tabora pamoja na Wabunge wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora tuna matatizo ya barabara. Kwa kuwa tuna matatizo ya barabara, kipindi chote kinapofika wakati wa bajeti, tunapigia kelele sana kuhusu suala la barabara. Lakini angalau muda huu kwa kweli tunaipongeza Serikali kuweza kuona angalau kidogo kwa kuanzia si kibaya lakini pamoja na hiyo kidogo ambayo tumeanzia, basi utekelezaji wa haraka uweze kuwepo ili mafanikio na matunda yaweze kuonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mtovu wa fadhila sana, nisipochukua nafasi hii, kumpongeza Mama Anna Abdallah. Mheshimiwa Anna Abdallah, alikuwa Waziri katika Wizara hii. Muda aliokuwepo hapo katika Wizara hii, alifanya kitu ambacho Mkoa wetu wa Tabora tulikuwa muda mwingi hatujakifahamu. Lakini baada ya kujua kwa nini Tabora hatupati barabara za kuweza kuwa na maendeleo, nikagundua kuwa Mama Anna Abdallah alikuwa na mapenzi sana na watu wa kuanzia Dodoma, Tabora, Kigoma. Lazima niliseme kwa sababu leo tunapiga kelele “Sungura Mdogo, mambo yako katika upembusi sijui yakinifu, mipango iko mbioni, msibirini tutalizingatia, tunalionia. Lugha nyingi ambazo wala kusingkuwa na maneno yote hayo ya misamiati ambayo kila siku inaundwa mipyka kama tungefuata maelekezo yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mama Anna Abdallah, alipata watu ambao wanaweza wakajenga barabara, ni Watanzania kwa kuweza kutumia pesa zao kama watapata benki, kama watapata wapi, ili mradi wametengeneza barabara zile kutoka Dodoma – Tabora – Kigoma ambapo kufika Kigoma pale wale watu wangeweza kusafirisha mizigo yao, Tanzania isingetumia hata senti tano, ni kitu ambacho sisi tungekuwa na faida nacho kubwa sana. Yule mtu ambaye angetengeneza baraba ile, yeye angepata pesa zake kwa ku-charge ile mizigo ambayo inatoka Dar es Salaam – Tabora – Kigoma, kwa hiyo, wangemlipa yule mtu kupitia fedha hizo. Wangekubaliana ni mikataba ya miaka mingapi, kama ni miaka kumi akimaliza, Tanzania inabaki na barabara yake na kodi ingeweza kuchukua. Kwa hiyo, siyo dhana tunazoendelea nazo kwamba barabara lazima ijengwe na pesa za wafadhili, barabara lazima ijengwe na pesa za wananchi au pesa za ndani ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sina budi kumshukuru mama huyu, kwa kweli Mungu atakujalia kwa imani na mapenzi ambayo unayo katika nchi yetu. Kibaya, alipotoka tu, sijui kuna mdudu gani ambaye aliingia, mpaka leo ndio tunapiga kelele ya hizi barabara. Lakini, laiti angekuwa bado yupo, nina imani saa hizi wala hizi kelele tusingekuwa nazo na misamiati yote hii isingekuwepo, ndio maana unakuta sasa hivi Mkoa wetu wa Tabora unazidi kwenda nyuma kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na Chuo cha Nyuki, yaani kwa sababu ambazo hazina maana kiliondoshwa kikapelekwa Arusha. Lakini bado isitoshe, sasa hivi kimerudishwa kiujanja ujanja, mguu ndani, mguu nje. Ushahidi ninao kwa sababu ukiangalia kwenye kile kitabu cha bajeti, hela zilizotengwa ni ndogo sana, kwa hiyo imo haimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tena, kwenye Kamati yetu ya Ardhi, wanataka watoe Chuo cha Ardhi na chenyewe wakipeleke Morogoro. Tatizo ni barabara hizo hizo na miundombinu. Lakini bado isitoshe nina imani kwa sababu mambo yote yanafanyika, mwaka 2000 mpaka 2005, Nyuki inaondoka, mwaka 2005 – 2010 Ardhi inaondoka, je, mwaka 2010 – 2015, si watatoa na kile cha Uhazili, mwisho watatoa na Mkao utakuwa Kijiji, sasa tutakuwa hatuna Mkao. Inasikitisha sana! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania lazima tubadilike tujue mwekezaji sio Mzungu, Mhindi, Mchina, hata Watanzania wenyewe wanaweza wakawa ni wawekezaji wazuri sana kwa sababu kwenye nchi yao wanakuwa na uchungu. Kwa hiyo, wazo hili, laiti kama lingeweza kutekelezwa katika nchi yetu, sisi tusingekuwa na kelele na barabara hizi. Tanzania ingekuwa imepata mapato makubwa sana kupitia barabara ile. Huduma nyingi zingepatikana hata Peramiho kule huduma za afya zingepatikana vizuri, vikundi mbalimbali vyta SACCOS vingeweza kupata mikopo kwa sababu nchi yetu ingekuwa na pesa nyingi. Inasikitisha, lazima tubadilike, tuwe tunaangalia pesa za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini je, wawekezaji wetu wa ndani ya nchi na wa nje, wanao uwezo wa kututengenezea barabara? Sasa hivi tuna mpango wa kusema itakapofika mwaka 2012, barabara zote katika nchi hii ziwe zimeunganishwa, kulingana

na hivi visungura na vikeki hivi, kweli tunaweza tukakamilisha? Kama hatutokamilisha, tuna mikakati gani mingine ya kuweza kuangalia barabara hizi ziweze kuendelea? Inasikitisha na inaumiza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda haraka haraka, napenda kuongelea usafiri wa reli. Usafiri wa reli hamna kitu. Kitu ambacho ni cha kusikitisha zaidi, ukiangalia kwenye barabara ni matatizo, ukiangalia reli ndio tatizo kabisa ambalo liko mochuari. Mimi nashindwa hata kuelewa maana tukisema uwanja wa ndege, ni wachache sana ambao wanawenza wakatumia uwanja wa ndege, lakini na kwenyewe ndio hamna kitu kabisa. Upembuzi yakinifu kwenye uwanja ndege tayari lakini huo utendaji unaanza lini? Bora angalau mtupe matumaini maana hata mgonjwa ukimpa ushauri nasaha, unampa matumaini hata kidonge cha *Panadol* kula, anakuwa na matumaini kidogo. Upembuzi yakinifu tayari lakini kimya tu. Tunaomba Mheshimiwa Waziri atuambie, utaratibu wa ujenzi wa kiwanja cha ndege utaanza lini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye reli. Wabunge wengi wameliongelea suala hili na Kamati bahati nzuri na wenyewe wameliongelea kwa ufasha zaidi. Lakini mwaka jana tuliliongelea na tulismama katika Bunge hili hili lakini mambo yalikwenda ndio hivyo hivyo, tukimaliza kusema hapa yanakwisha, wanaopata shida, ni wale wananchi ambao wanasaferi na reli, wakubwa wengi watasaferi na magari na ndege lakini wale wanaosafiri na reli wanapata shida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiingalia ile treni, wasafiri wanaoingia mle, nadhani siku moja labda sisi Wabunge tufanye ziara pale stesheni wakati treni inaondoka, tukae pale, tuangalie watu wanavyopanda tuone inakuwaje.

### **WABUNGE FULANI:** Tupande kabisa!

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Wako Wabunge wengine wanasema inabidi tupande ile treni mpaka Kigoma. Sasa mimi nasema kama wataamua hivyo, itakuwa ni vizuri zaidi ili kusudi muweze kuona ni vitu gani ambavyo vinafanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoongea, ni kutetea watu na kuangalia wananchi wanapata shida kiasi gani. Shida wanazopata, ni kitu ambacho kinasikitisha, wanalipa nauli yao wakiwa kwenye nchi yao, lakini wanasaferi kwa shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu basi turudi nyuma tujifikirie na sisi wenyewe tulikotoka. Ukiwaangalia hawa watalaam wengi, wengi wamesoma *Tabora Boys*, *Tabora Girls*, Mirambo, Kazima basi hamkumbuki hata mlikotoka! Hebu jirudisheni hata mawazo kidogo mkumbuke mlikotoka, maana ukikumbuka ulikotoka, nafasi inaweza ikakusuta. Lakini basi mtu unasahau moja kwa moja. Hata historia watu wamesahau kwamba hata kura tatu ilianzia Tabora. Wengine inawezekana labda walikuwa Ulaya wakati ule wanasona, walipelekwa na Serikali au vipi, maana unasahau hata historia ya nchi hii ilivyokuwa. Lakini muelewe kwamba katika hiyo historia ya nchi hii, Tabora na yenye ina historia kubwa sana ya nchi hii ambayo inahitaji kuzingatiwa na kuenziwa. Labda nchi za Ulaya zingkuwa zinawapa msukumo, mngekuwa mnazingatia hili, lakini

kwa kuwa bado hawajaanza kuwapa msukumo, pengine hata ile kura tatu mnaona bado haijawa makini sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme kwamba, hii Tabora kwa kweli mnaionea. Hili nisipolisema leo, naweza huko mbele nikakosa nafasi ya kuongea. Tumepata ufadhilli kutoka Marekani katika hospitali yetu ya Kitete wa dola milioni 50 za vifaa vya hospitali ili viweze kusaidia katika kutoa huduma. Ndio hayo hayo ambayo ninayoyasema, eti toka Februari mpaka sasa, Wizara ya Afya na Hazina kuidhuinisha tu kuwa vile vitu viweze kusamehewa kodi, mpaka leo, Mheshimiwa Mwenyekiti, hawajaamua kwamba visamehewe au lah. Je, ni kwa sababu vinakwenda Tabora? Hivi Tabora kuna tatizo gani jamani?

### **MBUNGE FULANI:** Wanyamwezi!

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Vingekuwa vinaenda kwingine, labda vingeweza kusamehewa kodi. Vifaa mnapewa bure, vinaenda katika hospitali yenu, Tanzania hamtumii hata senti tano yenu, labda ni wale waganga amba wanawatibu watu, bado hata hilo na lenyewe pia linakuwa ni gumu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ikae chini ifikirie, Tabora ina tatizo gani? Hebu siku moja mtuambie, Tabora mna tatizo moja, mbili, tatu ili na sisi tujirekebishe, kama kuja kutubu, tutakuja kutubu kwenu kusudi Tabora yetu na yenye we iwemo katika Mikoa ile ya Tanzania. Inasikitisha na inauma sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana, msamaha wa kodi ni kitu kidogo sana kwa sababu vile vifaa vinatoka na vimeshukia Mombasa, ushahidi tunao na *document* tunayo. Napenda kukupongeza umenifundisha kitu cha kuandaa *document* kwa sababu ukiandaa hapa na ukiziwasilisha, kila kitu kinajulikana hiki ni sahihi na cha wazi. Kwa hiyo, hata hizo Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizihitaji naweza nikakukabidhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba kuidhinishiwa ule msamaha. Tangu Februari mpaka sasa kitu cha bure, una tatizo gani! Hamtumii hata senti tano yenu, vitu wametoka Marekani wanasema kama hamhitaji, tupeleke nchi nyininge. Kwa hiyo, pamoa na kuwa mtasema hazitoenda Tabora, lakini hazitaenda katika Mikoa mingine. Vikishindikana Tabora, vitaenda nchi nyininge, hata mimi nitakubali wapeleke nchi nyininge kwa sababu na kule Tabora nako kuna watu wana matatizo na wanahitaji huduma hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapomaliza, atueleze uwanja wa ndege, atueleze kuhusu hizi barabara utekelezaji wake utaanza muda gani na wa haraka zaidi. Naunga mkono hoja! (*Makofi*)

**MWENYEKITU:** Nakushukuru sana sana Mheshimiwa Aziza Ally, Mbunge wa Viti Maalum. Waheshimiwa Wabunge, Aziza, hiki ni kipindi chake cha pili ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Aziza, kwa kuweka rekodi na

kumbukumbu ziwe sahihi, itabidi vielelezo hivyo utaviwasilisha kama ulivyosema, ni muhimu sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Benson Mpesa, Baba Askofu Mtarajiwa, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini. Atafuataiwa na Mheshimiwa Ania Chaurembo.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu, hoja ya Waziri wa Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda niungane na Wabunge wenzangu kusema kwamba ninaunga mkono hoja hii kwa sababu, kwanza ni hoja inayoletwa na Serikali yangu, lakini la pili, nimeona mipango iliyomo humu ndani inakusudia kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kiasi kikubwa na mimi kama Mbunge niliyepitia dirisha la Chama cha Mapinduzi, lazima niiunge mkono. Lakini kama nitakosoa, basi ni hapa na pale katika kurekebishana kitu ambacho ni cha kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu kwa kuhimili hili joto la michango ya Wabunge na kwa ujumla kwa kazi nzuri wanayoifanya. Lakini naomba nitumie nafasi hii pia kumpongeza Meneja wangu wa *TANROADS* – Mbeya, kwa ushirikiano mkubwa anaonipa ninapokuwa nafuutilia hoja mbalimbali zinazohusiana na barabara au miundombinu kwa ujumla, ninapata msaada wa karibu sana, naye katika nafasi hii, nampongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kwanza, nikiri na kuishukuru Serikali kwamba imetenga shilingi bilioni 12.8 kwa ajili ya barabara ya kutoka Mbeya kupitia Isanga, Iganzo, Mwansengwa mpaka Maongolosi, barabara ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, lingine, naomba niipongeze Serikali kwa kuendelea kutenga pesa kwa ajili ya uwanja wa ndege wa Songwe. Tumepewa pesa ya kutosha karibu bilioni 32.6 kwa ajili uwanja huu. Yote haya, ndio maana nilitanguliza pongezi kwa Serikali kwa sababu dhamira inajionyesha. Ila sasa, kilichobaki, lazima tupambane na vikwamishi vinavyosababisha hii miradi isitekelezeke kwa wakati tunaoutaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na hii barabara ya kuanzia Mbeya kwenda Makongolosi mpaka Itigi. Nataka niseme hivi, kwamba ndugu zangu, tunayo changamoto kwamba barabara hii sio kwa ajili ya watu wa Mbeya, barabara hii tulitegemea itasaidia katika mipango ya kuifungua nchi hii. Tunazalisha viazi, vinaoza, tungependa tuwauzie wenzetu wa Tabora, tupeleke viazi Singida, tupeleke viazi Mwanza, Shinyanga na kadhalika na ndiyo madhumuni makubwa na tulishakubaliana na sisi kama Watanzania lazima tufike mahali kusema, barabara nyingine hizi, *network* hizi zilizoanzishwa na ukoloni, tunachotakiwa sisi ni kuziweka lami. Katika mipango

tuliyokubaliana, tulisema tuenze na barabara ambazo zinafungua Mikoa. Hapa lazima utaifa tuutangulize mbele kwanza, uzalendo tuweke mbele kwanza na kuifungua Mbeya na Tabora mpaka Mwanza, ni hii barabara ya Mbeya – Makongolosi – Itigi au kupitia kwa ndugu yangu Mkumba pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa nini nimeamua niiseme barabara hii? Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, alitenga muda wake kuja kuweka jiwe la msingi la barabara ile. Kule kutenga muda tu ni jambo zito sana, ni dhamira inayoonyesha kabisa anakusudia kuyatekeleza haya ambayo yako kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mheshimiwa Waziri Kawambwa tulikuwa wote siku ile, kitendo kilichofanyika ambacho ndicho kinachonipa uchungu mimi, ni ile hali ya siku ile, ni kama tunataka kumdhaliilisha Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ile Rais alifanya kitendo hadharani kwa kumwita Mkandarasi – Kundan Singh kwamba lete kidole chako, tunafunga amini leo, unahakikisha unaimaliza barabara hii kwa wakati wake. Meya wa Jiji la Mbeya ndiye aliyetenganisha vile vidole. Hii ni *commitment* ya hali ya juu ya Rais, tunailindaje hiyo? Wananchi walioona tukio lile Rais akiweka amini na yule Mkandarasi, tunalilinda vipi tukio lile? Ni jambo zito sana hili! Sio suala la lele mama vinginevyo tutamuweka Rais katika hali ya kusema atawenza akachezewachezewa na watu namna ile na watu wameniambia tuulizie inakuwaje? Ile ilikuwa ni ahadi nzito kuliko hata pesa inayotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua matatizo yaliyojitekeza ni matatizo kwa upande wa Mkandarasi, kwa nini nalizungumza hili? Huyu Mkandarasi ndio tumempa tena kujenga baadhi ya kazi kule kiwanja cha ndege cha Songwe, hivi kama huyu alishindwa kuwa na wataalamu wanaotakiwa katika ujenzi wa kipande cha barabara kilometra 37 kutoka hapa Mbeya mjini kwenda Luhanjilo kwa kuanzia, leo anaiacha hii barabara anakwenda kwenye uwanja wa ndege wa Songwe .Tutaamini vipi kwamba uwanja wa ndege wa Songwe utakwenda kama ilivyopangwa wakati Mkandarasi ni huyu huyu? Ameongeza wataalamu lini? Pamoja na kutudanganya kwamba atajenga zahanati kila mahali itakapopita barabara lakini tunaisubiri ile ahadi kwa sababu aliitoa mbele ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu yangu ni huyu Mkandarasi ambaye ameonekana kwamba asimamishe kazi kwa sababu hana wataalamu wanaotakiwa lakini tumempa *contract* katika kiwanja cha ndege cha Songwe! Ninaomba Serikali inithibitishie kupitia kwa Waziri wetu, maana kiwanja hiki ni kiwanja cha Kimataifa na kazi ya kujenga tunakusudia *runway* isiyopungua kilometra nne, ni kazi ile ile sawasawa na barabara ambayo ilikuwa inajengwa kwenda Makongorosi, je, ameshaongeza wataalamu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hilo, tumepata usumbufu mkubwa sana kwa sababu kazi ya kuhamisha miundombinu katika barabara hii ya maji, umeme ilishaanza kufanyika. Baada ya huyu Mkandarasi kuondoka sasa imekuwa ni adha waliokatiwa maji, umeme imebaki kama ilivyo. Naomba Serikali ifanye *intervention* ya haraka sana katika kuinusuru barabara hii. Tunaihitaji barabara hii siyo kwa manufaa ya wananchi wa

Mbeya bali kwa ajili ya Watanzania wote na kwa ajili ya kuifungua Mbeya na ndugu zao wa Tabora, Mwanza, Shinyanga na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linalokwenda sambamba na barabara hii, ndugu zangu wa Isanga, Kata ambayo ni kongwe kabisa katika Jiji la Mbeya, Iganzo ambayo msemaji huyu ndiko alikozaliwa, Mwasenkw, wananchi walipaswa kulipwa fidia kwa ajili ya barabara hii. Ninaomba kuishukuru sana Serikali kwamba kwa kiasi kikubwa imejitahidi sana kulipa fidia kwa baadhi ya wananchi ambao walistahili kulipwa lakini lipo kundi kubwa sana la wajane, wagane, yatima ambao nyumba zao zimebolewa au zinatakiwa kuondolewa kwa ajili ya barabara hii. Naomba tena urejee upya ile fidia, kuna watu ambao kwa kweli hata ukiwaangalia, inasikitisha sana. Naomba suala hili ulitilie maanani ili tuangalie wale ambao bado hawajalipwa fidia kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutoka Mbeya kwenda Makongorosi, wafikiriwe haraka sana maana hali zao za maisha zimekuwa ngumu mno. Mheshimiwa Kawambwa, anajua unapofika mahali ndio eneo unalokaa wewe, unaweza kukadiria ni usumbufu gani unaoupata na wengine unawajua umekua nao, ni wazazi wako, wamekulea, inatia uchungu kidogo, naomba Serikali suala hili ilifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niiulize Serikali, uwanja huu wa ndege wa Songwe Julai mwaka jana 2008 ulikuwa ukamilike ili usaide kuifungua Tanzania ya upande wa Kusini Magharibi ili tuweze kufanya biashara na ulimwengu wa biashara. Tufanye biashara na *DRC*, Zambia, South Africa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri, uwanja huu ndio katikati ya kitovu cha Afrika kutoka Afrika ya Kusini kwenda Cairo. Mbeya kama unavyoju tulivyo na hewa nzuri, ninaamini kukamilika kwa uwanja huu, kutashamirisha biashara ya maua na vitu vingine. Kwa hiyo, ninapenda kujua baada ya kuchelewa kwa mwaka mzima, *time frame* inasemaje, ni lini uwanja huu utakamilika, ili na sisi hizi hadithi za kushangaa ndege zinazokwenda South Africa tuache zitue, kwa ajili ya kutupatia huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nizungumzie juu ya barabara ya zamani inatoka Mlima Nyoka na kwenda Uyole Kati. Barabara hii katika vikao vingi vya *TANROADS* Mkoa wa Mbeya, tulikubaliana kwamba itengenezwe na kuimarishwa. Lakini bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu amekubali kipande cha kutoka Uyole Kati kwenda Chuo cha Maendeleo cha Uyole kwenda Taasisi ya Kilimo Uyole na Chuo cha Kilimo Uyole kuingia kwenye daraja la Tazara amekubalia kwamba barabara hii itajengwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa Serikali kupitia *TANROADS*, kipande hicho kiendelezwe mpaka Ilomba, kupitia Pambogo, kupitia Inyala, kule Iyunga na itokeze kwenye lango kuu la Chuo cha MIST pale Mbeya. Bahati nzuri, upande wa Kusini wa barabara ile ya MIST, Kuyunga, MIST na barabara kuu tumepata fedha za wafadhili, tutajenga kwa kiwango cha lami. Lakini kwa kipande hiki cha barabara ya zamani, naomba sana kama tulivyokubaliana kwenye vikao, itekelezwe na kupewa uzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze jambo lingine nalo nila ndugu zangu wa TAZARA. Wafanyakazi waliokuwa wafanyakazi wa TAZARA na wafanyakazi ambao bado wanaendelea kufanya kazi TAZARA, bahati nzuri Mbeya ilikuwa ni kituo kikubwa sana, wengi walio- *retire* wamebaki katika mazingira yale ya Mbeya na wengine bado wanaendelea kufanya kazi. Hali ya wafanyakazi hawa, ninaomba nimpongeze Mwenyekiti wangu wa Miundombinu na Kamati nzima ya Miundombinu kwamba mmeliona hili. Sisi ndugu zenu ambao tunaishi kila siku na watu hawa kwa kweli imekuwa ni taabu sana, wengi waliostaafu wameamua kuza nyumba zao, wameamua kuza mali walizonazo kwa ajili ya kusubiri *pension* ambayo mpaka leo hawajapewa, wamekosa nini Watanzania hawa maskini ambao wameitumikia nchi kwa uzalendo mkubwa sana? Wenzetu upande wa pili wa Zambia, wamejitalidi kuboresha hali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja hii.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mpesa kwa machango wako mahiri kabisa.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nimwite Mheshimiwa Ania Chaurembo na ninadhani atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho kama sitakubaliana na wanaofuata kutumia dakika chache sana zitakazosalia.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie katika hoja hii iliyopo mbele yetu ya Waziri ya Miundombinu. Katika hotuba yake leo hii Waziri wa Miundombinu amezungumzia suala zima la ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Nyerere, Dar es Salaam. Suala hili nilitegemea katika kuzungumza kwake atalizungumzia pamoja na wananchi wa Kipawa, Kipunguni na Kigilagila waliohusika na upanuzi wa uwanja huu wa ndege.

Mhesmiwa Mwenyekiti, ninapenda baadaye Waziri kabla sijaanza kuzungumza, atuelezee, je, utakuwa ni ukarabati tu au ule mpango wa kuwahamisha wananchi wa Kipawa bado uko palepale? Kwa sababu gani nasema hivi? Ni kwa sababu wananchi wale wa Kipawa wako pale zaidi ya miaka 13 sasa, wamezuiliwa kufanya kitu chochote na nimekuwa nikizungumza mara kwa mara katika Bunge lako hili, hawaruhuswi kukarabati, kutia rangi, kutengeneza choo na matokeo yake nyumba chungu nzima katika eneo lile tayari zimeshaanguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka 13 ni miaka mingi katika uhai wa binadamu na wananchi wale imefikia hadi shule ya Kipawa ambayo ilikuwa imeezuliwa imefungwa na Serikali toka miaka hiyo, ndio baadhi ya wananchi ambao hawana pa kuishi baada ya nyumba kuanguka kabisa wanaishi katika eneo lile la shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika shule hiyo ya Kipawa utakuta wananchi wanakaa pale kaya tatu, nne katika darasa nmoja na kati ya kaya na kaya yamefungwa mashuka, kanga au vitenge tu, hii si haki ya binadamu, huu ni uonevu mkubwa wanaofanyiwa wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga mipango yake ya maendeleo kama bado kuna matatizo katika kulitekeleza jambo lile basi watoe maamuzi ya ziada, wananchi wale baadhi yao wamepewa hadi viwanja, wengine wamelipia viwanja vile lakini *offer* hawajapewa na wengine hata viwanja hawajaonyeshwa na wengine hawajapewa. Hili ni tatizo tena tatizo kubwa na eneo ambalo walikuwa wamepewa la Majohe na Buyuni watu wenye mashamba yale wakienda wanawashikia mapanga wanasesma Serikali haijatulipa fidia. Sasa inaonekana Serikali inapanga mipango kwa kweli bila kuweka taratibu zake sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi juzi katika magazeti imeonyeshwa kwamba wametenga shilingi bilioni 30 kwa ajili ya kuwapa fidia wananchi hawa lakini wananchi hawa wamenituma nije kuwasemea hapa Bungeni wanasesma hizi shilingi bilioni 30 ndio fidia ya maeneo yote haya ya Kipawa, Kigilagila na Kipunguni? Tathimini ya mwaka 2002 ilikuwa ni shilingi bilioni 22 na zaidi mwaka 2009 wanadai wamefanya tathimini nyingine imepatikana shilingi bilioni 60 na zaidi kidogo, sasa wanataka kujua kwa sababu hawana taarifa ya barua au maelezo yoyote, wao wapo wapo tu, wanangoja rehema ya Mungu na Serikali kuamua. Pamoja na uvumilivu wao wote, hizi shilingi bilioni 30, wananchi hawa miaka 13 wakati walipoambiwa wasifanye jambo lolote ilikuwa mfuko wa *cement* shilingi 3,500 sasa hivi mfuko wa *cement* ni shilingi 15,000, vifaa vya ujenzi vimepanda kupita kiasi, je, fedha hizi zitakidhi mahitaji kweli ya wananchi hawa kujenga maeneo ya kuishi na familia zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza Serikali ina kigugumizi gani? Kama wameweza kukarabati uwanja wa Mwalimu Nyerere kwa nini wameshindwa kuwapa hawa wananchi haki zao? Wananchi hawa wameyumba, mpaka sasa hivi hawajui chochote, wamechanganyikiwa kabisa. Nimekutana na Kamati yao kabisa, wananchi wanalia kwa Serikali, wamenipeleka mpaka chumbani wanasesma angalia tunavyoishi, sasa hivi tunashindwa hata kuzaa. (*Vicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli wameniambia hivyo, hayo siyo maneno yangu maana vyumba vinatenganishwa na shuka, familia moja ina watoto sita, saba, mnajua sisi Waswahili tunaza sana, hakuna mtu pale mwenye watoto wawili, sikumwona, hapo ndio wanalala shulenii, nyumba zao mapango kabisa, nyumba zote zimedondoka. Kwa nini lakini hawatendewi haki wananchi hawa? Mheshimiwa Waziri hebu naomba uwaeleze hawa wanachi wa Kipawa, Kipunguni na Kigilagila waelewe hatima yao na hii shilingi bilioni 30 ambayo imetangazwa na Serikali ni ya nini na je, ni kwa ajili ya maeneo yote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri mwenyewe tulikaa kuzungumza, waliniambia karibu watu 5,000 na zaidi wanahuksika na suala hili. Wananchi hawa wamesema uvumilivu wao umetosha, miaka 13 wamevulia, kauli yangu hii naisema leo wanategemea wapate jibu ili wajue hatma yao na Serikali yao wanaiheshimu, hawataweza kuendelea tena na uvumilivu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno haya, sasa hivi napenda kuzungumzia mambo ya ATCL. ATCL ni Shirika la Ndege la Tanzania, leo naambaa hapo

hapo kwanza kwa sababu kuna uozo mwingi sana. Shirika hili pamoja na jitihada kubwa ya Serikali kulibeba ili liwe na uhai, ni kweli Shirika hili limebeba Nembo ya Taifa letu lakini tuliambiwa hapa Bungeni kwamba kuna ndege za *Airbus* zimenunuliwa lakini ndege hizo Marubani wote wa Tanzania hawawezi kuziendesha, mpaka wapate mafunzo kidogo ili waje wazishughulikie na kuna wakati hiyo *Airbus* niliikuta *Airport* imefunikwa kitambaa kikubwa, sasa tunataka kujua kama hii *Airbus* inafanya kazi au imekwenda kwenye matengenezo wakati hata hajatumika? Je, wale Marubani walioleta ambao walikuwa wanakaa hoteli kubwa bado wanaendelea kulipiwa na wapo nchini? Marubani wa Tanzania ambao walitakiwa kwenda kusoma, je, kwa muda wote huu zaidi ya miaka miwili, wameshapelekwa kusoma?

Mheshimiwa Spika, lakini kama hiyo haitoshi hapo hapo kuna Shirika la *DAHACO*, *DAHACO* ni Shirika ambalo lina miaka zaidi ya 21 baadaye ikaingia Swissport, shirika hili kuna matatizo pale mengi sana. Baada ya kuingia Swissport, wale wafanyakazi ambao walikuwa wanafanya kazi pale zaidi ya miaka 25, walikuwa wapewe haki zao, hawajapewa. Hivi sasa watu wanaojiriwa pale wanaajiriwa kwa mkataba wa miaka miwili. Sasa wale wafanyakazi wanaauliza kuna kigugumizi gani mbona wao hawapewi haki zao kwanza? Ni nani atakuja kuwapa haki zao wakati wawekezaji wanabadilishana. Hili ni tatizo na ninaomba Kamati ya Miundombinu ambayo ndiyo inayofuutilia masuala mbalimbali, ipitie Swissport na ikakutane na baadhi ya wafanyakazi isikilize kilio chao. Mwenyekiti wa Miundombinu, nafikiri amenisikia vizuri sana. Hii ni kero kubwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama hiyo haitoshi, nilikuwa nataka kumshukuru Mheshimiwa Waziri, hapa alizungumzia habari ya barabara katika jiji letu la Dar es Salaam, mimi kwa kweli ninamshukuru na ninampongeza. Mheshimiwa Rais alizungumzia jiji la Dar es Salaam, Waziri Mkuu alizungumzia jiji la Dar es Salaam kwa sababu jiji hili ndio kioo cha nchi yetu ya Tanzania. Nathubutu kusema ndio Mji Mkuu wa Nchi hii na Watanzania wote wanakimbilia Dar es Salaam. Mmeshuhudia jinsi gani jiji la Dar es Salaam lilivyo kwa linamsongamano na tatizo kubwa la usafiri ni barabara. Kwa hiyo, kwa hili napongeza sana na hasa barabara ile ambayo tayari imeanza ya kutoka Twiga, Jangwani hadi kufikia Ubungo Maziwa, naipongeza Wizara ya Miundombinu kwa sababu tayari imeanza kushughulikia barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nashukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofifi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuwasiliana na mchangaji anayefuata na anayemfuata, wamenithibitishia kabisa dakika zilizobakia hazitoweza kuwatoshla kuwalilisha maeneo wanayotoka kwa ukamilifu mkubwa. Ninaomba nirudie, baada ya kuwasiliana na wenye haki ya kuchangia kwa dakika hizi zilizobakia, kila mmoja amenithibitishia kwamba hazitamtosha.

Waheshimiwa Wabunge, kama hivyo ndivyo itanipasa tu nisitishe shughuli hizi lakini tutakaporudi mchana msemaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Paul Lwanji, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Anthony Diallo, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Dr.

Samson Mpanda, hao ndio watakuwa wachangiaji wetu wa mwanzo katika kipindi cha jioni.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwashukuru sana kwa ushirikiano mlionipa asubuhi hii na nadhani tumekwenda vizuri na sina tangazo lingine lolote hapa mezani, basi kwa hali hiyo nitasitisha shughuli hizi za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(*Saa 6 .48 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, habari za jioni.

**WABUNGE FULANI:** Nzuri.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na shughuli yetu na kabla hatujaendelea, sasa nimwombe Katibu, atuongoze kwa shughuli ya jioni.

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Hoja ya Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu**

(*Majadiliano yanaendelea*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nilisema mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Paul Lwanji, simuoni, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa mchana huu, kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu. Nami nieleze yangu machache niliyonayo haswa yale yanayohusu Jimbo langu la Kilwa Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, Kilwa Kaskazini, sasa hivi na sisi tumo katika mambo ya miundombinu, hatukurudi nyuma japokuwa kuna mambo kadhaa ambayo nitayasema sasa hivi kama yanetiliwa mkazo zaidi basi mwaka 2010 sitakuwa na wasiwasi wa kuwepo tena kwenye Mjengo huu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, watu wa kwetu kule Kilwa wanasema kwamba asiyeshukuru kile kidogo apatacho basi hata ukimpa kikubwa hatashukuru tena huyo na atakuwa si mtu. Ila sisi tunashukuru sana kwamba barabara zetu, kama hazipo kwenye matayarisho, zinajengwa au zipo kwenye mkakati wa hali ya juu sana. Tumetofautiana sana na wasemaji wengi waliozungumza mwanzoni kulalamika

kuhusu barabara zao lakini kusema kweli barabara za kwetu, *Alhamdulillah*, katika miaka mitatu hii niliyokuwepo mimi katika nafasi hii, nashukuru Mungu Mheshimiwa Waziri ametuona na si Waziri tu ni pamoja na Mawaziri wengine, wamejitalidi kadri ya uwezo wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, barabara ya kutoka Kipatimo mpaka Chumo, kwa kweli ilikuwa ni ndoto ya mbali kabisa, watu walikuwa hawafikirii hata siku moja kwamba itajengwa lakini sasa inatia moyo. Daraja la Lyomanga linatia moyo ambapo ndiyo ulikuwa mpaka mkubwa wa kuigawa Kilwa Kaskazini upande wa Pwani na upande wa Bara kiasi ambacho hata Waheshimiwa wingine wakubwa wa Serikali walikuwa wanashindwa kuvuka kwenda upande wa pili. Kwa mfano, Mheshimiwa Mwanri na wengine wakifika tu walikuwa wanapita barabara ya pwani pwani kule, ya Kilwa Kaskazini, walikuwa wanashindwa kupita kwa sababu ya ubovu wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, hiyo barabara ya Kipatimo mpaka Chumo, sasa hivi imefunguliwa na ndugu zangu Waheshimiwa karibuni kwetu muone machungwa na kuna mapango mazuri sana ambayo wengine wanasifia mapango ya Amboni, mapango ya Amboni kwetu sisi kule ni kama sehemu ya kuchezea watoto. Kwetu sisi kuna mapango mazuri, makubwa na yale yaliyotumika kwenye Vita Kuu ya Majimaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa Vita ya Majimaji ilipoanza kwa kufyeka zile pamba, usiku ule wanawake wote na watoto wakaenda wakajificha kwenye yale mapango, wale Wajerumani walipoanza kupigana wakashangaa, wakauliza aah, mbona wanawake ambao tungewatesa hawapo? Kumbe wote walijificha kwenye mapango na Wajerumani hawakujua. Mapango yale ni kivutio kikubwa sana, sasa njooni muone. Mheshimiwa Waziri mmoja alikuja pale akaweka na jiwe lake la msingi, sitaki kumtaja jina lakini ni mama, aliweka jiwe la msingi pale safi kweli kweli mambo sasa hivi yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mpango wetu wa sasa hivi tunataka kusheherekea kumbukumbu ya Vita Kuu ya Majimaji pale ilipoanzia. Mwaka juzi nilipokuwa hospitali, nilijibiwa na Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana, akasema kwamba mwaka ujao kutakuwa na sherehe Kilwa Kipatimo na Ndete lakini toka mwaka ule nilipokuwa hospitali mpaka miaka mitatu iliyofuata, hakuna sherehe yoyote iliyofanyika kule Kipatimo na Ndete yote ilikuwa ni kwa sababu ya barabara. Sasa hivi barabara ni nzuri na wote karibuni isipokuwa tu mngetuongezea pesa kidogo tu kutoka Kipatimo mpaka pale kwenye ule Mnara wenyewe tu na barabara ile ya kuingia kwenye mapango yale ingekuwa barabara kabisa, watu wote tungeshukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha pili, ni barabara kutoka Nangurukuru kwenda Liwale. Asilimia 75 ya barabara hii imepita kwenye Jimbo langu, sasa wananchi wameupokea ule mradi kwa mikono miwili na kazi kusema kweli inafanyika vizuri lakini ajabu ni kwamba pesa wale Wakandarasi mpaka leo hawajapewa. Sasa license ya kuthibitisha kwamba kazi wameimaliza inakuwa ngumu kweli kuwapa wale watu kwa sababu wanaidai Serikali fedha nyingi sana. Pale kutoka Mlima Tembo mpaka Njinjo

Mjini, barabara haiendi vizuri, sijui wanakwamishwa kwa sababu ya kutokupewa pesa zao au vipi? Kwa hiyo, naomba Serikali muitazame sana barabara hii ili iweze kupitika muda wote na mambo yaende sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, barabara kutoka Ndundu mpaka Somanga, nimefurahi nimesoma mchana huu kwamba barabara hiyo imetengewa fungu zuri kabisa na huenda ikafanikiwa mwaka huu au mwanzoni mwa mwaka ujao. Lakini mambo ni yaleyale kwamba upangaji wa mradi hauko sawasawa. Watu wa umeme wamepitisha milingoti na mabomba yao katikati ya barabara. Sasa barabara inakuwa inapita juu ya mabomba na minara hiyo mimi naona italeta ukorofi baadaye maana inaonekana kama watu hawa hawakuwasiliana vizuri. Lakini ni matumaini yangu kwamba hizo nguzo kuzipitisha pembedi kidogo itakuwa ni rahisi kuliko kujenga barabara hiyo na mkifanikiwa hivyo, nitashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne, kwa kweli Serikali mnachelewa kupeleka pesa kwenye Halmashauri zetu. Pesa zinachelewa mpaka wananchi wanaanza kuwa na wasiwasi. Wanasema Mbunge wetu mgonjwa na barabara zetu nazo ngonjwa? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nategemea *by the end of this year*, mambo yote yatakuwa sawasawa na mimi nawahakikishia wananchi wangu wa Jimbo la Kilwa Kaskazini, wakae mkao wa kula, mambo yatakuwa mazuri kadri Mungu atakavyotuwezesha. Mimi nitasukuma na nitakuwanao bega kwa bega mpaka kuhakikisha kwamba barabara zote zinafanya kazi kama ilivyopangwa na kama nilivyoahidi wakati wa kampeni za kutafuta kiti hiki nilichokikalia leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri, Rais, Makamu wa Rais kuja kwetu kule kuona majabu yaliyoko kule, inakuwa ngumu kweli kweli. Kule kuna vitu vingi ambavyo pengine wengine hamjawahi kuviiona hata siku moja. Kuna minazi, michungwa, midimu na kila kitu na Kilwa ilivyobadili sasa hivi si ile Kilwa ya zamani, tupo juu juu, juu zaidi na mimi nasema kidumu Chama cha Mapinduzi kwa kusikia kilio chetu. Japokuwa Mbunge wao kidogo ana hitilafu, ila sasa niko ngangari kinoma, karibuni sana ndugu zangu. (*Kicheko/Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina mengi sana ya kusema ila msipotimiza mambo ambayo mmeyaa hidi na ambayo mmeanza kuyafanya vizuri mwaka 2010 nitakuja na lugha nyingine kabisa sio kama hii na tutaanza vitu vingine tofauti na mimi simhofii mtu na wala simuonei haya mtu. Lakini sitegemei haya yatatokea naamini mambo yatakuwa mazuri na Mungu, *Inshallah*, atatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Kilwa Kaskazini, ahsante sana. (*Makofsi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nashukuru sana. Kuna matatizo kidogo, Waheshimiwa Wabunge wengine wameonekana kwenye orodha yangu kwamba walikwishachangia hotuba zilizopita, haya yalikuwa ni makosa madogo madogo ya

Sekretarieti, sasa naomba kulisahihisha hilo, Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, ni kweli hujachangia hotuba za bajeti. Kwa hiyo, tutaona ni namna gani tutaweza kulizingatia kwenye orodha hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa Dr. Anthony Diallo, naomba niwatangazie kwamba tunao wanafunzi 50 wa Shule ya Msingi Amani kutoka Dar es Salaam wameongozana na Walimu wao, ninawakaribisha sana na ninawataenia kila la kheri katika kuangalia shughuli za Bunge, karibuni sana. (*Makofii*)

**MHE. DR. ANTHONY M. DIALLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniruhusu kuzungumza kwenye hoja iliyopo mbele yetu.

Kwanza, nimshukuru Waziri na timu yake kwa kutuletea bajeti ambayo kulingana na nilivyomsikiliza asubuhi, huenda ikatatua baadhi ya matatizo tuliyonayo lakini kama utekelezaji utakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuingia kwenye hoja yenyewe, naomba nizungumze machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge tunapokuwa hapa, tunazungumza kwa niaba ya wananchi wetu. Sasa tunapowauliza Mawaziri, tukaonekana tunatumia labda lugha kali, wasituelewe vibaya, hiyo ni kwa sababu ya kukaa mwaka wa kwanza unaahidiwa, mwaka wa pili unaahidiwa, mwaka wa tatu huoni kitu na unaona mwisho unakaribia, kwa hiyo, Mbunge ni lazima atakuwa mkali. Siyo kwa sababu ya uchaguzi, sikubaliani na ile hoja kwamba Wabunge wanakuwa wakali kwa sababu presha inapanda, presha inashuka, hii ni kawaida miaka yote, kwamba mtu ukimwaahidi, kwa uungwana atasubiri mwaka wa kwanza, wa pili na mwisho atakuwa mkali sana na mwaka kesho itakuwa mbaya zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika mipango yetu ya maendeleo ya nchi hii, bajeti ni mali yetu wote, nikimaanisha Serikali, Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wote wa Tanzania. Sasa kusitokee vikundi ambavyo vinaona vyenyewe ni vya muhimu zaidi na mipango yao inaweza kwenda mbele zaidi, kuliko Wabunge wengine, kuliko maeneo yetu tunayowakilisha wananchi, mambo yakienda vibaya wote hapa tunakuwa *responsible*, ndiyo maana tunasema kuna mambo wanayoyafanya wenzetu Serikalini, mengine hatukubaliani nayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipangilio ya fedha hizi kwenye barabara ambazo wamependekeza, kesho tutaleta mapendekezo ya kubadilisha. Ninaomba sana Waheshimiwa Wabunge tuelewane, kwa sababu uwezo wa kubadilisha tunao na tusipobadilisha, hawa hawatapata somo. Ilishatokea mwaka 1997 na nina hakika, tunaweza kufanya na sasa mbele ya safari watakuwa waangalifu zaidi kwamba nikipanga ninavyoona inanifaa mimi, kuna uwezekano Wabunge na Bunge kubadilisha mpangilio huo. Kanuni zinaturuhusu, utawala ni wa pamoja, Bunge na Serikali na vyombo vingine vya dola. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upangaji wa miradi wa mwaka huu, unanishangaza kidogo, kwa sababu katika Sera zetu, tulikubaliana kwamba barabara zinazounganisha Mkoa na Mkoa, ndiyo kipaumbele chetu namba moja na barabara zote zikaainishwa. Bahati nzuri, wakati ule kulikuwa na Wizara inaitwa Mipango, kwa bahati mbaya sana tunaanza kuona dosari ya kukosekana kwa Wizara ya Mipango, kwa sababu unapoweka mtoa pesa na mtengeneza mipango ni yule yule kunakuwa na matatizo makubwa sana na matatizo haya tunaanza kuyaona mwaka huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ambazo zimefanyiwa usanifu au upembuzi yakinifu mwezi wa tano mwaka huu, mwezi mmoja na nusu uliopita, tayari zimepata *allocation* ya pesa, tunaacha barabara za muhimu ambazo tulikubaliana kama Taifa kwamba ni kipaumbele namba moja. Mfano barabara ya kwanza ilikuwa ni hii ya kutoka Babati, Kondoa, Dodoma, Iringa, ndiyo ilikuwa kwenye *priority* namba moja. Barabara ya pili ilikuwa ni kutoka Manyoni, kuunganisha na Kigoma. Sasa barabara hizo, kwa bahati mbaya sana hatia ile ya Manyoni ambayo tulikuwa tunaitegemea kwamba itajengwa, *contract* hiyo nasikia imefutwa, wanataka wabadilishe eti waanzie Tabora kuja Manyoni ambapo itachukua mwaka mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge mliopo kwenye eneo hilo, ni lazima mjue hilo. Tungeacha *contract* ifunguliwe, waanzie Manyoni kuelekea Tabora. Tukitaka waanzie Tabora, ni mambo mapya, kutangaza *tender* upya na kuna muda unaohitajika mpaka utafika mwaka wa uchaguzi, hamjaona barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine linalonishangaza ni kwamba nchi yetu inafuata mfumo wa Serikali zote duniani, kwamba fedha zinakuwa *allocated* kwa mwaka mmoja, sasa umezuka mtindo wa fedha zinawekwa kidogo mwaka huu, hazitumiki, zinapelekwa mbele utadhani sasa siyo nchi ni kampuni kwa sababu kampuni ndiyo zina-close tarehe 30 mwezi wa sita lazima fedha zote zirudishwe Hazina. Sasa huu utaratibu wa kusaini mikataba ya fedha za mwaka jana, tunasema sawa, za mwaka huu tutazi-*allocate* kesho, tutaleta mabadiliko *tuzi-allocate* kwa sababu hawajapata ruhusa na utaratibu upo, tutaufuata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zisipotumika, zinarudishwa maana namna hiyo watu wataanzisha mradi, nitawapa mfano. Barabara ya kutoka Dumila kwenda Mikum, ni kilomita karibu 207, ni shilingi bilioni 156 kulingana na makadirio yao, safari hii wameomba shilingi bilioni nane, bado itahitaji miaka mingapi kumaliza hiyo barabara? Ina maana kila mwaka, fedha za barabara itabidi ziende kule, ndiyo hatari ambayo tunaanza kuiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika kuna baadhi ya mambo ambayo hayaeleweki kwenye bajeti, nina hakika Waziri kesho wakati ana-wind up, atatueleza vizuri. Mfano kiwanja cha ndege cha Mwanza, wametenga shilingi milioni 700 na ni kwa ajili ya viwanja viwili ambavyo vinaonekana kwenye kitabu cha bajeti yaani ni Mwanza na Kigoma. Hata barabara ambazo ni za kiwango cha lami zinaanza kwenda na zenyewe kwenye shilingi milioni 500 na kuendelea kwa kilomita mmoja, sasa hizi shilingi milioni

700, utajenga kweli viwanja viwili vya ndege? Labda kwa viwango vya changarawe! Nitaomba sana Waziri naelewa yupo makini atajaribu kutufafanulia vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Dar es Salaam *expansion*, mimi sielewi kabisa. Unajua wakati mwingine tunakosa *business skills*, wewe kiwanja cha ndege tayari kiko *congested*, kiko katikati ya mji, leo unatumia nadhani shilingi bilioni karibu 35 kwa kiwanja ambacho *in the next ten years*, hakitakuwa kinafaa tena kwa Dar es Salaam, sasa hizo shilingi bilioni 35 kwa nini usitumie kwenda kujenga kiwanja kipyä kwenye *green areas* kama Kisarawe na sehemu nyingine, ukajenga na barabara ya kwenda na kurudi *Airport* kama tunavyoona Johannesburg na Pretoria, barabara ni *non stop* utakwenda mpaka *Airport*. Sasa shilingi bilioni 35 bado utaanza kujenga *runways* upya, unajenga *runway* ya nini, hicho kiwanja cha mjini kinatakiwa kuwa *for business jets* yaani mtu ana ndege zake anakuja kutua huko mjini, baada ya muda hicho kiwanja kitakuwa hakifai!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna-spend pesa leo shilingi billioni 35, sijui shilingi bilioni 40 kufidia watu tu, bado hujajenga kiwanja, kiwanja nacho *expansion* hii itachukua karibu ya shilingi bilioni 27, karibu shilingi bilioni 60 pamoja na *cost over running*, itakuja karibu shilingi bilioni 80 na bado si chini ya miaka kumi utatakiwa kujenga kiwanja kipyä. Ndugu zangu, tuwe makini na matumizi yetu ya pesa, namna hii hatutafika popote ni kama tunavutia sigara pesa zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nadhani nitapata majibu kama inavyotakiwa na nina hakika Serikali wanatusikia, wasichukue mambo haya *personal*, tukisema hapa, ni eneo letu la kujidai na tunapozungumza kwa kufoka, mtu anafokea *institution* siyo mtu mmoja. Kwa hiyo, nina hakika wenzetu watatuelewa, siyo tutoke hapa, mtu mwingine hata kusalimiwa, hasalimiwi. Namna hiyo mtakuwa mnatuchukulia vibaya na hizo kazi zitakuwa haziwafai kwa sababu mnaelewa *limit* na majukumu yanayotuleta hapa Bungeni. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na nitaunga mkono hoja baada ya kupewa ufanuzi huo, ahsante sana. (*Makofit*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Dr. Anthony Diallo. Baada ya kupata mchango wa Mheshimiwa Dr. Anthony Diallo basi sasa nimwite Mheshimiwa John Paul Lwanji na Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni ajiandae.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Nikutake radhi kwa kuchelewa kidogo kwa sababu Mji wa Dodoma sasa hivi umekuwa na magari mengi, kwa hiyo *traffic* imekuwa kubwa na ndiko tunakoelekea Mji Mkuu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba niishukuru Serikali, kwa sababu sijachangia upande wa bajeti pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini nimepata bahati hii, niwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Manyoni Magharibi, kwa uvumilivu wao na nadhani wataendelea kunivumilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali kwa kunijengea Ofisi ya Jimbo na ninashukuru sana Ofisi ya Spika, kwa kuelekeza kwamba Manyoni Magharibi, Itigi ni mbali kwenda Manyoni Mjini kwa hiyo kulikuwa na umuhimu wa Serikali kujenga ofisi pale Itigi na ninataka kukuhakikishia Mwenyekiti, ofisi ni nzuri na shilingi milioni arobaini zimetumika vizuri. Watu wanasema ni ndogo lakini mimi ninahitaji ofisi na ukumbi na sehemu ya wasaidizi wangu kufanya kazi, sihitaji sehemu ya kulala mle, kwa hiyo, nadhani inatosha kabisa. Nashukuru sana kwa hilo na nadhani adha ya watu wa Itigi kwenda Manyoni mara kwa mara kunifuata sasa itakwisha na tutachapa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru pia kwa Serikali kutenga fedha kwa ajili ya hospitali ya Mkoa wa Singida. Hiyo ni hatua kubwa sana kwa Mkoa wetu kwani ni hospitali ya kisasa inayojengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sitakuwa mbali sana na msemajii aliye kaa sasa hivi. Ninaipongeza Serikali na ninampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jitihada zake kubwa za kusaka fedha kwa wafadhili kwa ajili ya barabara ya Manyoni, Itigi, Chaya, Tabora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeipigia kelele sana barabara hii na mara nyingine watu wamepata kizunguzungu, tumesikia Serikali ya Kuwait, tumesikia Saudia, Iran mpaka vichwa vinazunguka, ni nani hasa atajenga barabara hiyo. Juzi tukapata taarifa kwamba Serikali ya Iran imeingia mkataba na Serikali yetu kujenga barabara kutoka Manyoni – Itigi – Chaya na tenda zilitangazwa na Wakandarasi wakakaribishwa kupeleka *bids* zao. Nasikitika sana taarifa hii imekuwa kinyume kabisa na hotuba ya Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa hawa Mawaziri wa Wizara hii ni waadilifu sana na sikutarajia hata kidogo kwamba wangekuwa na tatizo. Kuna matatizo mengi Wizara hii, lakini wanaongeza matatizo juu ya matatizo. Wakati nafuatia masuala, haya nimefika ofisini kwao ni waadilifu kweli kweli! Kwanza Mheshimiwa Kawambwa kaanza hata kutumia gari aina ya *Isuzu trooper* kuonyesha mfano wa kupunguza gharama na mambo mengine. Sasa nilikaribishwa nikanywa chai, lakini tatizo ni kwamba majibu yangu katika muda wa siku tatu hawakuweza kunipa kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ukurasa wa 56 pale inapoanza: “Aidha, nafikiri ni ile miradi ambayo iko katika mchakato wa kupitiwa makandarasi wa kujenga...” Sijui nianzie wapi, kwa sababu ni sehemu ndefu. Lakini imesema: “Aidha, miradi ambayo ipo katika mchakato wa kuwapata makandarasi ni Sumbawanga, Kasesya, Kasanga, Poti kilomita 105, Tanga - Horohoro – Songea – Namtumbo, Tunduma – Sumbawanga, Songea – Mbanga, Dodoma – Babati – Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi, Manyoni – Itigi – Chaya.” Lakini pamoja na kwamba hiki ni kitabu cha bajeti which is more assertive na ndio maandishi haya, lakini cha ajabu Mheshimiwa Waziri hakusoma hiki kifungu. Amesema kwamba hii imekuwa relegated, maana yake ni kwamba imekuwa relegated hii Manyoni – Itigi, sasa yenye we haiko katika mchakato wa kutafuta wakandarasi, iko katika mchakato wa upembuzi yakinifu na usanifu. Halafu

ikatajwa barabara kutoka Tabora kuja Nyahua ndiyo ambayo inapata wakandarasi na inaanza kujengwa kwa lami.

Kwa hiyo, sishangai hata mwenzangu hapa amezungumza kwamba wame-revise wakati makandarasi na tenda zimetangazwa sijui kama watanunua magazeti yote kuficha ushahidi. Haiwezekani! Ni mtu mmoja tu kaenda kumwona Mheshimiwa Waziri Mkuu kamwambia bwana kwa nini inakuwa hivi? Hivi Jimbo la Manyoni Magharibi liko wapi? Hii iliyosuasua sana ya kutoka Dodoma kwenda Manyoni ndiyo hapa inaanza kupiga hodi ni kwa Mheshimiwa Chiligati na Mji wa Manyoni unakwenda kwa Mheshimiwa Chiligati Jimbo la Manyoni Mashariki. Mimi kote ukisema kutoka Manyoni, Itigi, Tabora, hakuna; Manyoni – Mkiwa – Isuna, hakuna. Leo ni utashi wa mtu au watu wakisema bwana haiwezekani, tena ni wa CCM sisi wenyewe! Sijui watatuambia nini katika suala hili. Rais katafuta fedha.

Hivi nchi hii inaanzi wapi jamani? Si inaanzi Dar es Salaam! Mamlaka yanaanza wapi? Hata Mjerumani wakati anajenga reli alianza kupeleka mataruma Kigoma? Haikuwezekana hata kidogo! Hizi ni *expenses* za ajabu sana kwa sababu utatoa lami, utatoa sijui vifaa vya ujenzi vyote unavihamisha kutoka Dar es Salaam kwenye *port* mpaka Tabora hapa katikati unaacha kujenga, hizo gharama ngapi? Haya ni utashi wa kisiasa zaidi. (*Makofi*)

Jamani, tatizo, hawa wenzetu tunawalaumu bure, tunasema wanapendelea hawa watendaji, sijui Mawaziri; mimi nawaambia tunawavuruga sisi wenyewe. Mpango ulishapangwa, sisi tunaingia jikoni sasa. Ni haki? Kweli huu ni uungwana? Mimi sijawahi kuona hata siku moja. Huu si uungwana hata kidogo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaambia kifungu cha 103 itabidi kitumike kwa Wizara hii. Kweli kabisa! Kama hatutaeleza sababu, viti hivi wote tunafanana, viti hivi ni vyekundu, mimi sikuja hapa nimeletwa na wananchi wa Manyoni Magharibi kuja kukalia kiti cheusi hapa, kiti changu ni chekundu au hamwoni? Kiti changu hiki ni chekundu.

**MWENYEKITI:** Ni chekundu Mheshimiwa Mbunge, viti vyote humu ndani ni vyekundu isipokuwa cha Spika.

**MHE. PAUL LWANJI:** Sasa damu yangu ni ya kunguni? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mimi nadhani sitendewi haki, hatukutendewa haki hata kidogo. Watumishi wa Serikali watalaam wamekaa wameona ni vyema waunganishe nchi, sisi tunataka Mikoa. Unaona, vimikoa *parties* hapa na hapa ndiyo barabara zetu zilivyo kuonyesha kwamba ioneckane kuna *activities*, sasa ndiyo mnaniuza! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mimi naomba, tunasema tunazungumza kwa lugha kali, ndiyo hivyo kwa sababu ni sisi wenyewe ndiyo tunajivuruga. Ni lazima tutazungumza kwa lugha kali. Ijumaa iliyopita, nataka narudia, wakandarasi

wamekwenda kupeleka tenda ya hii barabara wakaambwa aah! Hii barabara, basi imeahirishwa. Sasa nadhani watatengeneza maana magazeti yapo yaliyotenda na kila kitu na ushahidi, nchi imetangaziwa sasa inatakiwa sasa barabara itangazwe ianze kujengwa, tena imetangazwa haraka haraka. Sasa wote tunagombania fito moja, mimi fito nimezipata unaninyang'anya! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ndugu zangu, nataka maelezo ya kina kwa sababu hiyo sehemu inapita kwa John Paul Lwanji au kwa nani? Kwa sababu wale ni wananchi na ni haraka haraka unatoka hapa unaelekea hivi, unakwenda haraka haraka, sasa unafika katikati tena, matatizo. Afadhali ijulikane sehemu moja mnakwenda, tunamaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hilo nadhani nitaomba maelezo ya kina na nimewaeleza nimemwona mpaka Waziri Mkuu nimemwandikia *ki-note* pale, *no body is answering*. Nilipomwuliza mtu mwingine aka-*shift blame*, kuna matatizo ya ilani. Ilani wapi na wapi? Serikali imeshinda kwa kishindo kwa kura zaidi ya milioni moja, amemshinda mpinzani wake, itaondoka wapi? Eti Serikalini kuna matatizo! Kule huenda fedha, wakati *memorandum of understanding* imekuwa *signed* na mambo mengine fedha zipo. Mheshimiwa Waziri nitaomba jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo kana kwamba hiyo haitoshi barabara ya Rungwa. Itigi – Mkiwa, Itigi – Rungwa – Chunya wenzangu wameizungumzia hapa Mheshimiwa Askofu amezungumza vizuri sana, lakini historia hii ya upande wa barabara hii kutoka Itigi kwenda Rungwa mwaka 2004 ilipata mkandarasi *Badre East African Construction Company* na barabara hii ikaunda mradi maalum wakisema ni mradi wa Elnino kwa sababu *infrastructure* yote iliharibiwa na mafuriko, ikatengewa fedha za kutosha. Tatizo sio Serikali.

Tatizo ni kwamba mkandarasi yule aliyepewa akaenda ku-*messup*, yule akafuata starehe huko porini na mambo mengine, hakufanya kazi. Mheshimiwa Magufuli wakati anakagua barabara akaenda kumfukuza na mradi ule ukafungwa na alipoondoka ndiyo ukafungwa. Basi zimekuwa zikitolewa fedha kidogo kidogo na safari hii nimeangalia ni asilimia 10 sijui ni 15 zimepanda kutoka barabara ya Rungwa, bado **parch** zimefichwa hivyo sehemu korofi ziko vile vile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri wanayofanya sasa hivi lakini sasa hawaunganishi hata ukatengeneza sehemu vizuri, lakini unapofika sehemu nyingine unakuta kwamba ni korofi huwezi kutumia hiyo barabara. Ningeliomba tena hapa waangalie aidha warudishe ule mradi kabisa. Lakini mimi juzi juzi nimewaandikia barua hawajajibu mpaka leo. Tuliomba watenge angalau Shilingi bilioni tano siyo bilioni moja na unakuta zile *periodic maintenance* zinaletwa, zile za maendeleo haziji. Sasa kutakuwa na *shortfall* ya hapa na pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sana. Sina tabia ya kuzungumza kwa ukali namna hiyo, lakini imenibidi nifanye hivyo kwa sababu naonewa. Tunaonewa bila sababu! Hapa huyo sijui mnayesema sungura ni lazima tugawane sawa sawa hata kama ni kucha tupate! Haiwezekani hata kidogo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, nitaunga mkono hoja pale kutakapokuwa kumefanyiwa mabadiliko na kwa kweli utashi wa kina kuonyesha kwamba barabara hiyo inarudishwa na mchakato unaendelea kama kawaida, hizo *bids* zikubaliwe ,vinginevyo sioni sababu ya kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Huyo alikuwa ni Mheshimiwa Paul Lwanji. Baada ya kumsikia Mheshimiwa Paul Lwanji akisisitiza mgawanyo wa sungura hata kama ni kwato, basi tuendelee kumsikiliza Mbunge anayefuata.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru sana kwa kuweza kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia hoja hii ya Waziri wa Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanga ni kuchagua na kila mwaka tunapokutana hapa huwa tunapanga. Tatizo ambalo nililonalo kidogo ni namna tunavyopanga mipango yetu. Ukitu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, tunazungumzia ziliwu kazi za mwaka juzi, za mwaka jana, kulikuwa na upembuzi yakinifu, kulikuwa ku-*award*, kazi kwa makandarasi na kadha wa kadha.

Lakini katika kitabu hiki kimechanganywa kiasi kwamba hata unashindwa *ku-track* vizuri kwamba kazi zipe ziliwu zinaendelea, zipe zimepewa kipaumbele safari hii na kadha wa kadha. Sasa hii inafikia kila mahali ndiyo Wabunge tunalalamika kwamba kunakuwa pengine na tabia ya watu kujipendelea kitu ambacho sio kizuri kwa nchi yetu.

Mpango wowote wa bajeti unapaswa kuwa na *correlations*. Lakini licha ya kuwa na *correlations* lazima kuwa na *coordination* vile vile. Haiwezekani miradi mipya inaanishwa leo ina-*override* miradi ya huko nyuma. Kumekuwa na kisingizio cha mara kwa mara kwamba hii fedha kuna mhisani tunamsubiri, hii fedha mhisani kapatikana hii bado. Lakini nadhani kila Mkoa una haki sawa na kila eneo lina haki sawa. Mipango ambayo tulipanga kwanza ukiangalia tulisema kwamba hata Dodoma yenewe hii inaweza ikakua tu kwa sababu tumefungua miundombinu kwamba barabara kutoka Kaskazini – Arusha kwenda Iringa imefumuliwa, barabara kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza, kwenda Kigoma imefumuliwa. Tukifanya vile kwanza kwa haraka maana yake tumefungua nchi. Lakini inavyoanza kuzuka miradi mingine, mara ya kukatiza hapa, mara ya kutoka hapa kwenda huku, sasa haya yote yanavuruga mpango mzima wa nchi. Naomba tufikiri kama nchi, tusifikiri kama watu *individual* ndani ya nchi kwa sababu hakuna raia ambaye ana haki sawa ya raia mwingine. Hii nchi ni yetu sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema hivi na tunaomba Wizara ya Miundombinu, ina dhamana kubwa sana kwa sababu hatuwezi kuongeza *production* katika nchi hii bila kufungua namna ya kufikisha mazao yetu, namna ya kusafirisha mali na kadha wa kadha. Hii yote inatokea kwa sababu kumeanza kutokea tabia ambayo siyo nzuri. Naomba kwamba tatizo hili likome. Naomba Waheshimiwa wanaohusika kuandaa bajeti tuangalie

*priorities za nchi ni zipi and then tuweke the self interest ambazo tunaziweka katika mipango hii. Kwa sababu vinginevyo tuna-confuse the whole thing.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wanazungumza hapa, lakini sio kwamba wamechukua, lakini tunadhani kwamba kuna haja sasa ya kutumia lugha yeny uzito kidogo, yeny mtekenyo kuona kwamba hatujafurahishwa na baadhi ya mipango. Pale ambapo wamefanya vizuri tunawapongeza. Ndiyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushukuru kwamba kuna miradi ambayo inaendelea kwa mfano tumekuwa na hadithi ya kujenga *terminal* ya *airport* ya Mwanza. Ni muda mrefu sana. Unapojenga *terminal* Mwanza, uwanja wa Mwanza ukawa Uwanja wa Kimataifa, umefungua Tanzania katika nchi hii na nchi za Maziwa Makuu. Tunaongeza uchumi katika nchi yetu! Hili hatulioni. Leo unazungumzia Mwanza kuitengea Shilingi milioni 700 pamoja na kiwanja cha Kigoma, hivi *what are you talking about?* Naomba tuangalie jamani hii nchi tujaribu kuipa haki yake na hadhi yake. Leo hii Mwanza uwanja wa Ndege ukiweza kuwa uwanja mkubwa utasaidia kuongeza mapato, bajeti ya nchi itakua na utegemezi utapungua.

Lakini leo hii kana kwamba hakuna anayesikia namna hiyo. Sasa tunahitaji Waziri atoke Mwanza kwa Wizara ya Miundombinu ndio tupate uwanja wa ndege wa Mwanza. Tunaamini kila Mtanzania ana haki ya kufanya hivyo kwa sababu ni nchi yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si mambo mazuri sana kwa sababu hata ukiangalia kwenye hotuba ukurasa wa 79 Waziri kasema, naomba ninukuu kidogo hapa kuonyesha jinsi ambavyo hayuko *serious*. Anasema: “Kuhusu kiwanja cha Mwanza, awamu ya kwanza na ya pili ukarabati na upanuzi, maegesho ya ndege za mizigo na viungia vyake imekamilika.” Hatukatai, huu ni muda mrefu imekamilika, tunachotaka Mwanza ni *terminal building* ili uwanja ufanye kazi kama uwanja wenye hadhi. Leo hii *run way* ya Mwanza kwa taarifa zilizopo hapa ni *all the best run way* hapa nchini. Lakini hakuna *terminal, then what are we doing*. Tunafanya vitu nusu nusu. Haya mawazo nusu tuachane nayo, tufanye vitu kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la *ATCL*. Hivi kweli Mheshimiwa Waziri uko *serious* na *ATCL* kwa sababu kwenye ukurasa wa 74 umezungumza hapa, kwanza *ATCL* hii iko mahututi, leo hii ndege inayoruka ni moja ile *Dash 8* ile nyingine iko Mwanza *grounded* pale. Hivi kweli tumefikia hapa, tunasema kuna mwekezaji Mchina, atakuja lini? Ni nini juhudzi za Serikali kuiokoa *ATCL* usafiri na hasa sasa wa ndege ni kiungo muhimu sana kwa uchumi wa nchi. *Then are we serious?* Iwapo nchi nyingine leo Uganda walikuwa wame-ground baada ya kuingia mkenge na sisi kwenye *alliance*, leo wenzetu wana ndege nyingi za kwao, wanaruka, wana ile ambayo inaitwa *Sound*, leo sisi tunaishia kukodisha ndege za ajabu ajabu ambazo zimeshachoka. Hivi mnataka Watanzania wafe kwenye hizi ndege zetu ndiyo tuone kwamba sasa kuna dharura?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kwa sababu mimi sioni ni kwa nini *we are not so serious*. Leo ni mwaka wa pili tunasema *ATCL* tunarekebisha, mimi nashangaa! Hiyo Bodi ya *ATCL* mimi sioni hata hiyo inafanya kazi gani. Ile Bodi haina kazi, wanaongeza gharama kubwa zaidi. Lazima tufanye *restructure* kwenye *ATCL*. Leo unazungumza kwamba *ATCL* changamoto zinazoikabili ni kuboresha huduma zake na kupunguza gharama za uendeshaji. *Then what are we talking?* Leo ina ndege moja ya watu kama 40 namna hii inayoruka sasa hivi.

Hii nchi jamani inasikitisha sana. Wewe unaamua kuleta *airbus* una- *phase-out Boeing*, bado ma-pilot wa *Boeing* unao unaongeza gharama za ma-pilot wengine wa kuendesha *airbus*. Hivi mtu unafikiri huhitaji kwenda Chuo Kikuu au shule kujua hesabu za A, B, C, D? Hahitaji! Ni watu na mawazo na mtazamo wa kufanya shughuli za biashara kwa ajili ya nchi hii. Wanafanya miradi! (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kingine, *to be honest, I am very sorry*. Hivi kweli unamkabidhi mtu aongoze Shirika kama *ATCL* mtu ambaye hana hata taaluma sahihi katika *industry* husika, hivi tunategemea tutasonge mbele kweli? Halafu leo huyu mtu unampa *assignment* nytingine unaacha mtu mwengine akaimu nafasi yake. Mtu anayekaimu na mawazo yanakuwa ni ya kukaimu. Hatutaweza kusonga mbele. Kuna tatizo gani Mheshimiwa Waziri *ATC*? Mimi naona shirika letu la ndege, kwanza ukiangalia ni sehemu kubwa sana kwa ajili ya kuleta vivutio na kutangaza nchi yetu. Lakini pili ni usafiri ambaeo ni wa karne hii. Watu wanafanya biashara, wanafanya shughuli zao.

Leo tunategemea ndege nytingine, wenzetu hapa Kenya *airway we have all the lessons* wametangaza nchi yao vizuri sana, wanaendelea vizuri sana na *Precision Air* ambaeo wameanza hivi karibuni, sasa wako mbele zaidi, leo chombo cha Serikali ndiyo kiko mahututi kweli! *Are we fair to our country? Are we honest ourselves?* Ni aibu kubwa sana. Mheshimiwa Waziri ninaomba kwa kweli unapokuwa una-*windup* hoja yako nataka maelezo ya kina kwamba *how do we move on ku-rescue ATCL*, vinginevyo kwa kweli sijui patakuwaje hapa ndani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la barabara. Kuna barabara. Kuna barabara unakuta imeandikwa isizidi uzito wa tani 10 na barabara ya Nyashimo – Ngasamwa, hii barabara upande wa Mkoa wa Shinyanga ni *trunk road*, upande wa Mkoa wa Mwanza ni *regional road*. Sasa magari yanayopita upande wa Mkoa wa Shinyanga kwa sababu ni *trunk road*, yana uzito mkubwa zaidi. Upande wa Jimboni kwangu ni uzito mdogo, yakipita yanaua zile *structure*, madaraja yana-fall. Sasa unajiliza, hivi tuwaambie kwamba mkishafika hapa mshushe mizigo yenu kwanza mpakie kwenye gari nytingine ndogo ndiyo muweze kupita kwenye barabara yetu? Hivi tutakwenda namna hii? Tunapaswa kuwa na barabara ambazo hazina *dead end*. Lazima tuchukue jitihada yetu turahisishe *movement* ya mazao na bidhaa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Wizara hii nadhani kuna haja ya kuangalia namna gani muweze ku- *correlate* mipango yenu ili iweze kusaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka kwa sababu muda umeshakwenda, nashukuru barabara ya Lamadi – Bariadi Mwigumbi imeshatangazwa na nilikuwa najaribu kuangalia kwenye kitabu hiki, sikuona fedha, lakini baadaye nikaambiwa kwamba fedha zipo zimeshatengwa shilingi bilioni sita za kuanzia, sawa tunashukuru. Lakini sambamba na hii barabara ya Nyanguge, kwenda Musoma ni ya muda mrefu sana, imeshakuwa na mashimo.

Lakini kibaya zaidi kuna sehemu ambazo zina matatizo ya *congestion* ya watu sehemu ambazo kuna msongamano wa watu. Watu wengi wanagongwa na magari kwa sababu hakuna matuta. Nilikuwa naomba angalau sehemu ambazo zina matatizo haya kama pale Nyamikoma, kama pale Kalemela na hata Lamadi yenyewe tuweke matuta kupunguza kasi ya magari kwa sababu watu wengi wanagongwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, napenda sasa nimalizie kwa kusema kwamba kuna yale mazuri mnayafanya tunawapongeza. Sio kwamba mnafanya mabaya tu, mmeefanya mazuri mengi sana. Tunapongeza sana Wizara hii kwa yale ambayo ni mazuri tunawapongeza wewe Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wote. Lakini tunasema hivi, tufikie mahali sasa tufikiri kama nchi. Tusifikiri kama mtu kwa utashi wake.

Tufikiri kwa utashi wa nchi hii. Wenzangu wamesema sitaki kurudia lakini Mheshimiwa Waziri nadhani ni changamoto kwako. Hainingii akilini kweli kwamba tunawaza kujenga uwanja mwingine au kufidia watu Kipunguni na Kipawa huko Dar es Salaam kwa bilioni 30 wakati huo huo tungeweza kujenga uwanja mwingine mpya sehemu nyingine na ikasaidia zaidi. Mawazo kama haya tuyafanyie kazi. Tusiwe na mawazo mviringo. Mawazo mviringo hayawezi kutotoa pale tulipo. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri na bahati nzuri wote ni watani zangu hata mkikasirika mimi ni baba yenu nitasema tu. Lazima tuwaambie mwelewe haya, mna dhamana, kwa sura zetu ni wapole kweli. Naomba muwe jasiri wa kufanya vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Miundombinu. Kabla sijasema lolote, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu Dr. Shukuru Kawambwa na Naibu Waziri Mheshimiwa Chibulunje pamoja na Watendaji wengine wa Wizara ingawa itaniwia vigumu kweli kuunga mkono hoja yao kabla ya kupata maelezo kwa haya ambayo nitayaeleza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza pia Serikali kwa shughuli nzuri au kwa kujenga Chuo Kikuu cha aina yake hapa Dodoma na sasa Serikali ina mpango wa kujenga (*airport*) Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa hapa Dodoma eneo la Msalato ingawa katika ukurasa wa 18 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Kawambwa ametenga Sh. 1,600,000,000/= kiasi ambacho hakisaidii kitu. Hata katika hotuba yake hakueleza

kwamba kiwanja hicho kitaanza kujengwa lini au hizo fedha ni za kufanya nini. Sasa hilo sitalizungumza kwa sababu ni mradi wa hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Wabunge wenzangu ambao wametetea sana barabara ya Babati – Dodoma, Dodoma – Iringa kwa sababu wanaelewa umuhimu wa barabara hiyo. Nadhani waliopanga bajeti hii hawaelewi umuhimu wa barabara hiyo. Barabara hiyo ni barabara iliyobuniwa zamani enzi za mkoloni (*Great North Road*) inayotoka Cairo mpaka *Cape Town*. Maeneo yote barabara hii ni ya lami. Lakini ukifika Babati mpaka Iringa barabara hii siyo ya lami. Wabunge wenzangu wamechangia sana kwamba katika barabara muhimu ndani ya nchi hii barabara ingepewa umuhimu wa namna moja. Lakini sielewi huyu anayepanga, Mhandisi anayeshirikiana na wenzake kupanga barabara zilizo muhimu katika nchi hii anaifikiriaje hiyo barabara. Mwaka jana tulipewa Shilingi bilioni 12, hizo Shilingi bilioni 12 zimeyeyuka, hatuelewi zimekwenda wapi, hazijafanya kazi yoyote. Tulitegemea juzi Waziri aliposema kwamba Waheshimiwa Wabunge wa baadhi ya Mikoa waende *VETA* pale anavyotia saini mikataba mbalimbali na wakandarasi.

Nilisikiliza kwa makini nikitegemea Dodoma tutatajwa, hatukutajwa Dodoma, Iringa hawakutajwa na Manyara hawakutajwa. Kumbe barabara yetu haipo kwenye bajeti. Hivi tunakwenda wapi? Mwaka huu wa fedha barabara hii imetengewa Shilingi bilioni 5.6, hizo ni za kufyeka msitu ambao uko kando kando ya barabara au ni za kufanyaje? Kwa sababu bilioni 12 hazijafanya kazi, bilioni 5.6 hatujui zitafanya kazi gani. Tupewe Shilingi bilioni 12 zetu za mwaka za mwaka 2008/2009 tujue zinafanya kazi gani, kwa sababu isije ikawa kama kiini macho kwamba zile Shilingi bilioni 12 zimewekwa mfukoni zimepelekwa mahali pengine.

Sasa Shilingi bilioni tano ndio tunapangiwa kwa ajili ya mwaka huu. Hapana. Tunataka kujuua, Shilingi bilioni 12 za mwaka 2008/2009 zimefanya kazi gani? Maana mwaka umekwisha, ulikwisha jana, hakuna mkandarasi yeote barabarani hata aliywewka kibao, hata aliyefyeka eneo la kazi, hayupo. Sasa leo tumepangiwa Shilingi bilioni 5.6, za nini? Tuelezwe! Hizo Shilingi bilioni 12 zimefanya kazi gani za mwaka jana na Shilingi bilioni 5.6 za mwaka huu zitafanya kazi gani? Lakini mimi nadhani sisi wa Manyara, Dodoma na Iringa tuijhesabu kwamba tuna Shilingi bilioni 17 hasa Dodoma – Babati, tuijhesabu kwamba tuna Shilingi bilioni 17 wala siyo Shilingi bilioni 5.6 za mwaka huu. La sivyo, Serikali ituambie Shilingi bilioni 12 zimefanya kazi gani?

Jamani chakula kinapikwa hapa hapa Dodoma, leo Wabunge tunapitisha bajeti za Wizara mbalimbali hapa hapa Dodoma, lakini chakula hiki kinaliwa nyumba ya tatu. Sisi wa Dodoma tumeachwa kila siku tunapiga kelele. Tumechoka kupiga kelele tuambiwe fedha zilizotengwa zimepelekwa wapi Shilingi bilioni 12 za bajeti iliyopita? Cha ajabu Dodoma – Iringa ni Shilingi milioni 20 hivi, zinafanya kazi gani? Hata nyumba ya vyumba viwili haijengi, sembuse barabara! Tunaomba kujuua bajeti ya mwaka jana barabara ya Dodoma – Iringa ilipangiwa Shilingi milioni 574 sasa badala ya kwenda mbele tunarudi nyuma, tunarudi kinyume nyume, sijawahi kuona. Naona kwa mara ya kwanza na nasikia kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kwamba barabara hii itakapotengenezwa, wenzetu wanaotoka Ruvuma kule Peramiho wakitaka kwenda Arusha hawawezi kuzunguka Chalinze, wanaotoka Mbeya hawawezi kuzunguka Chalinze, njia ya mkato ni Iringa, Dodoma, Babati kwenda Arusha. Wanaotoka Rukwa hawawezi kupita Chalinze na nauli itakuwa kiasi kidogo na wananchi watafaidika na uchumi wa Mikoa hiyo mitatu utapanda. (*Makofî*)

Lakini mtu kutoka Peramiho azunguke Chalinze, abiria kutoka Mbeya akitaka Arusha azungukie Chalinze, kutoka Rukwa azunguke Chalinze na wa Dodoma tuzunguke Chalinze. Hivi umuhimu kwa nchi yetu tunapangaje? Mimi naomba Wahandisi wa Wizara ya Miundombinu watuambie umuhimu ni kati ya Wilaya na Wilaya au kati ya Mikoa na Mikoa? Tangu bajeti iliyopita tulizungumza kwamba umuhimu uwepo kati ya Mikoa na Mikoa na wala siyo Wilaya na Wilaya. Lakini bajeti iliyolekwa mwaka huu inatshangaza. Inanishangaza! Mheshimiwa John Lwanji pale kataka kulia. Mwanaume akilia machozi yanaingia tumboni, mwanamke akilia, machozi yanatiririka.

Naomba kilio cha wananchi wa Dodoma kisikike sasa. Mheshimiwa Zabein amelia pale, na mimi naendelea kulia nikiungana na Mheshimiwa Zabein na Wabunge wenzangu wa Mikoa yote waliozungumza kwamba barabara hii umuhimu wake uonekane sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwamba naomba kabla sijaunga mkono hoja, basi nipate maelezo. Kama hakuna muhisani, *UDOM* tumejenga kwa pesa za ndani, kuna barabara nyingi tulizojenga kwa pesa za ndani. Nimeona kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, kuna barabara nyingi tunajenga kwa pesa za ndani. Hii barabara inashindikana kitu gani? Tuambiwe kinachoshindikana ili tuwaeleze wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu bajeti iliyopita, tulipitia kwa kujidai kwenye maeneo yetu kwamba tunajengewa barabara ya lami sasa, kwenda Arusha itakuwa masaa mawili kutoka Dodoma, mpaka Minjingu, baada ya saa moja uko Arusha; baada ya masaa matatu unafika Arusha. Lakini sasa, kwenye bajeti iliyosomwa, hakuna pesa zilizotengwa. Shilingi bilioni 12 hazikufanya kazi, Shilingi bilioni tano zitafanya kazi gani? Tunaomba, tunakusihî Mheshimiwa Waziri, hebu lifikirie hilo, wananchi wa Mikoa hii mitatu wapate majibu. Wala sio Mikoa hii mitatu tu, hata wa Kusini wanalia kwa sababu ya barabara hiyo, wenzetu wa mashariki huko wanalia kwa sababu ya barabara hiyo uone ilivyo muhimu barabara ninayo izungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze sasa pia kuhusu reli ya Tanzania. Mwekezaji *RATES*. Alipoingia mkataba na Serikali, tuliambiwa kwamba huyu mtu ana uwezo wa kuendesha Reli ya Tanzania. Lakini cha ajabu, mabehewa ni yale yale. Tena siku hizi, viti vyâ kwenye mabehewa yamechanika zaidi, unaweza ukatoka na mende ukikaa kwenye behewa la *TRC*. Unaweza ukatoka na mende na chawa kwa sababu, *sponji* zile zimechakaa, mabehewa ni yale yale, vichwa vyâ treni ni vile vile, reli ni ile ile na walifanya *restructuring* kwamba wanataka kufanya vitu vizuri katika njia hiyo ya reli.

Lakini wananchi wetu wanataabika kama nini! Mizigo haiendi, wahindi wanakula hela, hakuna kinachoendelea. Kama hawawezi si wanyang'anywe! Kwani wako wangapi? Mbona wakati tulipoendesha Watanzania wenyewe tulikuwa tunaweza? Leo imekuaje? Kama yule hawezi kazi, kama Kampuni ya *RITES* hawawezi kazi wafukuzwe. Wawekezaji wako wengi, tena wako wengi kweli wanaoweza kufanya hiyo kazi. Wananchi wetu wamechoka kulala kwenye vitanda vyenye chawa, mende na huduma mbovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani Watanzania walipokuwa wanaendesha treni, treni ili kuwa inakwenda kila siku. Sasa inakwenda mara tatu, mara nne kwa juma. Tena kwa kusuasua. Naomba Serikali ione namna; *either* kumtoa huyo mwekezaji, au *management* kubadilishwa. La sivyo, wananchi wetu wataendelea kuumia. Nina taarifa ambazo nimezipata kwamba Serikali ina matatizo makubwa na makandarasi kama saba hivi ambao walifukuzwa kazi katika maeneo yao ya kazi pasipo kufuatwa utaratibu.

Kama mkandarasi hafuati utaratibu, afukuzwe. Lakini taratibu zifuatwe. Kuna *site meeting*, kuna barua za onyo, kuna mambo mengi ambayo yanatumika katika kumtoa mkandarasi katika eneo lake la kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, kuna wakandarasi ambao wamefukuzwa kazi, pasipo kufuata utaratibu. Ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu alichunguze hili na alete taarifa kwenye Bunge lako Tukufu kutuambia kwamba ni watu wa Wizara yake waliozembea ndio maana Serikali imeshitakiwa? Kwa sababu hawa wakandarasi saba wameishitaki Serikali na mwengine jina lake ni *Prismo Badr Joint Venture* alifukuzwa kazi, alikuwa anajenga barabara ya Marangu - Tarakea. Ametushtaki huyu Bwana Mahakama ya Kimataifa kule Paris na ameamriwa arudishwe kazini. Sasa atarudishwaje wakati *contractor* mwengine ameshakuwa kwenye *site*? Sasa kuna pesa tunazotakiwa kulipa pale, kuna mabilioni ya walipakodi zinatakiwa zilipwe na Serikali, tutazitoa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni uzembe wa mtu mmoja au wawili au watatu, Serikali itueleze kwamba hawa watu wamechukuliwa hatua gani za kisheria. Haya mabilioni ya pesa ni za dawa za hospitali, ni za akina mama wajawazito, ni za shule au za madarasa? Nitaunga mkono baada ya maelezo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Felister Bura. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Hassan Kigwalilo na Mheshimiwa Peter Serukamba ajiandae.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Miundombinu - Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri, pia nampongeza Naibu Waziri – Mheshimiwa Ezekiah Chibulunje kwa kazi nzuri na pia kwa hotuba hii ambayo ni nzuri na mimi naiunga mkono mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuunga mkono, sio kwamba mimi nafaidika sana na hiyo hotuba, sio kweli, isipokuwa kuna kasoro chungu nzima ambazo nitazifuatilia kwa karibu. Lakini kwa kuunga mkono, mnawenza kunifirkiria vizuri zaidi. Kabla suaunga mkono au kabla sijachangia vizuri., naomba kutoa rambirambi kwa aliyekuwa Kaimu Mufti na Sheik Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Marehemu Suleiman Gorogosi kilichotokea hivi karibuni Mkoa wa Lindi kwa ajali ya gari. Pia naomba kutoa rambirambi kwa kifo cha Prof. Haroub Othman ambaye alikuwa Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Pia ningependa kutoa rambirambi kwa aliyekuwa Katibu wa Chama Wilaya ya Nachingwea - Marehemu Cheyo ambaye ni mwenyeji wa Liwale, amefariki hivi karibuni na alifia Liwale. Baada ya rambirambi hizo, naomba kuchangia hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuendeleza ujenzi wa barabara ya kutoka daraja la Mkapa hadi Somanga. Eneo hilo kusema ukweli ambalo linapata kilomita kama 60, ilikuwa ni kikwazo kikubwa sana kwa wasafiri waendao Mikoa ya Lindi na Mtwara na hasa wakati wa usiku. Ni tishio kwa usalama kwa vile majambazi walikuwa wanavizia sana kuhatarisha maisha ya wasafiri. Pia naihimiza Serikali ifuutilie kwa karibu, iweze kukamilika haraka iwezekanavyo ili tuweze kutumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa barabara ya Lindi, pia kunaihitaji na kukamilika kwa mitandao mingine kutoka Nangurukuru kwenda Liwale. Kutoka Nangurukuru kwenda Liwale ni kilomita 231, ni barabara ambayo ni fupi sana na ndio changamoto kubwa kuwaletea maisha bora kwa kila mwanaliwale. Vinginevyo, barabara inayotumika, kama wakati wa masika ni ile ya kuzunguka hadi Lindi. Wafanyabiashara inawagharimu sana, hatimaye wananchi wa Liwale wanagharamika kwa maisha yao. Sio hivyo tu, hata baadhi ya wafanyakazi huwa wanaogopa kwenda Liwale kwa kuhofia kwamba watasafiri kwa taabu. Lakini hadi sasa, naishukuru Serikali kwamba kwa kipindi hiki cha kiangazi unaweza kusafiri kwa muda wa masaa saba kutoka Dar es Salaam kwa kupitia Nangurukuru hadi Liwale na kutoka Liwale kwenda Nachingwea kwa kiwango hicho hicho cha changarawe inaendelea vizuri. Lakini kwa kawaida, kiwango cha changarawe ni kusema Serikali kila baada ya muda iwe na mikakati mingine ya kuendelea kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa masika, barabara hii haipitiki na kwa bahati barabara hiyo pia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Katika Mikutano yetu ya RCC, tumekuwa tunakutana mara nyingi sana na mara nyingi tunaizungumzia barabara hiyo ambayo inasaidia sana hasa kwa upande wa Serikali kwa kuwa kutoka Kilwa kwenda Liwale ni kilomita 231, lakini kama atapaswa Mkuu wa Mkoa atoke Kilwa kwenda Liwale, azunguke mpaka Lindi, kwa hiyo, ni kusema itaigharimu sana Serikali sio kwa ziara za Mkuu wa Mkoa tu, lakini hasa kwa shughuli za Serikali. Hiyo ni gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo njia kusema kweli inatumika sana wakati wa Mwenge, lakini tangu umepita Mwenge, ningetegemea kwamba baada ya hapo, itakuwa imeshajifungua moja kwa moja kama vile alivyoahidi Mheshimiwa Rais kwamba itatumika kipindi chote cha mwaka, lakini hivi sasa tunatumia wakati wa kiangazi peke

yake. Naomba sehemu zile korofi, za barabara hiyo ziimarishwe. Kwa mfano Mlima Tembo sasa hivi wametia lami, nashukuru; lakini pia kuna maeneo kadha, kwa mfano sehemu za Kimamabi, sehemu za Namajani, Miguruwe karibu na Zinga. Maeneo haya yote yakiweza kuboreka, kwa vyovoyote vile tutakuwa na uwezo wa kutumia barabara hiyo kipindi chote cha mwaka kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais na sisi tunaifutilia kwa karibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada ambazo tunafanya, mbali na kuzungumzia katika *RCC* zetu kuhusu barabara hiyo, pia mimi mwenyewe na Mkuu wangu wa Mkoa, Mheshimiwa Sadiki Meck Sadiki, tumekwenda ofisini kwa Mheshimiwa Waziri kuelezea umuhimu wa barabara hiyo na kwamba mwaka jana zilitengwa Shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya barabara hiyo kurekebisha zile sehemu korofi. Nasikitika kusema kwamba mpaka hivi sasa tunawabembeleza wakandarasi waendelee kufanya kazi na hawajaanza kulipwa kitu chochote. Sasa matokea ni kwamba hata zile sehemu korofi, ambazo wangeweza kutengeneza vizuri kwa kuwa hawajapewa kitu, kwa vyovoyote vile hiyo kazi itakuwa ni hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa sielewi kama Serikali haiwezi kusaidia Shilingi bilioni 1.4 kupatikana. Sasa nashanga hawa wanaolilia lami, wanalilia lami ya nini? Mimi ningeona basi Serikali kitu kama hicho Shilingi bilioni 1.4 watoe na nyingine Shilingi bilioni 1.4 ili mradi sisi tunaopata barabara ya kokoto, tuweze kutumia kipindi chote cha mwaka. Sisemi kwamba wananchi wa Liwale hatutaki lami, hatuna makuu wananchi wa Liwale. Kama vile Mbunge wao, mtapoweza kutuwekea lami *Alhamdullilah* tutashukuru Mungu. Lakini umuhimu wa lami upo pale pale. Kwa hiyo, ningeomba tu sehemu zile korofi mngeona uwezekano wa kuweka lami ili barabara hii kweli iweze kutumika kipindi hicho chote cha mwaka. Katika kufanya hivyo, yale maisha bora kwa kila mwananchi, basi yatafika mpaka Liwale. Vinginevyo ni maelezo ambayo wananchi wa Liwale yatakuwa hayana maana kwao. Kwa kuwa ughali wa maisha unategemeana na usafiri na usafiri ukiwa mrefu, kwa vyovoyote vile maisha yanakuwa magumu kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja kwamba tuliwahi kwenda na Mkuu wangu wa Mkoa, Mheshimiwa Saddiq, kwa Waziri, lakini nasikitika mpaka hii leo nikiangalia katika ile kabrasha siaona maelezo yoyote ya kuonyesha kwamba hizo pesa zitapatikana au kuna mikakati ya aina fulani. Ninachoomba, tupate pesa za maendeleo ya ujenzi wa barabara hiyo, nitashukuru sana kama Waziri na Serikali kwa ujumla wataliona hilo na kuweza kutukomboa wananchi wa Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka Liwale kwenda Nachingwea, barabara inakwenda vizuri, kasoro sehemu chache chache, lakini hata hivyo namshukuru sana au nawashukuru sana *TANROAD* Mkoa wa Lindi, ambao wanajitahidi kwa juhudhi zote pamoja na kwamba upatikanaji wake wa pesa ni mgumu mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa mwaka 2007/2008, Serikali iliruhusu barabara kutoka Liwale kuititia kijiji cha Ndapata, kuititia pia *Selous* hadi kufika Ulanga Mashariki ifufuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi katika *RCC* tumezungumzia suala hilo na hadi hii leo bado hatujaona upande wa Serikali ina fanya nini. Ningeshauri na ningehimiza kwamba tafadhali Serikali ione umuhimu wa barabara hiyo ambayo hapo zamani ilikuwepo na kwamba wananchi wa pande zote mbili wa Ulanga na Liwale, sehemu Ndapata ni wamoja na kwamba tendo la kuzuia barabara hii kutokana na wanyama wa *Selous* amba baadaye mwaka 2007/2008 lilionekana lifutwe, basi naomba sasa mikakati ya dhati ichukuliwe kwa kushirikisha Wizara zinazohusika, Miundombinu na Maliasili. Ni kitu ambacho mchakato wake ulishaanza, lakini baada ya mabadiliko hapa katikati naona haya mabadiliko yanakuwa yakitokea kwenye uongozi, basi yatokee kwenye makaratasi pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba taratibu hizi za kiserikali zisiendelee. Kama itatokea katika uongozi kuna mabadiliko, basi naomba kwenye Serikali mambo ya makaratasi yabakie vilevile ili tuweze kufuatilia kwa karibu. Namshukuru sana Mheshimiwa Chibulunje, Naibu Waziri kwa kutembelea Liwale na kuweza kukagua barabara ya Nangurukuru kuja Liwale, pamoja na mimi mwenyewe. Palikuwa na mahali fulani karibu tupate ajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote baada ya kuyaona, alivyoweza kuhimiza na kusema kwamba tutaendelea kupata pesa, naomba tuendele kupata pesa kwa ajili ya maendeleo ya barabara ya Nangurukuru kwenda Liwale. Pia kutoka Liwale kwenda Nachingwea, isirudie Mbwemkuru ifike mpaka Nachingwea. Itamrahisishia hata Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba au Katiba na Sheria kuititia Mahakama ya Liwale aje mpaka Nachingwea. Sisi ni wanandugu, sasa kama tunatengana kwa barabara, tutapatana kwa nini? Inashangaza! Hapa karibuni, tuseme kipindi kilichopita mwaka jana, tuliamiwi palikuwa na pesa nyingi sana zaidi ya Shilingi bilioni ngapi sijui zilikuwa zinalipwa kwenye *Richmond*. Sasa fedha hizi hazilipwi tena, kwanini zisifanye kazi ya kutengeneza barabara, kwa maana ya hii barabara ya Nangurukuru kwenda Liwale? Naomba tena kuunga mkono hoja. *Inshaallah*.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu ajiandae.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Miundombinu ni jambo la msingi sana kwa maendeleo ya nchi yoyote duniani. Mimi leo nimetafakari sana, nimeamua kufikiri kidogo kwamba nadhani umefika wakati, mazoea tuyache kidogo. Ningesema mwaka huu tuuite mwaka wa maendeleo. Tukiamua kuuita mwaka wa maendeleo, tunaweza. Nimeangalia vitabu vyetu vya bajeti, mwaka huu *OC* ni *three trillion* matumizi ya kawaida. Nikasema tukiamua na Mwalimu alisema tufunge mkanda jamani, tukakaa miezi 18 tumefunga mikanda. Kupanga ni kuchagua, kwenye trilioni tatu hizi, chukua asilimia 15 tu, asilimia 85 waachie waendeshe Serikali, asilimia 15 tufanye maendeleo. Ukikata asilimia 15, unapata Shilingi bilioni 450. Hapa ndani kelele zisingekuwepo? Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuiambie *this time* Serikali ipunguze asilimia 15 kwenye *OC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shida gani watu kujinyima kwa maendeleo yetu? Linawezekana. Ni rahisi tu. Barabara zetu hizi, sijui reli, hatuhitaji kuwasubiri *ADB*, hatuhitaji kumsubiri nani, tukijinyima tutafanya wenyewe. Lakini haiwezekani tulete maendeleo wakati tunakula kuku, haiwezekani! Haiko nchi duniani iliendelea huku inakula kuku. Haiko, mimi sijui! Soma historia, Waingereza walivyopata maendeleo yao. Wakati wa maendeleo ya viwanda, waliuana, walifanya kazi, walijinyima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya vita kuu ya pili ya dunia, kuna Rais aliyejuka wa Marekani aliwaambia kazi ya kwanza, najenga barabara, akachukua wafungwa akaanza kujenga barabara. Wakajinyima, sisi tunataka tuendelee huku tunakula kuku, tunabadilisha magari kila baada ya mwaka mmoja, haiwezekani! Kwa hiyo, mimi nikasema, kwanza leo naomba tukubaliane, mnikubalie Waheshimiwa Wabunge, tuiombe Serikali ipunguze asilimia 15 ziende kwenye *infrastructure*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo la kutafuta fedha, leo sisi kama Serikali tunazo *share ZAIN*, kampuni ya simu, asilimia 40. Tuzipeleke kwenye soko la hisa tutapata pesa sio chini ya Shilingi bilioni 300, soko la hisa litakuwa, limeendelea, tutakuwa tumewawezesha wananchi wetu na tutapata pesa za kupeleka kwenye *infrastructure*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo *share BP* karibu asilimia 50, tunazo *share Kilombero Sugar*, tunazo *share NBC*, tunazo share zilizobaki *NMB*. Kupanga ni kuchagua. Tutamalizana humu nilete kwangu, nilete kwangu, kwasababu tunagawania umasikini. Hizi kero zote ni za umasikini tu hizi, *nothing else*. Tunamalizana kwa sababu hatutaki kufikiri, nawaomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha waje na mkakata wa kuiendeleza hii nchi. Hatuwezi kwenda tuondoke kwenye *box* hili. Nilitaka nianze kwa kusema niwaonyeshe Serikali ziko pesa. Tuzitafute hela hizo tufanye *infrastructure*. *Infrasructure* zenyewe zinafa tuendelee, tujenge barabara, *infrastructure* za *irrigation*, tufanye umeme, Bandari na Reli nchi imetoka hii. *Simple!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tutakaa tunasema kwangu hujafanya, wewe mtu mbaya, tutawamaliza bure yarabi hawa, hakuna pesa. Tutafute pesa, nchi hii ina pesa. Baada ya kusema hayo, nimesema tukipata pesa, tutafanya kazi ya reli maana hali ya reli ni mbaya sana. Tuweke pesa, tusicubiri mpaka *World Bank* waje, haiwezekani.

Lakini pia suala la Bandari, nchi ya Singapore imeendelea kwa sababu ya Bandari. Sisi tunazo Bandari za maziwa, na Bandari karibia tatu za bahari ya Hindi. Mungu atupe nini? *What do we want from God?* Tunamtakia nini tena huyu Mungu kwa kazi aliyotufanya hii? *Our geographical position* inatu-favor kuendelea zaidi. Tumefanya vizuri, lakini tunaweza tukapiga hatua kubwa zaidi kuliko tunayopiga sasa. Leo tunaanza kupambana, tumwondoe *TICTS*, hivi najiuliza, ukimwondoa *TICTS*, huyo anayekuja anakuja na maziwa na asali? Na anakuja lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, gazeti la *Daily News*, limeandika juzi, *TICTS* wameweza *facts* mambo waliofanya. Mimi naomba leo Serikali ije na majawabu ya *facts* walizoziweka *TICTS* kwenye gazeti la *Daily News*. Naomba Mheshimiwa Waziri atupe majibu. Simple! Tuache kelele hapa. Hatuwezi kuendelea bila *investors*, tukubaliane tu.

Nilitaka niongee suala la ATC. Huwezi ku- *run Airline* kwa Shilingi bilioni moja. *I mean tukubaliane na hayuko anayeweza kuja akikuta wewe mwenyewe hauko serious.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tatizo ni *management, fire them*, kama ni Serikali wekeni pesa tufanye kazi. Lakini hivi tutapigiana kelele, hatuwezi kwenda. Nilitaka niongelee suala la barabara, nimeanza kueleza tunavyoweza kupata pesa. Lakini zipo barabara za muhimu. Nataka mimi *specifically* niongelee barabara hii ya kutoka Manyoni kwenda Kigoma. Wenzangu wamesema, jamani Wazungu wanasema *time is money*. Tumetangaza kazi ya kilometra 89 ya kutoka Manyoni, Itigi mpaka huko Chaya, *ma-contractor* wameleta bili zao, unawaambia waondoe. Unachotaka tukaanzie Tabora ili uwafurahishe watu wa Tabora! Mnawadanganya watu wa Tabora, hamtaki kuwafurahisha. Kwa sababu, ukianza upya maana yake unapoteza miezi saba mingine. Kwa hiyo, watu wa Tabora hawa, barabara hiyo wataiona mwaka kesho watakapotoka kwenye uchaguzi ambapo walioshindwa wameshindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Why do we want to loose time?* Tunapoteza miezi sita kuandaa barabara hii ya Manyoni, Itigi mpaka Chaya. Lakini, hiyo miezi sita mnataka leo haina maana? Tuanze upya. Nani kasema? Nami nasema lazima tuendelee na mpango uliyokuwepo, tunajua tunatafuta mtu wa kufanya *design*, kwa hiyo, kilichobaki tuendelee, lakini wakati kuna Tabora, kuna barabara ya Tabora mpaka Kaliuwa kilometra 126. *Designs* ziko tayari. Nawaombeni tuitangaze barabara hii.

Basi mimi ndio ninachowaomba tu, pesa za kutoka Kidawe kuja huku, ziko tayari, tutangaze barabara hii, twende. Kwa kweli tunawashukuru kwa kazi hiyo nzuri, lakini tunajenga barabara, Rais Mheshimiwa Kikwete juzi amekuja na *plan* ya kuokoa uchumi wetu. Moja ya area ni kwenye barabara. Nawaombeni sana tukubaliane hapa ndani, barabara hizi nydingi zimejengwa na Wachina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *so what are we doing? We are transferring our funds to the Chinese.* Hayabaki kwenye *economy* yetu. Tukubaliane barabara yenye *project* zaidi ya bilioni 50 kama unataka kujenga wewe mtu wa nje, uwe na *local shareholder* ili hela hii irudi. *Trickle down effect* kwenye *economy*, ni kubwa! *This is simple economics.* Haihitaji *degree* hata kidogo! Kwa hiyo, nawaomba wenzetu watusaidie kwenye hili. Lakini baada ya kusema hilo la *local shareholder*, tuwasaidie, mimi leo kwa bahati nzuri nimewahi kufanya kazi *TANROADS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka leo niliongelee suala la *TANROADS*. Liko hapa, lina babaishwa babaishwa hivi, hawataki kuelewana vizuri. Utaratibu wakati imeanzishwa ile *agency*, wengine tulikuwepo. Ilikuwa nafasi ya *CEO* lazima itangazwe, apatikane kwa ushindani, nafasi za *ma-director* lazima zitangazwe wapatikane kwa ushindani, nafasi za *ma-manager* lazima zitangazwe wapatikane kwa ushindani. Mimi nasema utaratibu ule ni mzuri na uendelee. Faida yake ni moja tu, kwamba hawa watu wanakuwa *serious* kwenye kazi kwa sababu hana hakika baada ya miaka mitatu kama atarudi, kwa hiyo, anakuwa *serious* kwenye kufanya kazi. Cha msingi, utaratibu huu uwe wa wazi na tuwa-*engage* wafanyakazi nao walielewe hili kwamba jamani eeh,

tunachokileta hapa ni kwa faida yenu na faida ya mikataba nitawaambia dunia ya leo inavyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi kumetokea *recession* Marekani, *GM* ameanguka, watu wameondolewa kazini. Lakini wangkuwa wameajiriwa *Permanent Pensional*, wasingewatoa ng'o. Leo hii tunayo *ATC* pale, ina ndege mbili, wafanyakazi lukuki, huwezi kuwafukuza, inabidi uwalipe kwa sababu ni *Permanent Pensionable*. Wangkuwa kwenye *contract*, kesho tungewaondoa. Hii ndiyo dunia tunayokwenda sasa jamani! *We must change! Change is necessary, of course.* Mabadiliko yanositua, lakini mimi ninachosema, wale wanaotaka kusimamia mabadiliko *waw-engage* watu wayaelewe yale mabadiliko na mtu akikuangalia kweli akuone kweli unayo nia ya mabadiliko ya kweli. *I mean your heart wants to deliver the best*, tutakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana wenzetu, watusaidie, hili litatusaidia sana tunakokwenda huko tunakokwenda. Kwa kweli nimekaa kwenye *organisation*, leo tunatamba barabara zimejengwa, sababu wale watu wamefanya kazi nzuri, kwa hiyo tunapotaka kuwaletea mabadiliko haya ili waweze kupata *motivation* vitu gani, lazima sasa nao tuwapishe kwenye hii *process*. Lakini *process* ni nzuri, isimamiwe vizuri, isimamiwe kwa haki tutawasaidia watu hawa. Kwa kweli na kiongozi wa *TANROADS* ambaye najua analisimamia hili, cha msingi alisimamie kwa ukweli, kwa haki na uwazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala hili la mikataba. Wakandarasi wanafukuzwa kazi na rafiki zangu wa magazeti nao wameingia. Wamekuwa sehemu ya kulalamika kwa hawa waliofukuzwa. Jamani tukubaliane hapa ndani. Sisi tunajinyima, tunatafuta pesa ili tujenge barabara. Unampa mtu *contract* ya barabara anafika miezi mitatu amenza kazi, haendelei, haijengwi, wananchi wanapiga kelele, wewe unampa pesa, unafanya nini? *Ume-breach contract* nakufukuza tu. Wakijua kwamba hawa watu wako *serious*, hawa watu hawatatushazea. Tumepata matatizo kwenye barabara za kutoka Mtwara zile za *special project* mpaka huku Singida. Matatizo yale hatujifunzi tu? Hawa watu wanatufikisha kubaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema huyu anayefanya kazi hii, tumsaidie kiongozi wa *TANROADS*, wanaofanya mchezo, tuwfukuze ili wajue Watanzania hawa wapo *serious* na pesa zao na magazeti tuache. Lakini ili tusipate matatizo, watu wa *AG* wamsaidie mtu wa *TANROAD*, Wizara imsaidie na tusomeshe watu wa *arbitration* ili tujue kwamba una uhakika unapotaka kufuta mkataba, vitu vyote umefuata ili wewe upo kwenye *safe side*. Tutakwenda watu hawa watakuwa *serious*. Lakini bila hivi watakuwa wanatuchazea, leo tunagombana tatizo la Dodoma – Manyoni, toka mwaka 2001, barabara ya kilomita 100 mpaka leo inajengwa. Maana yake nini? Ameingia mkandarasi katikati akasema hela mlizonipa ni ndogo, sitaki. Tumevurugana wee, nikamwambia haya anza tena. Amekwenda mara akasema sitaki. Anafukuzwa, Waswahili wengine wanaanza kupiga kelele huko, wanaandika magazetini. Jamani tunahitaji barabara sisi. Cha msingi tu-review Sheria zetu, tu-review zile *tender document* zetu, ile *bill document* iangaliwe vizuri, watu wa *AG* wasaidie watu wa *TANROADS* tuliangalie vizuri ili mikataba hii iwe na maana.

La mwisho, watu hapa wlipiga kelele, kiongozi wa *TANROADS* analipwa hela nyingi. Mimi nimekaa kwenye ile *agency*. Wale waliopita wote, walikuwa wanalipwa hivyo hivyo. Hivi akilipa Mtanzania kuna dhambi gani? Wakati analipwa Mgħana tuliona sawa, wala hamna aliyepiga kelele humu ndani. Lakini pia suala la mshahara nime-negotiate, wameniambia nakupa hii kazi, nasema sawa. Hebu tuwaache Watendaji wafanye kazi, sisi tu-demand wao ku-deliver ndiyo jukumu tulilonalo. Tukitaka na sisi tuwe sehemu ya kuamua mfukuze yule muache yule, tumeħaribu, tutawavuruga watu hawa hawatatupeleka popote. Nawaombeni sana sisi tu-demand delivery.

Mwisho Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana barabara ya kutoka Tabora kwenda Kaliua kilometra 126 viwango viwepo Wiziri itangaze barabara hii. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Peter Serukamba. Waheshimiwa Wabunge sasa nitamwita Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi kuzungumza leo hii. Awali ya yote, nashindwa kuelewa nilikuwa mtu wa kwanza kuingia katika *hall* hili leo asubuhi na nilikuwa mtu wa kwanza kuomba kuchangia leo na karatasi yangu ilikuwa ya kwanza kuingia pale kwenye Meza, lakini nimekuwa mtu wa 14, kulikoni? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba basi niende moja kwa moja na kwa kuwa sijajua kama nitaweza kupata nafasi nyingine, napenda kuwapongeza wananchi wa Bukene. Kwanza kabisa, wananipta moyo kabisa na mimi najisikia kwa sababu katika Mkoa wa Tabora Majimbo tisa Jimbo la Bukene lilikuwa la pili kwa wingi wa kura na kwa Rais na kwa Mbunge na mpaka sasa hivi tunaendelea vizuri, tunashirikiana nao vizuri na sauti ya Bukene inaendelea kuzungumza. Nawapongeza, ninawashukuru na mimi nawaambia sauti ya Bukene nilioiomba itafanya kazi kama nilivyoomba na sitaogopa na wala sitashindwa kuwasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea zaidi tena, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa mambo yote aliyyofanya, yanaonekana katika miaka minne hii na kwa kifupi tu juzi tumeangalia maji ya Ziwa Victoria yanakwenda Kahama, hayo ni maendeleo na ni hatua nzuri kwa Mheshimiwa Rais wetu kwamba anasema na kutenda pamoja na Watendaji wake. Hongera sana. Vile vile, tumeweka juzi juzi hapa tumeona maboti yakienda *Lake Tanganyika* na *Lake Nyasa*, hizo ni hatua nzuri kwa Awamu ya Nne, kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Rais na Mawaziri wanaohusika kwa kazi nzuri wanayoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile siwezi kusahau katika Awamu hii ya Nne nilipokuwa nachukua Jimbo la Bukene kulikuwa na *Secondary School* mbili tu, lakini sasa tuna *Secondary School* Kata zote na tuna *Form Three* tunakwenda kwenye *Form Four* na *Secondary School* nimechangia chumba kimoja cha Sekondari kwa hela yangu mwenyewe, wala si *CDF*. Kwa hiyo, nawapongeza wananchi kwa sababu niliwhamasisha na wenyewe wakaanza kuchangia tukaenda na sasa hivi tuna *Secondary*

*School* kila Kata, tuna *Secondary School* tunakwenda kwenye *Form Three* na wengine kwenye *Form Four* na wengine kwenye *Hostel*. Nawapongeza pia wale waliocheza Timu za Mpira, juzi nilipata timu 116 kutoka vitongojini mpaka vijihi kuja kwenye Kata mpaka kwenye Jimbo kushindania kombe linaloitwa *Teddy Kasella-Bantu Cup*, namshukuru aliyenipa kombe hilo na nawashukuru waliofanya mashindano hayo na nawapongeza waendelee hivyo ili tuhamasishe michezo kwani michezo ni ajira, michezo ni afya, michezo ni furaha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naingia kwenye ajenda yenewe. Ninaanza kwanza nyumbani kwenye Jimbo, maana yake wanasema Waingereza: “*Charity starts at home.*” Kuna barabara ambayo inapita kwangu, barabara ambayo inatoka Dar es Salaam kupitia Morogoro, Dodoma, Singida, Nzega ambayo ni *T3 (Trunk Road Three)*. Barabara hii ni ya Taifa inakwenda kutokea Kagongwa kwenye Wilaya ya Kahama Mkoa wa Shinyanga. Katika kuangalia hapa nimeona barabara hii imeshushwa gredi imekuwa ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikitika kusikia kwamba barabara hii inashushwa gredi na ndiyo hayo hayo nazungumza kama alivyosema Mheshimiwa Chegeni, unakuta barabara yote inakuja na malori yenyе mizigo mikubwa yanayotoka Burundi yanatoka kule kwenye *Trunk Road Three* mpaka yanafika Kagongwa, yakifika Kagongwa yanapoingia kwenye Jimbo langu yaanza kupita kwenye vumbi. Kwa hiyo, yanaharibu zaidi zile barabara kwa sababu zile barabara haziwezi kubeba uzito wa mzigoo unaotoka Burundi au unaokwenda Burundi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kisehemu chenyewe ninachozungumzia ni kilometa 54.5 kwa upande wa kwangu inatoka Nzega, Itobo, Bukooba. Halafu kutoka pale ni kilometa 11 kufika Kagongwa ambayo ni Kahama ambayo ni Shinyanga Mkoa. Sasa kwa ujumla wake ni kilometa 66 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishaandika barua kwa Waziri na nikamkuta hayuko nikamkabidhi Mheshimiwa Naibu Waziri na niliamini watanisaidia kwa sababu ni kasehemu kadogo sana kanakoleta sheshe pale. Lakini leo kwa mshangao ni kwamba kametolewa kameshushwa gredi. Lakini bado kama walivyosema wenzangu Wanyamwezi na Wasukuma hawa wawili ni watani wetu. Kwa hiyo, naomba basi mtafakari, mtafute jungu kuu halikosi ukoko. Kwa hiyo, ule ukoko kidogo pale naomba utee ulete pesa utengeneze hako kasehemu ka-T3 kutoka *Nzega Round About* kupitia Itobo na kwenda mpaka Kagongwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa sehemu ya Itobo walishawekewa ‘X’ kwenye nyumba zao ili waweze kubomolewa. Kwa hiyo, ni kitu sio sahihi kuwarudisha tena nyuma, kuwaambia sasa iwe ni barabara ya Mkoa na ukiwaambia ni barabara ya Mkoa maana yake wanaweza hiyo barabara isiwe ya lami ikawa ya changarawe. Kwa hiyo, naomba iwe barabara ya Taifa kama ilivyokuwa kama wanavyosema Waswahili, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika barua yangu vile vile nilisema ukitoka Itobo kwenda Bukene ambayo ni Makao Makuu ya Jimbo ni kilometra 20, pale pana vumbi vile vile. Kwa hiyo, nilikuwa nawaomba muweke lami ili kuonyesha uwiano. Kwa sababu ikitokea ile barabara T3 iende Itobo iende Kagongwa halafu kutoka Itobo kwenda Bukene pawe vumbi haileti mantiki kufika Makao Makuu ya Jimbo. Kwa hiyo, naomba na yenye ingechukuliwa kama ka-*complimentary* ili kuweza ku-*cover* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutoka Bukene kwenda Mambali na kufika Tabora hiyo *in fact* ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na alisema ataweka kwa kiwango cha changarawe, hiyo sina tatizo ikae hapo kama ya Mkoa na iwekwe kwa kiwango cha changarawe kama ahadi ya Mheshimiwa Rais ilivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara nyingine ambayo wanasema kwa kweli tungekuwa tunaulizwa na kutoa mawazo ingetusaidia sana. Kuna barabara ambayo inatoka Tabora inakuja mpaka Mambali inapita huko kwenda Mwanza inaitwa *Old Mwanza Road* ambayo inapita Semembela ambako ndiyo kwenye mazao zaidi na watu wengi zaidi inakuja kutokea Chambo ile nayo ingewekwa iwe ya Mkoa kwa sababu pale ndiyo kwenye mazao na pale ndiyo kwenye watu.

(*Hapa kengele ya kwanza ililia*)

Eeeh, hiyo kengele ya kwanza?

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mmeni-*fix* nini? Basi wacha niende haraka haraka. Baada ya kusema hayo, naomba niende moja kwa moja katika suala la barabara ya Singida-Manyoni kwenda Igunga kale kasehemu pale hakajakwisha, ni kwa sababu ya kuacha *Contractor* tunawachagua bila ya umakini. Naomba tuwe makini katika kuwatafuta ma-*contractor*.

Kwa mfano, barabara ya kwenda Kilwa – Dar es Salaam ile tumepa *Contractor* anaitwa Kajima kwa kuwa na matumaini ya kuamini kwamba Kajima ni *Contractor* aliyetengeneza barabara nzuri pale *Salender Bridge* na alitengeneza barabara nzuri ile ya kwenda Jangwani. Lakini Kajima huyu siye Kajima yule aliyetengeneza *Salender Bridge*. Ame-*sub-contract* watu watengeneze madaraja na wengine watengeneze mifereji.

Kwa hiyo, barabara hiyo imekuwa sio bora. Kwa hiyo, tunaomba mnapoanza kutoa tenda muangalie watu ambao mnawapa tenda ili tusirudie kuvunja mikataba tulivyofanya kipande kile cha Singida-Manyoni kile ambacho kinatuvurugia tena ratiba, tunashindwa kumaliza kwa wakati.

Miaka miwili inakuwa miaka minne na hiyo inaharibu kusaidia wananchi kutumia barabara zao kwa uchumi. Naomba mnapotoa tenda muangalie, yule anayetoa tenda atoe tenda kweli, kama anashirikiana na *sub-contractors*, basi wawe bora kama alivyo yeche,

wasitumie majina ya wenzao au wasiwe kampuni pwangu kwa kifupi ili kazi zao ziwe bora, isiwe tunakwenda tunaharibu, tunavunja mikataba halafu tunakwenda kufanya kazi ambayo haitusaidii na inaendelea kuchelewesha kazi za maendeleo kwa sababu mnategemea kufanya miaka miwili mnafanya miaka minne.

Nitasema haraka haraka kuhusu suala la reli. Reli ya Dar es Salaam – Tabora mpaka Kigoma au Tabora – Mwanza yenyewe zamani ilitengenezwa na Mjerumani. Mimi ushauri wangu ningeomba Serikali imtafute Mjerumani, imwite ili aweze kufanya kazi hii na naamini kabisa Mjerumanu akiita kwa historia na kwa sababu watu wote tunajua tumepewa historia na mababu zetu kwamba Wajerumanu walikuwa wakali lakini vitu vyao vilikuwa imara zaidi, atafanya kazi hii kwa furaha kwa sababu ni *historical*, atatengeneza reli yetu vizuri na hivyo tutapunguza matatizo ya wasafiri wanaokwenda Kigoma na wanaokwenda *Bukene*, *I mean* wanaokwenda Mwanza kupitia Bukene na hapo tutaweza kupata usafiri kwa kuitisha mizigo yetu na ajali zitapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, basi ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu na nakushukuru kwa kutuachia dakika kama mbili kabla kengele haijagonga. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, sasa namwita Mheshimiwa Benito Malangalila, atafuatiwa na Mheshimiwa Elizabeth Batenga.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushuuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Miundombinu. Kabla ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha mpaka saa hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Miundombinu. Lakini kabla ya hapo, ningependa kutoa pole kwa familia ya Naibu Mufti, Shekh Gorogosi pomoja na Mhadhiri Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. Haroub Othman. Binafsi sina hakika kama nitaiunga mkono hotuba hii na ninazo sababu.

Lakini kabla sijafika kuzungumza kitu ambacho sitakiungia mkono hoja hii, ningependa nizungumze kidogo juu ya barabara ya Iringa-Dodoma. Mimi nilikuwa Mhandisi Msaidizi wa Taasisi moja ilikuwa inaitwa *TRM Trunk Road Maintenance*. Nakumbuka niliona ramani ya barabara ya Iringa-Dodoma ilichorwa mwaka 1964. Sasa toka mwaka 1964 mpaka leo bila shaka ni siku nyingi sana, sasa kama ramani ya barabara ilichorwa toka mwaka 1964 mpaka leo kuna upembuzi yakinifu na lugha nyingi sana toka mwaka 1964 upembuzi yakinifu haujawkisha mpaka leo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi juzi nilikuwa natoka Iringa nikaja na barabara hii. Tulivyofika kwenye zile kona na Nyang'olo kukawa kuna lori moja limedondoka mle, tumekaa pale masaa matano, ikabidi tugeuze kutoka pale tukarudi kulala Mafinga. Kesho yake ikabidi tutoke Mafinga tupite Morogoro tukafika hapa Dodoma. Tazama ni adha gani ambayo wananchi wa Iringa wanapata kuja Makao Makuu ya nchi yao Dodoma. Tazama sisi wananchi wa Mufindi tunazalisha mbao, ukitoka Mufindi kupeleka mbao Dar es Salaam gharama yake ni Sh. 1,400,000/=. Lakini ukitoka Mafinga kuleta mbao Dodoma ukipita hii njia ni Sh. 1,700,000/=. Ukitoka Mafinga kwenda Dar es Salaam

kilometra zake ni kama 600 hivi, ukitoka Mafinga kuja hapa Dodoma hazizidi sana kilomita 300, lakini gharama hii inazidi kwa sababu ya ubora wa barabara kutoka Iringa mpaka Dodoma. (*Makofi*)

Mimi binafsi huwa sipendi sana kusema kwa ukali na namwomba Mungu leo anipunguzie hasira. Kwa sababu gani? Wizara ya Miundombinu zamani ikiitwa Ujenzi, ilifanya mambo ya ajabu sana. Mheshimiwa Lwanji hapa anasema kuna mkandarasi ametafutwa kujenga barabara kutoka Manyoni mpaka Tabora huko, *tender documents* zimekwishatangazwa, mkandarasi anatafutwa, ghafla Wizara ya Miundombinu hii inabadilisha, barabara ikaanzie Tabora. Hivi toka lini mto unafuata njia? Lazima kuwe na *continuity of network of roads*. Mtu unatoka Dar es Salaam unafika Dodoma, unafika Manyoni barabara ya lamim ukitoka Manyoni unaendelea barabara ya lami mpaka Tabora. Ndiyo utaratibu wa barabara ulimwenguni kote na ndiyo ustaarabu unavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mzuri mimi ni Mhandisi, ila tu huwa sipendi kuitwa Eng. Malangalila, *no. I am a qualified Engineer from University of Dar es Salaam*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu ni rafiki yangu, Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, najua wewe ni mtu mpole sana, lakini upole huu kwa hakika hautakusaidia sana kama hutekelezi wajibu wako ipasavyo. Wabunge wote wanasema barabara ya Manyoni lazima ianzie Manyoni, Wabunge wote humu ndani sijaona hata mmoja hata Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu hapa hakusema, ye ye mtu wa Tabora lakini hakusema barabara hiyo ianzie Tabora irudi Manyoni. Sasa haya maamuzi yanatoka wapi? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije barabara za Jimbo langu la Mufindi Kusini. Naishukuru sana Serikali kwamba kuna pesa wametupa angalau kidogo kutoka pale Igowole kwenda Kasanga, kwenda Mtambula – Ipilimo - Ihawaga mpaka Nyigo. Naishukuru sana Serikali. Kwa nini naishukuru Serikali? Unajua Serikali huwa inasahau tu baadhi ya barabara zake? Unaweza kukuta baadhi ya barabara zimepotea tu kwenye vitabu. Zimepotelea wapi? Hujui. Zimekabidhiwa nani? Hujui. Zina maelezo gani? Hakuna. Sasa tunakwendaje? Ni dhahiri kwamba vitu kama hivi ndivyo vinavyoleta matatizo makubwa tena makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka juzi aliyekuwa Waziri wa Wizara ya Miundombinu alikuwa Mheshimiwa Chenge. Kuna barabara moja inaitwa Nyigo-Mgololo. Barabara hii mimi nilikuwa *Technician* niliyeanza kusema, nilivyoangalia barabara ya Iringa-Dodoma. Barabara hii mimi ndiye nilikuwa nimu-*assign* aisimamie kutoka *TRM*, *TRM* ilikuwa ni Idara ya Serikali ya Wizara ya Ujenzi ambayo leo ni Wizara ya Miundobinu. Lakini wamekuja kuisahausahau tu hivi hivi tu kienyeji tu. Niliwaambia mwaka juzi kwamba mimi nimechoka, nawakabidhi barabara yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka Mheshimiwa Spika Sita alisema: “Mheshimiwa Chenge hii barabara Mheshimiwa Malangalila amewakabidhi” Mimi nikaamini kabisa kwamba barabara hii itachukuliwa na Wizara ya Miundombinu, mwaka jana. Barabara hii nadhani Mheshimiwa Waziri Kawambwa alikuwa Waziri. Nilirudia

maneno yale yale kwamba barabara hii mliipasua, mlikuwa mnaiendesha ninyi. Barabara inaanzia Mufindi inaingia Njombe, Mufindi-Njombe, Mufindi-Njombe *and then* inaishia Mufindi katika kiwanda kikubwa kabisa cha Karatasi cha MTM zamani ikiitwa *SPM Southern Paper Mills* sasa hivi kimepewa heshima kinaitwa *Mufindi Paper Mills, the largest paper mills in Africa*. Kiwanda kikubwa kabisa cha karatasi katika Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa sana kwa nini Wizara hii haitaki kuichukua barabara yao. Nashangaa kweli kweli! Nilisema nimwombe Mungu ili nisikasirike. Lakini katika hili nakasirika mno! Kwa sababu Waheshimiwa Wabunge hapa wanasema wanaonewa, sisi tunaonewa sana. Tena tunaonewa mno! Hakuna hata sababu ya mimi kuendelea kuzungumza jambo hili mwaka hadi mwaka mpaka naota mvi na naota na upara kwa sababu ya barabara hii. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimechoka sana. Nimechoka, nilisema sina hakika kama nitaiunga mkono Wizara hii. Mwaka jana niliunga mkono kwa asilimia 70, kwa hakika kama hawasemi chochote mwaka huu nitaiunga kwa asilimia sifuri, kwa kutoa shilingi. Mimi sina kigugumizi katika hili. Wanatuonea, tena wanatuonea sana. Tazama kiwanda cha *MPM* kilitembelewa na mgeni kutoka Benki ya Dunia, Menejimenti wakasema bwana tunaomba utusaidie ututengenezee barabara hii iwe ya lami, wakasema mimi nawashangaa sana Serikali yenu. Mimi Benki ya Dunia siwezi kuzungumza na Halmashauri ya Wilaya, ninataka kuzungumza na Serikali, Serikali Kuu na Wizara ya Miudombinu, kama sasa Serikali yenyewe ya Miundombinu hawaitambui umuhimu wake, Benki ya Dunia tutaitambuaje? Mimi nilivyoambiwa maneno hayo kwa kweli nilikasirika sana kama ninavyokasirika sasa hivi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani nimekasirika kweli kweli, kwa sababu...

**MWENYEKITI:** Taratibu tu mkono wako usigonge kichwa cha Mheshimiwa Kaboyonga. (*Kicheko*)

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Wakati mmoja Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Anna Abdallah, wakati anatoa hotuba yake hapa Bungeni, alisema kwamba Wizara ya Ujenzi ilikuwa ina mpango wa kuhudumia barabara zote zinazokwenda katika mashamba makubwa, zinazokwenda katika viwanda vikubwa na barabara zote zinazokwenda katika hospitali kubwa hapa nchini. Sasa unapozungumzia viwanda vikubwa, kiwanda cha *MPM* ni moja kati ya viwanda vikubwa kabisa katika Tanzania na kwa maana hiyo ningependa nimkaribishe Mheshimiwa Kawambwa atembelee kiwanda kile aone jinsi kilivyo kikubwa na ninavyozungumza hapa au watu wengine wanasema Mheshimiwa Malangalila anajipendelea mambo ya Mufindi Kusini tu. Kile kiwanda kinaajiri Watanzania wote. Mimi hapa nazungumza kwa niaba ya kiwanda cha Watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sijui niseme nini. Nataka kusema kwamba nadhani Wizara ya Miundombinu imenielewa. Nimesema kwamba kama hataitambua

barabara hii mimi nitatoa Shilingi, sina kigugumizi. Nitaomba Waheshimiwa Wabunge pia mnunge mkono kwa sababu hii sio kiwanda cha Mufindi Kusini tu, ni kiwanda ambacho kinahudumia Watanzania wote. Tazama kama barabara hii ingekuwa inapitika vizuri, sasa hivi kile kiwanda kinachukua mkaa toka Zambia, inapita barabara ya Nyigo - Mgololo kilomita 60, sasa yale malori makubwa kama walivyosema wenzangu kwamba inatoka huko na mzigo mkubwa inapita mle inaharibu madaraja. Kwa hiyo, inabidi lizunguke mpaka Mafinga mpaka Mgololo kilomita 160. Sasa angalia tofauti kati ya kilometra 60 za kwenda Nyigo - Mgololo kuzunguka mpaka Mafinga mpaka Mgololo kilomita 100 tofauti ya kilomita 100. Sasa hapo hiyo tofauti inaonyesha kwamba kile kiwanda cha *MPM* tunakibebesa mzigo usio na sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imeweka pamba masikioni, hasa Wizara ya Miundombinu, haitaki kusikia kilio changu mimi kama Mbunge wa Mufindi Kusini, haitaki kusikia kama kilio cha Watanzania wote, nasema kwamba safari hii watasikia. Tazama, unajua yako mambo mengine tunayasoma katika vtabu vitakatifu kwamba, yuko maskini mmoja alikuwa hana chakula. Halafu yuko tajiri mmoja alikuwa anakula. Huyu maskini ilikuwa ni kuokota chembe chembe za mabaki zinazoanguka mezani kwa yule tajiri. Sasa mimi naokota chembechembe ambazo Wizara ya Miundombinu wanakula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tazama iko siku maana yake maishani hapa tunapita tu, wote iko siku tutalala. Nimesema kwamba mimi ninakula chembechembe kwa shida na njaa.

(*Hapa kengele ya pili ililia*)

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili Mheshimiwa Malangalila.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Nakushuru Mwenyekiti.  
(*Makofi/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Benito Malangalila na kwa kweli nikushukuru sana kwa ile tahadhari yangu, naona mpaka umemaliza mchango wako, Mheshimiwa Kaboyonga yuko salama kabisa hapa. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Namwita Mheshimiwa Elizabeth Batenga na Mheshimiwa Brig. Mstaifu Hassan Ngwilizi ajiandae.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie machache katika hoja iliyo mbele yetu. Napenda niwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Watendaji wote wa Wizara hiyo kwa hotuba nzuri iliyosomwa mbele ya Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakayoyazungumza moja ni pongezi na shukrani, lakini pia nitakuwa na maombi machache. Mimi napenda niipongeze Serikali kwa kuamua tena barabara ya Kagoma-Rusahunga kujengwa. Ni juzi tu tulihudhuria sherehe ya kutia saini mkataba wa ujenzi wa barabara hiyo pamoja na barabara nydingine. Mimi pamoja na wananchi wa Mkoa wa Kagera napenda nishukuru sana kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningeomba Serikali iwe makini sana, iwe karibu sana na mkandarasi huyu aliyetia saini. Kwa sababu barabara hii imesuasua muda mrefu. Mkandarasi wa kwanza aliywewka hakufanya vizuri akaondolewa, basi tukasota kwa muda wa mwaka nzima na zaidi.

Lakini pia kwa kuwa mkataba unasema itajengwa kwa muda wa miezi 36 inaanza leo na gharama yake nilivyoambiwa ni Shilingi bilioni 191 lakini ukiangalia katika fedha iliyotengwa ni Shilingi bilioni 19 tu kwa mwaka huu wa kwanza ambayo ninaihesabu ni kama asilimia 10 ya fedha yote iliyotengwa. Kwa hiyo, sasa sielewi katika miaka hiyo miwili mingine zitakuwa zinatengwa kiasi gani ili barabara hiyo iweze kujengwa katika muda uliopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niipongeze Wizara ya Miundombinu kwa kupandisha daraja barabara ya Mgakorongo – Kigarama mpaka Mrongo kuwa barabara Kuu. Kwa kweli napenda kuipongeza sana Serikali. Hii ni barabara ndefu inayoambaa mpaka wa nchi yetu na Uganda. Kwa hiyo, kwa hilo ninaishukuru. Lakini pia barabara ya Kyaka – Bukene mpaka Kasulu na yenye we imepandishwa kuwa barabara kuu na yenye we pia tunashukuru. Lakini kuna barabara nyingine ya Rutenge – Rubale – Izimbya – Ombwea – Buhamira mpaka Kishoju, ambayo inaunganisha Wilaya ya Muleba, Bukoba Vijijini na Karagwe. Kwa hiyo, ni barabara fupi na itatusaidia sana. Hii imepandishwa na kuwa barabara ya Mko. Barabara nyingine ni ya Mkumbo – Nyabushozi – Kabindi mpaka Nyantakara na hii pia imepewa kuwa barabara ya Mko, kwa hiyo, na yenye we tunashukuru na tunatarajia kwamba sasa zitaweza kutengenezwa kwa kiwango kile kinachotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ambayo mimi kwa jina ambalo ningependa iitwe ni barabara ya Usagara – Geita – Bwanga mpaka Kalebezo. Hiyo barabara kwa sababu ambazo hazieleweki, ilipofika Bwanga haikuendelezwa. Kwa hiyo, kuna kipande cha barabara kutoka Bwanga kwenda Lunazi hadi Kalebezo kilomita chache kutoka Biharamulo mjini.

Barabara hii kwa kweli imekuwa, tungeita ni barabara yaani siasa. Kisiasa ina athari kubwa sana kwa sababu badala ya kuendeleza hiyo ikaisha, hata hivyo tunashukuru kwamba hiyo barabara ya Mko ambayo ilijengwa kutoka Bwanga hadi Kyanyora na yenye we inatusaidia.

Lakini pia kwa sababu hii ni sehemu ya *trunk road* sehemu ya barabara kuu ambayo ingekwenda kuungana na ile ya kutoka Kagoma kwenda Lusahunga, hajatengenezwa, basi watu wanajiuliza ni kwanini? Hata katika Bodi ya barabara tulilizungumza hili na Meneja wa *TANROAD* kwa kweli aliliona na akasema kwamba atalishughulikia au litakuwa katika mipango ya baadaye. Kwa hiyo, nilikuwa ninaiomba Wizara ilishike hilo huenda pengine Mheshimiwa Waziri hajatembelea kule hata Naibu hajatembelea kule, haielewi hii barabara, lakini kama itawapendeza, basi tunawenza tukawapeleka wakaona ukweli na uhalisi wa hali halisi ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho nilikuwa naomba kuzungumzia ni uwanja wa ndege wa Bukoba. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba kazi ya ukarabati imeanza. Lakini ningependa kumwambia kwamba haijaanza kwa sababu mimi ni mwezi uliopita tu nilikuwa Bukoba kwa hiyo, nimeona haijaanza. Ila tunashukuru kwamba fidia kwa watu ili kupisha ukarabati kweli wengi wamelipwa na huenda kuna wengine ambao hawajalipwa, lakini ukarabati haujaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu uwanja sisi tungependa kuona unatengenezwa katika muda mfupi inavyowezekana, kwa sababu sisi tunajiuliza, hivi Mheshimiwa Rais kuja akatua Geita, akasafiri kilometra 300 kwenda Bukoba, ina maana gani? Makamu wa Rais, anakuja anatua Geita, anasafiri kwa barabara kilometra 300 na zaidi kwenda Bukoba na hata wakati wa kuondoka. Sasa watu wanajiuliza hivi sisi tunaopanda ndege hapa, roho zetu ni tofauti na za wale viongozi wetu? Kwa hiyo, nilikuwa naomba huu uwanja wetu wa ndege utengenezwe kwa kiwango ambacho kinatakiwa kama Mheshimiwa Waziri alivyoeleza katika Hotuba yake.

Lakini swalii, hivi uwanja wa Mpanda na uwanja wa Bukoba ni wapi na wapi mpaka viwanja hivyo viwiwli vibebane katika *vote* moja au *sub vote* moja? Ni kwanini? Kwanini kila uwanja usipewe kiwango chake hata kama ni Sh. 10,000/= tukajua Bukoba tumepewa Sh. 10,000/= *talken figure* tukaielewa hivyo? Je, kama hatuoni kazi zinaendelea si tutasema kwamba unajengwa uwanja wa Mpanda kwa sababu ni kwao Mheshimiwa Waziri Mkuu? Kwa vyovyyote vile tafsiri itakuwa hivyo, kwasababu wameviunganisha. Kwa hiyo, naomba hizi fedha zilizotengwa, Shilingi bilioni 4.5, basi watugawie Bukoba tujue ni kiasi gani na Mpanda nao wajue ni kiasi gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo ninaomba Wizara au Serikali iwaonee au ione umuhimu wa kuwasaidia watu wa Mkoa wa Kagera kwa kuangalia usafiri wao wa meli. Hata ungetengeneza barabara pamoja na *MV Bukoba* iliyozama, lakini bado tunapanda meli na bado tunahitaji meli kwasababu ya huduma zake. Ni njia rahisi ya usafiri, ni njia rahisi ya kubeba mizigo.

Mheshimiwa Waziri amesema kwamba *MSL* ina changamoto hiyo ya hiyo *MV Victoria*, lakini tusiishie hapo tu, itafute mbinu. Hivi kweli kwa watu walio pembezoni kule, Serikali haiwezi ikajikakamua ikanunua meli mpya nzuri na watu wale na wenyewe wakaona wako Tanzania?

Lakini pia hapo awali huduma za treni na huduma za meli zilikuwa zimeunganishwa pamoja, mtu angeweza kusafirisha mzigo kutoka Dar es Salaam moja kwa moja hadi Bukoba, angeweza kusafirisha mzigo moja kwa moja kutoka Dodoma kwenda Bukoba, lakini sasa hivi baada ya kampuni hiyo mliyoiweka kuendesha reli, sasa hivi utaratibu huo haupo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba huduma zote zilizokuwa zinapatikana kipindi kile, reli na meli zikiwa zinafanya kazi pamoja basi utaratibu huo urejeshwe ili watu waendelee kupata huduma ambazo wanazitarajia. (*Makofi*)

Mheshimiwa mwenyekiti, kwa kuwa sikuwa nimeandaa mambo mengi, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. BRG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kuniona. Lakini vilevile nampongeze Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri ambao amejaribu kutueleza hapa juu ya utekelezaji wa Ilani ya CCM, Ilani ambayo mimi naamini imetekelvezwa vizuri na wana-CCM katika hilo hatuna haja ya kuona aibu. Lakini kabla sijaendelea na yale niliyotaka kuyasema kuhusiana na mchango wangu, kwanza niwapongeze ndugu zangu wa Jimbo la Mlalo kwa kazi nzuri wanayoifanya ya utekelezaji wa Ilani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu wa Mlalo hawakuwa nyuma katika kutekeleza suala la elimu. Hivi sasa katika Jimbo la Mlalo tuna sekondari 26, hiyo ni wastani wa kila Kata kuwa na zaidi ya Sekondari mbili. Aidha, niwapongeze ndugu zangu wa Mlalo katika utekelezaji wa ujenzi wa zahanati na vituo vya afya, kujichimbia barabara zao zile za vijiji na napenda tu kuwahakikishia kwamba barabara ya Mlalo kwenda Mng'aro sasa imechukuliwa ni barabara ya Mkoa na inatengenezwa kwa kiwango kizuri kabisa. Najua sasa hivi tunalo tatizo la njaa kule Mlalo, tuna tatizo la njaa kwenye Kata za Mng'aro, Mnazi, sehemu za Sunga na baadhi ya sehemu za Kata ya Mlalo. Tunajua kwamba chakula kilitolewa na cha ziada kimeombwa, kwa hiyo, nawaomba ndugu zangu wale ambao wana matatizo ya njaa wavute subira kwasababu hayo yameshafikishwa kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiwe mtovu wa shukrani, namshukuru Mheshimiwa Waziri na *TANROADS*. *TANROADS* wamejitahidi sana katika utekelezaji wa barabara katika Wilaya yetu ya Lushoto na hususan katika Jimbo la Mlalo. Najua kwamba kazi bado inaendelea, kuna maeneo bado yanahitaji kutengenezwa zaidi, lakini naamini kwamba kwa uongozi wa *TANROADS* tulionao, malengo yake yatakuwa yamefikiwa. Najua kwamba barabara ya Mbaramo kwenda Mlalo imekuwa ni kilio cha muda mrefu cha wananchi wa Kata ya Mbaramo, lakini kama wanavyojua Mheshimiwa Rais alishalitolea uamuzi hili wakati wa ziara yake ya mwaka jana kwamba barabara hiyo ni lazima ijengwe na watu wa mazingira wanaohitajika kufanya *environmental impact assessment*, basi wahakikishe wanakwenda kuona ni jinsi gani mazingira hayataathirika lakini barabara ile ni lazima ijengwe katika kuwaokoa ndugu zetu wa Kata ya Mbaramo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalizungumza hili kwa sababu nimekwishawasiliana na Wizara na Waziri anayehusika na Mazingira amesema kwamba atalifuatilia suala hili ili ihakikishwe kwamba *environmental impact assessment* inafanyika ili barabara hiyo iweze kujengwa haraka iwezekanavyo. Ninachohitaji kumwomba Mheshimiwa Waziri ni kwamba Mheshimiwa Rais, alitoa ahadi hii mwaka 2008 Julai na sasa tayari tuko mwaka 2009 Julai. Isije ikafika tena mpaka mwaka 2010 tukawa tunaendelea kuulizana juu ya *environmental impact assessment* hiyo. Wananchi wa Mbaramo wameteseka vya kutosha na wanahitaji kuondolewa kero ambayo inawakabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niingie kwenye suala la Miundombinu. Kwanza nampongeze sana Mheshimiwa Waziri. Nimekuwa nikisikiliza wachangiaji kadha wa kadha wakilaumu, mimi nataka kumhakikishia Mheshimiwa Waziri kwamba pamoja na lawama hizo lakini asikate tamaa. Asikate tamaa kwa sababu suala la miundombinu

katika Taifa lolote ni suala la kufa na kupona. Wamekuwepo Mawaziri kabla yake, walikuwa wanalaumiwa hivi hivi na hata baada ya yeze kuondoka lawama hizi zitaendelea kwa sababu mwenye shida ndiye anayejua shida hiyo iko kiasi gani. Wote hapa tunakumbuka ndugu zetu wa Mikoa ya Kusini walivyokuwa wanalamika juu ya barabara ya kuelekea Lindi na Mtwara. Sasa hivi kilio kile hakipo tena, imebakia kero ya kutoka Mtwara hadi Lindi kuelekea Songea. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ndio maana nikasema usikate tamaa. Ndugu zetu hawa wa Mikoa ya Magharibi wanapolalamika, wanalamika kwa sababu ni tatizo, hakuna nchi yoyote ambayo inaweza ikaendelea bila miundombinu madhubuti. Mimi ninaamini kwamba suala la reli, suala la barabara kuelekea Magharibi ni suala ambalo lazima lipewe kipaumbele. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua yamezungumzwa hapa kwamba mbona barabara fulani ndizo zinazopewa kipaumbele, imetajwa barabara ya Chalinze kuelekea Segera na kadhalika, hiyo naamini ni sawa, lakini vile vile ni lazima tuangalie Mikoa hii ya Magharibi, kwa sababu hatuwezi kufanya maendeleo yoyote katika nchi yetu hii bila ya kuhakikisha kwamba Magharibi imefunguka. Sasa Magharibi hii inafunguka vipi? Pamoja na kwamba sasa hivi tunazungumzia barabara, lakini ukweli ni kwamba, barabara sio kitu cha kuaminika kubeba mizigo mizito. Reli ndio ambayo imekusudiwa kubeba mizigo mizito. Kwa hiyo, ni lazima tuangalie tuweke umuhimu katika kuhakikisha reli yetu ya kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma kwenda Mwanza, kwa kweli iko katika hali ya kuweza kumudu mizigo inayotoka Magharibi na sio tu kujenga reli, nakumbuka Mheshimiwa Rais, amezungumza juu ya kupanua reli. Hiyo haina mjadala, ni lazima reli hii tuipanue kwasababu *gauge* tunayotumia sasa hivi ni ya kwetu ya *East Africa* tu sio *Internatinal*.

Pili, ni lazima tujitayarische kui-*electrify*, tutumie umeme kwenye reli hiyo. Tatu, ni lazima tujitayarische na nitashukuru kama wenzetu wanaohusika na mipango watalizingatia hilo. Sasa hivi tunazungumzia reli moja, lakini kwa kweli tunahitaji *double lines*. *Double lines* kwa maana ya kwamba ikitoka Dar es Salaam kwenda Kigoma, kwenda Mwanza na yule anayetoka Kigoma na Mwanza basi ma-treni haya hayapishani, hayangojani. Hivyo ndivyo ambavyo tunaweza tukasema kwamba mipango yetu ya reli itawenza kustahimili hata kwa zaidi ya miaka 100 zaidi ijayo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tufikirie suala la kujenga reli kutoka Mtwara kwenda *Mbambabay*. Tupende tusipende tunajua kwamba reli hiyo ni lazima itakuja kujengwa na jinsi tunavyozidi kucheleva ndivyo jinsi ambavyo gharama zitazidi kupanda. Tupende tusipende reli ya kutoka Tanga kwenda Musoma itabidi ije ijengwe na wakati wa kujenga ni sasa. Vilevile ni lazima tuunganishe Tunduma – Sumbawanga mpaka Kigoma sio kwa barabara tu, na reli vilevile ni lazima tuweke huko. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanja vya ndege, sasa hivi tunazungumzia tuna Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza na huu wa Songwe. Lakini ni lazima tujenge uwanja ule wa Mtwara. Ruvuma, ni lazima, sehemu za Songea tuje tujenge uwanja tupende tusipende. Bandari ni lazima, bandari ya Dar-es-Salaam tuiwekee mikakati. Jana nilikuwa nasoma kwenye gazeti wenzetu wa Mombasa wamechukua mkopo wa dola milioni 200

kwa ajili tu ya bandari ya Mombasa mbali na ile ya Lamu wanayojenga. Hiyo yote ni katika kujitayarisha kushindana kibiashara na Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika dunia hii aliyewahi amewahi, sisi tukijazinduka kwamba sasa ndio tunahitaji tutengeneze bandari vizuri Tanga na Mtwara, wenzetu watakuwa wamekwishatupiku katika biashara na haitakuwa rahisi kuja kuwabadilisha hao ambao sasa hivi wanafuatwa na biashara hizo, kwa maana ya wenzetu wa Uganda, Rwanda, Burundi, kongo, kama wameshazoea njia hiyo, basi itakuwa ndio njia yao ya kudumu. Sisi tutabakia tu ooh, wenzetu hawa hawatupendi. Yote haya maana yake ni lazima mipango iwekwe.

Najua mwaka jana tulielezwa kwamba itakuwepo Tume ya Mipango. Najua kwamba sasa fedha zimeanza kutengwa, mimi sijui kama Tume yenye ya Mipango imeshachaguliwa ama vipi, lakini la msingi ni kwamba nchi haiwezi kuendelea hivi bila mipango. Hata sasa hivi matatizo hayo unasikia Waheshimiwa Wabunge hawa wanazungumza, ni kwa sababu mipango yetu tunangojea mpaka tuje tuelezw hapa Bungeni, hakuna kinachoeleweka kwamba mipango hii, *strategic plan* yetu ya miundombinu katika nchi hii iko vipi. Inakuwa *treated* kama *top secret*. Sasa hakuna *top secret*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Miundombinu. Kwanza na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Idara za barabara kwa maana ya TANROADS, Meneja wa TANROADS Mkoo wa Pwani, lakini pia hata Msimamizi Mkuu wa TANROADS Taifa, ndugu yetu Mrema, kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuhakikisha masula ya barabara yanakwenda kama vile inavyotakiwa na matarajio ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuzungumzia Utaifa. Mwelekeo ninaouona sasa hivi kwenye mambo ya maendeleo hatutilii mkazo utaifa kwanza. Wapo wachache wanaweza kuona utaifa kwanza, lakini pia wapo wengine wanaona kwanza nipate mie, utaifa baadaye. Kwa sababu ni kweli sisi ni Wawakilishi wa wananchi na kila mmoja yupo kwa ajili ya kuhakikisha wananchi waliomchagua anawasemea hapa Bungeni. Lakini hata Serikali pia isikie kilio cha Mbunge ili wananchi wapate mafanikio ya Mbunge wao na waridhike na kazi waliyomtuma hapa Bungeni. Lakini tofauti kubwa ninayoiona sasa hivi ni pale ambapo Mbunge mmoja anaweza akasimama akaelekeza kuwa barabara hii sasa iachwe, lakini ielekezwe barabara hii upande anakofanyia yeye kazi upande wa kwake. Hatuwezi kufanya kitu kama hicho! Ni hatari sana na ni jambo ambalo halijengi mazingira mazuri kwa yule Mbunge ambaye barabara yake inaambiwa sasa ni hapana. Huo ndio ninaosema ni umimi kwanza na sio utaifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumzia utaifa ni kwa sababu barabara inapojengwa, ni imani yangu barabara ile magari yatakayopita pale ni kwa ajili ya maendeleo ya Tanzania; Wananchi watakaoitumia barabara ile ni Watanzania; lakini

hatimaye pato litakaloingia ni la Taifa kwa ujumla na wananchi wote tunategemea barabara kwa maana ya maendeleo. Mfano upanuzi wa barabara ya Chalinze – Segera. Chalinze ni katikati, anayekwenda Dar es Salaam anayekwenda Tanga, Kilimanjaro, Arusha, hatimaye nchi ya jirani Kenya na Uganda. Sasa unapoizungumza barabara ile ni kwanini ipanuliwe lakini kubwa ni kwa ajili ya pato la Taifa kwenye sekta ya barabara. Atakayepita kwenye barabara ile sio wananchi wa Chalinze, sio wananchi wa Tanga, sio wananchi wa Kilimanjaro, sio wa Arusha, lakini yejote yule hata kama ni Mganda atatumia barabara ile maadam tayari ameshaingiza pato la Taifa. Hicho ndicho ambacho tunataka kukifanya sisi Wabunge kutetea Taifa letu. Ni utaifa kwanza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunapozungumzia ujenzi wa barabara hizi ni pamoja na zinapotengenezwa, yaani zinapojengwa, lakini ni lazima baadaye zifanyiwe matengenzo na matengenezo ni muhimu. Lakini tukubaliane barabara hiyo iliyojengwa kama ikiwa ni miaka 20 iliyopita au miaka 15 iliyopita, wafadhili wakiwa wamepatikana kwa ajili ya kuifanya matengenezo, shida inakuwa wapi? Wafadhili tuwaambie nini? Kwa hiyo, kwa namna moja au nyingine tufikie hatua ndugu zangu tukubaliane kwamba maslahi ya Taifa yawe mbele kuliko umimi kwanza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini iko hadithi moja ya mtu mmoja kakaribishwa chakula, baada ya chakula kwisha alipoambiwa sasa, mzee tukuletee maji? Akasema aah, hapana bwana tumbo limejaa. Mzee sasa tukupe Fanta? Akasema aah, sukari nyingi. Je, Pepsi? Gesi. Aah! Sasa mzee hapa vinywaji vimekwisha, tukuletee nini hapa? Naona vinywaji vilivyobaki hapa ni bia za baridi? Akasema hiyo hiyo, barabara! Nilettee moja baridi. Sasa inafikia mahali hutaki lakini vingine unavitaka vya baridi. Hayo ndio ambayo yanaonekana sasa hivi. Tunazungumza huku isiende, huku ondoeni, lakini baadaye wakikuambia sasa mzee tunakumegea kidogo, umetulia. Lakini pia ipo dhana ya watu kunyamazishwa, wanaweza wakaja na spidi kubwa hapa. Lakini baadaye wakishapoozwa, aah, ndio hivyo tena *Alhamdulillah*, mtu anajikuta tayari sasa amesharidhika, sio yule uliyemwona asubuhi au uliyemwona jana akilalamikia suala fulani. Sasa ndio hayo tunayoyasema, sio utaifa, ni umimi. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, naishukuru Serikali kwa kuipandisha hadhi barabara ya kutoka Lugoba – Tukamisasa – Ubena. Barabara hii ilikuwa ni ya Halmashauri na kipato cha Halmashauri yetu ya Bagamoyo, kwa kweli kilikuwa ni kidogo sana na hakiwezi kuhimili vishindo vya matengenezo ya mara kwa mara ya barabara ile. Namshukuru Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake baada ya kutilia umuhimu pamoja na barabara nyingine zote ambazo zimepata hadhi, sasa hivi na Wabunge wengi wameshukuru kuhusu jambo hilo na mimi nina haki ya kumshukuru Mbunge pacha wangu na Watendaji wake kwa kuiona barabara hiyo na kuipandisha hadhi kuwa sasa ya Mkao. Lakini pia nashukuru na maeneo mengine yote ambayo barabara zao zilikuwa za Halmashauri, lakini sasa zimepata hadhi kuwa za Mikoa na zile ambazo zimepata hadhi kuwa za Taifa. Lakini ni jitihada kubwa wanazozifanya wenzetu hawa kwenye Wizara hii ya Miundombinu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi juzi tulifanya uzinduzi wa daraja lile la Ruvu, daraja lile ni kiungo kikubwa sana cha maendeleo nchini. Wananchi wote wa Tanzania

na ambao sio wa Tanzania, walipongeza sana daraja lile kumalizika kwani ni kiungo kikubwa cha biashara na pato la Taifa letu. Mapato mengi yanayoingizwa hapa nchini daraja lile ni kiungo. Lakini sasa wakati umefika kuitazama barabara ya Morogoro nayo, itakapokuwa imewezezeka, basi nayo iweze kupanuliwa kwani ni kiwango pia cha kuingizia pato la Taifa. Lakini naomba sasa watendaji sasa msiiite Chalinze – Dar es Salaam, anzeni kuiita Dar es Salaam – Chalinze; maana ikitajwa Chalinze – Dar es Salaam kuna mstuko kidogo wa wananchi na baadhi ya watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tuzungumzie tunapohitaji kujenga barabara zetu. Tufikie hatua sasa Serikali iweke malengo kwamba katika kipindi cha miaka miwili itazame ni maeneo gani sasa yanayostahili barabara zijengwe. Katika kipindi cha miaka miwili mingine waelekeze nguvu sehemu gani? Badala ya sasa hivi kupeleka fedha robo robo humu kwenye maeneo ya barabara hizi na hatimaye muda unaisha zile hela hazitoshi na wakandarasi wetu ndio hao tunawasema, hatimaye zile barabara zinashindwa kukamilika kwa wakati husika kwa maana ya kwamba fedha zinatolewa kidogo kidogo mno kwenye hizi barabara. Lakini tukijipanga tukasema sasa mwaka huu ni Kusini, mwaka huu Kanda ya Ziwa, mwaka huu Kaskazini, inaweza kuleta uwiano wa kuzimaliza hizi barabara kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la kivuko kile cha Kigamboni. Kivuko kimepatikana, wananchi sasa wapo kwenye furaha kuondokana na yale matatizo yaliyokuwa yanawakabili mara kwa mara. Lakini sambamba na kivuko kile, wananchi bado wanalamikia daraja, daraja ni muhimu sana. Nalisema hilo kwasababu hata wale wanaotumia kile kivuko kwa kule Kigamboni sio watu wa Dar es Salaam peke yake, ni wa nchi nzima. Sasa ni muhimu sana suala la daraja litiliwe mkazo sana. Lakini naiombe Serikali sasa, katika kuongeza pato la Taifa, kama kivuko cha Kigamboni ukiingia pale na *Saloon car* ni Sh. 800/=, hizi gharama ni kubwa sana kwa mwananchi wa kawaida. Inabidi tutazame, wenzetu wa Serikali waangalie hii hali. Kwa sababu kwa mtu wa kawaida Sh. 800/= kwenda na kurudi ni nyingi. Yapo magari mpaka Sh. 2,000/= au Sh. 1,500/= nafikiri. Sasa kama tunafikia hivyo, basi hata baadhi ya maeneo mengine yenye vivuko au yenye madaraja makubwa, kama suala ni kuongeza pato la Taifa katika sekta ya barabara, basi na muanze kuchaji magari yanayopita kwenye maeneo hayo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo nchi ambazo madaraja mengine unachajija ukipita pale. Kwa maana ya kwamba labda unalipia Sh. 2,000 gari lako, lakini hatimaye ni pato linaongezeka kwenye Taifa. Mfano daraja la Ruvu, tukififikia hatua kwa kipindi cha miaka miwili au mwaka mmoja kwa magari yote yanayopita pale pamoja na kupata hizi fedha kupitia kwenye mafuta, yapo magari mengine yanajaza mafuta kwenye nchi zao huko hawawezi kuchukua mafuta hapa nchini. Lakini tukianza kutoza ushuru kwenye magari kwa kutumia madaraja yetu kama hata yale magari yanayotoka nje, itakuwa ni moja ya pato la Taifa na hatimaye tunaweza tukajazia hizi pesa na zinaweza zikajenga baadhi ya barabara nyingine hizi ambazo zinalalamikiwa hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Wizara ya Miundombinu ifikie sasa hatua ya kuangalia mlundikano wa makontena pale Dar es Salaam. Wakarabati ile reli ya kutoka Dar es Salaam kuja Ruvu hapa na eneo lile la Ruvu pale mpaka Vigwaza ni eneo

kubwa sana. Kwanini wasianzishe *terminal* nyingine pale kwa ajili ya makontena hatimaye magari yanayotoka nje yasiingie Dar es Salaam na kuondokana na msongamano usiokuwa na sababu yoyote?

Magari yanayotoka nje yanayotoka mikoani yakifika Ruvu, eneo la Vigwaza, liko wazi Serikali iamue tu, lichukue makontena yale baadaye warudi huko makwao walikotoka badala ya kuingiza msongamano wa magari makubwa Dar es Salaam. Yale magari yanayoingia Dar es Salaam ni ya tani kubwa kiasi kwamba barabara za Mkoa za Dar es Salaam hamkuzijenga kwa umahiri wa magari ya tani hizo ambayo yanaingia. Tatizo liko wapi? Wekeni *terminal* pale, imarisheni ile reli, makontena yatoke Dar es Salaam yapelekwe Ruvu na hatimaye wenye magari sasa wachukue makontena yao na kurudi mikoani. Ni mipango tu na inawezekana. Kwa hiyo, nilikuwa naishauri Serikali pale itakapokuwa imeona suala hili linafaa, basi iweze kutilia maanani sana kuhusu suala la kuondoa msongamano na hatimaye kuweka maendeleo kwenye maeneo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii, lakini pia nazidi kuwashukuru Watendaji wote akiwemo Mheshimiwa Waziri na awe na moyo kama huo kwani yote haya yanayofanyika ni *challenge* ya kazi yake hiyo. Nakushukuru, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, namshukuru Mheshimiwa Ramadhani Maneno kwa mchango wake. Baada ya kuwasiliana na wachangiaji wanaofuata, wameomba niwape muda ulio kamili kwa siku ya kesho.

Kwa hiyo, ninaomba niseme kwamba katika orodha ile ya wachangiaji ambao hawakupata kuchangia hata mara moja, orodha niliyobakiwa nayo hapa inanionyesha nimebakiwa na wachangiaji wanne. Mheshimiwa Nimrodi Mkono, kwa hiyo, kama kesho tutaanza kuchangia atakuwa mchangiaji wa kwanza, Mheshimiwa Ephraim Madeje, atakuwa mchangiaji wa pili. Mheshimiwa tatu Ntimizi, atakuwa wa tatu na tutamalizia na Mheshimiwa Getrude Lwakatare.

Baada ya hapo tutaanza na wale ambao wamekwishakuhangia mara moja na kwa mujibu wa orodha niliyonayo hapa Mezani tunaye Mheshimiwa Lucas Selelili, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Juma killimba, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Omar Kwaang'w na wengine wanaoendelea kwa kutegemeana na muda kadiri utakavyozidi kuturuhusu.

Sasa kabla sijaahirisha shughuli za Bunge leo jioni Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niseme neno moja. Toka nilipokaa kwenye Kiti asubuhi na hasa wachangiaji walipoanza kuchangia, kila aliyekuwa anachangia ama alianza kwa kuniletea hapa *kiji-memo* akilalamika kwamba mimi nilikuwa wa kwanza kuomba ni kwanini nimekuwa watatu? Watatu naye anasema mimi nilikuwa wa kwanza kuomba kwanini nimekuwa watatu? Kwahiyoo, kila mmoja kati ya hao wote waliochangia karibu takribani watu sita kila mtu anasema ye ye aliokuwa wa kwanza kuomba.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, nadhani tukubaliane. Utaratibu tunaoukuta hapa Mezani ndio utaratibu ambao umepangwa na kila mtu atapewa nafasi kwa mujibu wa taratibu iliyopo. Kama kutatokea matatizo makubwa, Meza itachukua nafasi ya kuyarekebisha kama vile nilivyofanya kwa Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni. Kwa hiyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, ninaomba mwelewe hivyo na kwa kweli tunazingatia. Lakini kwa mujibu wa Kanuni inatupasa wakati mwingine kuchanganya jinsia, pande zote za Muungano na maeneo tofauti ya nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, ninaomba tukubaliane hilo, ndio uendeshaji mzuri wa shughuli za Bunge ndani ya Bunge letu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo, naomba nichukue nafasi hii niwashukuruni sana kwa shughuli za leo. Kwa kweli mmetimiza wajibu wenu kwa kiasi cha kutosha kabisa na mmesaidia kushauri mambo ya msingi kabisa katika Wizara yetu ya Miundombinu na kwa mujibu wa ratiba yetu, tutaendelea na Wizara hii tena kwa siku ya kesho. Kwa hiyo, baada ya shughuli nzito ya leo, ninaomba nichukue nafasi hii sasa kuwatamkia kwamba ninaahirisha shughuli za Bunge leo mpaka kesho saa tatu asubuhi, ndani ya Ukumbi huu. Asanteni sana.

*(Saa 1.37 Usiku, Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 2 Julai, 2009 Saa 3.00 Asubuhi)*